Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

# BUNGE LA TANZANIA

## MAJADILIANO YA BUNGE

## MKUTANO WA KUMI NA SABA

## KIKAO CHA NANE - TAREHE 11 NOVEMBA, 2004

*(Mkutano Ulianza Saa tatu Asubuhi)*

## D U A

*Spika (Mhe. Pius Msekwa) Alisoma Dua*

## HATI ZILIZOWASILISHWA MEZANI

Hati zifuatazo ziliwasilishwa mezani na: -

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. ABDISALAAM ISSA KHATIBU):**

Taarifa ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kwa mwaka ulioishia tarehe 30 Juni, 2003, *(The Report of the Controller and Auditor General for the year ended 30th June, 2003).*

Taarifa ya Mwaka na Hesabu za Benki ya Raslimali Tanzania kwa mwaka 2003 *(The Annual Report and Accounts of the Tanzania Investment Bank Limited for the year 2003).*

Taarifa ya Mwaka na Hesabu za Benki ya Posta Tanzania kwa Mwaka 2003 *(The Annual Report and Accounts of the Tanzania Postal Bank for the year 2003)*

Taarifa ya Mwaka na Hesabu za *Parastatal Pensions Fund* kwa mwaka 2003 *(The Annual Report and Accounts of the Parastatal Pensions Fund for the year 2003).*

## MASWALI NA MAJIBU

Na. 100

### Uboreshaji wa Barabara za Mjini

**MHE. HAMISI JUMANNE NGULI** aliuliza: -

Kwa kuwa Serikali sasa inajitahidi kujenga barabara kuu karibu zote kwa kiwango cha lami; na kwa kuwa barabara hizo kuu huishia nje kidogo ya miji au hupitia nje ya mji; na kwa kuwa mpaka sasa barabara za mijini ni mbaya au ni chache zenye lami: -

Je, Serikali ina mpango gani wa kuziboresha barabara za mijini pia kuziweka katika kiwango cha lami Kitaifa ili kwenda sambamba na uboreshaji wa barabara kuu?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA** alijibu: -

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Hamisi Jumanne Nguli, Mbunge wa Singida Mjini, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, Serikali inatambua hali ya uchakavu na pia haja ya kuimarisha barabara za mijini ili ziweze kumudu ongezeko la magari na kurahisisha usafiri mijini. Katika kutekeleza azma hii Serikali kuanzia mwaka 1998 - 2004, imekarabati kilometa 102 kwa kiwango cha lami kwa gharama ya shilingi bilioni 25 katika Manispaa ya Arusha, Tanga, Morogoro, Iringa, Mbeya, Tabora na Mwanza chini ya Mradi wa Uimarishaji wa Huduma Mijini *(Urban Sector Rehabilitation Project) (USRP)* unaogharimiwa kwa pamoja na Serikali yetu, Serikali ya Ujerumani, Serikali ya Ireland, Serikali ya Uingereza, Serikali ya Uholanzi na Benki ya Dunia.

Mheshimiwa Spika, Serikali kwa kutumia fedha za Mfuko wa Barabara kwa ajili ya matengenezo ya barabara za Halmashauri kati ya mwaka 2001/2002, Serikali imetumia jumla ya shilingi milioni 3935.2 kuzifanyia matengenezo barabara kwa kiwango cha lami katika Manispaa za Dodoma, Mbeya, Kinondoni, Miji ya Babati na Kibaha na majiji ya Mwanza na Dar es Salaam.

Aidha, katika mwaka huu wa fedha Serikali imepanga kuimarisha barabara za lami katika Manispaa za Arusha, Dodoma, Iringa, Morogoro, Moshi, Mbeya, Tabora, Temeke, Ilala, Kinondoni, Shinyanga na Jiji la Mwanza kwa kuziongezea tabaka la lami *(re-sealing),* kwa kutumia fedha kutoka Jumuiya ya Ulaya chini ya mpango wa *EDF 9* jumla ya shilingi milioni 2999.27 zitatumika kutengeneza kilometa 39.04 za barabara katika miji hiyo.

Mheshimiwa Spika, Mji wa Singida una barabara za lami zenye urefu wa kilometa 7.6, kati ya hizo kilometa 3.8 ziko katika hali nzuri na Wizara yangu imekuwa ikizifanyia matengenezo ya kwaida ili kuhakikisha barabara hizi haziharibiki. Katika mwaka huu wa fedha Serikali imetenga shilingi 2,330,000/= kwa ajili ya matengenezo ya kawaida ya barabara hizi. Kilometa 3.8 zilizo kwenye hali mbaya zinahitaji matengenezo makubwa.

Aidha, Halmashauri ya Mji wa Singida, imepanga kujenga barabara ya Boma yenye kilometa 1.2 kwa gharama ya shilingi milioni 200 kutoka kwenye Mpango wa Miaka Mitatu ya Kukarabati Barabara za Halmashauri pale mpango huu utakapopata

fedha. Kwa mwaka wa fedha 2005/2006 inapanga kuzifanyia matengenezo makubwa barabara za lami za soko, Lumumba na Standi zenye urefu wa kilometa 1.88 kwa gharama ya shilingi milioni 376.

Mheshimiwa Spika, Ofisi yangu kwa kushirikiana na Serikali ya Norway chini ya Shirika lake la Kutoa Misaada *NORAD* inaandaa mpango wa kukarabati barabara za Halmashauri. Mpango huo utakaojulikana kama *National Rural Transport Programme (NRTP)* utahusika na ukarabati wa barabara za Halmashauri za Wilaya na Miji ukiwemo Mji wa Singida. Mpango huu ukikamilika unategemewa kuanza kutekelezwa mwaka 2007 ukigharamiwa na Serikali ya *NORAD* na wafadhili wengine.

Mwisho kwa kupitia Bunge lako Tukufu naomba kutoa shukrani kwa Serikali ya Norway kwa kushiriki katika utayarishaji wa *NRTP* na kukubali kwake kuwa Mfadhili Kiongozi *(Lead Donor)* katika utekelezaji wake.

**MHE. HAMISI JUMANNE NGULI:** Mheshimiwa Spika, kwa kuwa katika barabara zetu nyingi za Halmashauri hizi ambazo zimejengwa kwa kiwango cha lami zinakuwa na ubora tofauti tofauti; aidha, labda kwa sababu ya pesa, ukiacha hizi ambazo zinapewa ufadhili na mashirika ya Kimataifa.

Je, Serikali inasimamiaje ubora wa barabara hizi ili zisiwe na ubora tofauti tofauti kwa kila barabara inayojengwa katika Halmashauri moja au katika Halmashauri mbalimbali tofauti? *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Spika, matengenezo ya barabara hasa barabara hizi ambazo zinatumia kiwango cha lami zinajengwa hasa kwa mikataba kati ya wakandarasi pamoja na Halmashauri zinazo husika au Serikali kwa upande mwingine na kwa mujibu wa mikataba hii huwa wapo wasimamizi wanaopaswa kufanya kazi zao vizuri na ni dhahiri kabisa kwamba unapoona tatizo hilo lipo basi usimamizi haukuwa mzuri sana.

Lakini nia ya Serikali ni kutoa barabara ambazo ni za hali ya juu na tutaendelea kuhakikisha kwamba jukumu hilo tutaendelea kulitekeleza.

Na. 101

**Huduma za Afya**

**MHE ASHA A. NGEDE (k.n.y. MHE. MUTTAMWEGA B. MGAYWA)** aliuliza: -

Kwa kuwa huduma za afya zimeendelea kudorora katika Jimbo la Mwibara:-

(a) Je, Serikali ina mpango gani wa kumalizia ujenzi wa Kituo cha Afya cha Igundu, zahanati za Sunsi, Kisorya na Nansimo, ikiwa ni pamoja na kutoa vifaa na dawa katika kituo cha afya cha Kasahunga na zahanati za Iramba, Buramba na Busambara?

(b) Je, Serikali ina mpango gani wa kutoa gari la wagonjwa ili kuwaondolea wanawake wa Jimbo la Mwibara kero wanayoipata ya kutembea umbali mrefu kwenda kutafuta huduma ya afya?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA** alijibu: -

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Muttamwega Mgaywa, Mbunge wa Mwibara, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo: -

(a) Mheshimiwa Spika, kutokana na ufinyu wa Bajeti ya Serikali na uwezo mdogo wa Halmashauri, uimarishaji wa huduma za afya katika Wilaya ya Bunda unafanyika kwa awamu. Awamu ya pili ilihusisha ukarabati wa vituo vya Afya vya Igundu na Busambara. Ukarabati huu ulifadhiliwa na *Christian Social Service Commission (CSSC).* Ujenzi wa zahanati mpya ya Sunsi umefanywa na Halmashauri kwa kushirikiana na wananchi na ilikamilika na kufunguliwa mwaka 2000. Mpango wa upanuzi wa zahanati hii kwa kuongeza majengo upo katika mpango kabambe wa Afya wa mwaka 2004.

Mheshimiwa Spika, ukarabati wa zahanati ya Nansimo uliyofanywa kwa kushirikisha nguvu za wananchi ulianza mwezi Januari, 2004 na kukamilika mwezi Mei, 2004. Zahanati hii ilifunguliwa na Mheshimiwa Waziri Mkuu.

Mheshimiwa Spika, ukarabati wa zahanati ya Kisorya utafanyika mwaka huu kwa kutumia fedha za Mfuko wa Pamoja wa Afya *(Basket Fund)*. Ukarabati wa zahanati za Iramba na Bulamba ulifanywa na *Christian Social Service Commission* mwaka 1996/1997 na kukamilika mwaka 1997 na kuzinduliwa na Kiongozi wa Mbio za Mwenge wakati huo. Aidha, ukarabati wa Zahanati ya Karukere, Igundu na Busambara ulioanza mwaka 1999 ulifanywa pia na *Christian Social Service Commission* na kukamilika mwaka 2000. Zahanati zote zilizokarabatiwa zimepewa samani na dawa kupitia mpango wa Taifa wa Dawa Muhimu *(EDP)* kwa utaratibu wa *Kit.*

(b) Mheshimiwa Spika, Halmashauri ya Wilaya ya Bunda ina mpango wa kununua gari la wagonjwa kwa ajili ya kituo cha Afya kimojawapo katika Jimbo la Mwibara kwenye Bajeti ya 2004/2005. Ili kurahisisha usambazaji wa vifaa na dawa, gari moja aina ya *Canter* limeagizwa nchini Japan kupitia Shirika la Kuhudumia Watoto Duniani *(UNICEF)* na pia gari la wagonjwa kwa ajili ya Kituo cha Afya Ikizu limeombwa kupitia *WHO/NORAD.*

Pamoja na kutokuwepo kwa gari la wagonjwa kwa wakati huu, Serikali inaendelea kuboresha shughuli za rufaa kwa wagonjwa kwa kuimarisha huduma za mawasiliano. Halmashauri kwa kushirikiana na Shirika la Afya Duniani *(WHO)* na Shirika la Maendeleo la Norway *(NORAD)* imeboresha mawasiliano kwa kununua simu za upepo *(Radio Call)* na kufungwa katika Vituo vya Afya vya Ikizu, Kasahunga, Manyamanyama. Aidha, *Radio Calls* nyingine zimefungwa katika zahanati za Nansimo,

Mugeta na Fuba, Nyamatoke na Guta. *Radio Calls* nyingine zimefungwa katika ofisi ya Mganga Mkuu wa Wilaya, gari la Idara ya Afya la Wilaya pamoja na moja inatumika Idara ya Afya Wilayani.

Aidha *Radio Calls* nyingine zimefungwa katika Ofisi ya Mkurugenzi Mtendaji wa Wilaya na Ofisi ya Mkuu wa Wilaya. Madhumuni ya kufungwa kwa *Radio Calls* hizi katika maeneo haya ni kurahisisha mawasiliano na hivyo kurahisisha huduma ya afya.

**SPIKA:** Hili linahusu Jimbo la Uchaguzi la Mwibara, kwa hiyo nadhani mwenyewe ameshafika mimi nilikuwa nawataadharisha Wabunge wengine, Mheshimiwa Muttamwega Mgaywa, swali la nyongeza.

**MHE. MUTTAMWEGA B. MGAYWA:** Mheshimiwa Spika, kwa vile sasa hivi tuna mpango pia wa kujenga hospitali kwa ajili ya matunzo ya kina mama ambayo itaitwa *Mama Zetu Hospital,* inatarajiwa kujengwa katika Jimbo hilo hilo, je, Mheshimiwa Waziri atakuwa tayari kutu-*support* katika ujenzi huu ambao unaanza Januari mwaka ujao?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Spika, kwanza naomba nikupongeze wewe mwenyewe Mheshimiwa Mbunge, lakini pamoja na wananchi wa Jimbo na Wilaya kwa ujumla kwa jitihada hiyo nzuri ambayo inafanywa. Ninaloweza kukuomba sasa ni kwamba maadamu mmeshaingia katika ujenzi huo basi wasilisha jambo hili kupitia Wizara ya Afya ili tuweze kuona kama kuna namna ya kusaidiana na wananchi pamoja na wafadhili wengine.

Na. 102

**Umaskini**

**MHE. WILFRED M. LWAKATARE (k.n.y. MHE. HAMAD RASHID MOHAMED)** aliuliza:-

(a) Je, kutokana na *Vision* ya miaka 25 ya kuondoa umaskini, utakuwa umepungua kwa kiasi gani?

(b) Je, ni mambo gani yanayokwamisha umaskini usiondoke kwa kasi kama ile ya kuongezeka kwa Ukimwi?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS (MHE. EDGAR D. MAOKOLA-MAJOGO)** alijibu: -

Mheshimiwa Spika, kabla ya kujibu swali la Mheshimiwa Hamad Rashid Mohammed, Mbunge wa Kuteuliwa, lenye sehemu (a) na (b), ningependa kutoa maelezo ya awali kama ifuatavyo:-

Dira ya Taifa ya Maendeleo kufikia mwaka 2025 ina malengo makuu matano ambayo ni kuwa na jamii:-

(i) Yenye maisha bora na mazuri na iliyoondokana na umaskini uliokithiri;

(ii) Yenye amani, utulivu na umoja;

(iii) Iliyo na utawala bora na uongozi imara;

(iv) Iliyoelimika na inayopenda kujifunza zaidi; na

(v) Kuwa na uchumi imara wenye kuhimili ushindani.

Mheshimiwa Spika, Dira ya Taifa imefafanuliwa zaidi katika mipango na mikakati mingine ya maendeleo ya kisekta kuwezesha utekelezaji wake. Kwa upande wa kupiga vita umaskini, malengo ya Dira ya Taifa yamefafanuliwa katika Mkakati wa Kuondoa Umaskini ambao kwa hivi sasa unafanyiwa mapitio kwa nia ya kuboresha.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo hayo mafupi sasa ningependa kujibu swali la Mheshimiwa Hamad Rashid Mohamed, kama ifuatavyo: -

(a) Lengo la mkakati wa kuondoa umaskini ni kupunguza umaskini uliokithiri kwa asilimia 50 kufikia mwaka 2010 kwa lengo la kuondokana nao kufikia mwaka 2025 kama Dira inavyoelekeza.

(b) Mheshimiwa Spika, ni vigumu sana kulinganisha kasi ya kuongezeka kwa UKIMWI na kasi ya kupunguza kwa umaskini ingawaje kuna uhusiano kati ya umaskini na ongezeko la UKIMWI.

Nakubaliana na Mheshimiwa Mbunge kuwa kasi ya kupungua kwa umaskini ni ndogo. Takwimu za kisavei ya mapato na matumizi ya kaya zinaonesha kwamba idadi ya watu walio chini ya ulingo wa umaskini kwa mahitaji muhimu imepungua toka asilimia 38.6 mwaka 1991/1992 kufikia asilimia 35.7 mwaka 2000/2001. Kasi ndogo ya kupungua kwa umaskini inatokana kwa kiasi kikubwa na ongezeko dogo la uchumi hasa ukizingatia vile vile kuna kasi kubwa ya ongezeko la idadi ya watu.

Maeneo na sekta ambazo maskini wengi wanashiriki katika kutafuta kipato chao kama vile kilimo na sekta isiyo rasmi yamekuwa na ukuaji mdogo sana. Zipo sababu nyingi zinazokwamisha ukuaji katika maeneo haya. Sababu kuu ni pamoja na: -

(i) Teknolojia duni inayotumika na kutegemea mno hali ya hewa, hivyo kuwa na uzalishaji mdogo kutokana na tija ndogo.

(ii) Ukosefu wa miundombinu ya kutosha kama vile barabara na nishati na hivyo kukwamisha uwekezaji wa kuridhisha katika maeneo haya.

(iii) Upungufu wa huduma muhimu za jamii na za kiuchumi kama vile uchache wa huduma za mikopo na vyombo vya kifedha katika maeneo hayo na hivyo watu kukosa mitaji ya kuendeshea shughuli zao.

(iv) Kutokuwepo kwa masoko ya uhakika kwa bidhaa na huduma zinazozalishwa katika maeneo haya.

Mheshimwa Spika, mwisho ni azma ya Serikali kukabiliana na haya yote kwa kusisitiza, pamoja na mambo mengine, kuhamasisha wananchi wawe na uchu wa maendeleo, kuendelea kupanua huduma muhimu za kijamii na kiuchumi ili ziwafikie wananchi wote, kujenga uwezo wa kiutendaji na kuwekeza kwenye miundombinu.

**MHE. WILFRED M. LWAKATARE:** Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Waziri, ningeomba anifafanulie kwamba kutokana na takwimu zake amesema kwamba utafiti uliofanyika umaskini umepunguza sasa ningeomba Mheshimiwa Waziri kupitia Bunge hili atueleze huo utafiti umefanyika wapi kwa kutilia maanani kwamba mimi huko ninakotoka umaskini unaonyesha kwamba umeongezeka kutokana na kipato cha watu ndani ya mifuko kuwa hakuna na vile vile watulishe kupata mlo mmoja kwa siku?

Pili, kutokana na takwimu alizozizungumzia Mheshimiwa Waziri amezungumza kwamba ifikapo mwaka 2010 umaskini unaweza ukawa umepunguza kwa asilimia hamsini, je, kwa kasi iliyopo takwimu hizi na kasi hiyo aliyoizungumza Mheshimiwa Waziri ni kweli mwaka 2025 umaskini kweli utakuwa umepunguza au tunataka kutoa kauli gani kwa Watanzania wategemee nini kufika mwaka 2025 ili tuhukumiane ifikapo wakati huo kama umaskini utakuwa haujapungua?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS (MHE. EDGAR D. MAOKOLA-MAJOGO):** Mheshimiwa Spika, *survey* niliyoisema imefanyika hapa nchini imefanyika kwa familia zinazoishi mijini pamoja na vijijini na mtakumbuka Waheshimiwa Wabunge kwamba hapa tumefanya semina mara mbili na tukagawa matokeo ya *survey* hiyo *house hold survey* iliyofanyika mwaka juzi na tukafafanua vikwazo ambavyo vinasababisha umaskini usipungue kwa kasi tunayoitaka. Ningemshauri Mheshimiwa Mbunge arejee tena takwimu hizo pamoja na maelezo ambayo tuliyatoa hapo.

Mheshimiwa Spika, ni kweli pia kwamba tunaposema umepungua umaskini kwa kiasi fulani zaidi ni watu wa mijini hususan kwa Dar es Salaam na ndiyo maana nimekiri kwenye jibu kwamba viko vikwazo vingi ambavyo vinawakwaza wananchi wanaotaka kuondokana na umaskini.

Lakini katika swali la pili anasema je, ifikapo mwaka 2025 kwa kasi hii tutakuwa tumepiga hatua kweli tutapunguza au tutakuwa tumeongeza umaskini?

Mheshimiwa Spika, ndiyo maana ningesema kwamba kuna jitihada hivi sasa zinaendelezwa na Serikali kwa kushirikiana na wananchi kupambana na umaskini kupitia mifuko mbalimbali.

Kwa mfano hili suala tunalolizungumzia linahusu zaidi umaskini wa kipato sababu upo umaskini wa kukosa nyumba ya kulala, umaskini wa chakula kama alivyosema, lakini unaozidi kuumiza wananchi ni umaskini wa kipato na ndiyo maana tuna mifuko mbalimbali na mwaka huu kwa mfano mfuko wa kuondoa umaskini kwa biashara ndogondogo upande wa *self* tumeongeza mikoa minane kati ya ile sita na kufanya mikoa kumi na nne ikiwepo Arusha, Kilimanjaro, Tanga, Mwanza na Ruvuma na sehemu nyinginezo na hivi leo au kesho nitawakabidhi Waheshimiwa Wabunge wote wa maeneo hayo masharti ya namna ya kutumia mikopo hiyo.

Kwa hiyo, ni matumaini yangu kwamba kwa juhudi zetu sisi wenyewe kama Serikali na wananchi na pamoja na kutimiza malengo yaliyowekwa na dunia ile *millennium goals* tutaweza tukapiga hatua na tutaendelea kupima kiwango cha kupunguza umaskini kadri miaka inavyoendelea ili tuone tumefikia hatua gani.

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, kabla sijamwita muuliza swali linalofuata, napenda kutambulisha wageni wa Kimataifa walioko kwenye *gallery* ya Bunge leo. Ni Waheshimiwa Wabunge wa Bunge la Jamhuri ya Kenya ambao wamekuja kututembelea siku ya leo. *(Makofi)*

Tunaendelea na swali linalofuata, Mheshimiwa Ussi Yahaya Haji.

Na. 103

**Wizara za Muungano**

**MHE. USSI YAHAYA HAJI** aliuliza: -

Kwa kuwa Tanzania ina Serikali mbili yaani Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Serikali ya Mapinduzi Zanzibar; na kwa kuwa kuna baadhi ya Wizara ni za Muungano: -

(a) Je, ni Wizara ngapi za Muungano zina majengo ya kudumu Tanzania Visiwani?

(b) Kwa zile Wizara ambazo zina majengo ya kudumu, je, Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ina mpango gani wa kuziwezesha Wizara hizo kuwa na majengo ya kudumu pamoja na Taasisi zake?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS (MHE. ARCADO D. NTAGAZWA)** alijibu: -

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Ussi Yahaya Haji, Mbunge wa Chaani, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Wizara za Serikali ya Muungano wa Tanzania zenye majengo ya kudumu Tanzania Zanzibar ni: -

(i) Ofisi ya Makamu wa Rais;

(ii) Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa;

(iii) Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa;

(iv) Wizara ya Elimu ya Juu, Sayansi na Teknolojia; na

(v) Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi.

(b) Mheshimiwa Spika, Wizara na Taasisi nyingine za Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ambazo hazina majengo ya kudumu Tanzania Zanzibar, hazina mpango wa kufanya hivyo kwa sasa kutokana na ufinyu wa Bajeti. Hali ya uchumi itakaporuhusu uwezekano wa kufanya hivyo utatazamwa kwa kuzingatia suala zima la kuwa na majengo ya kudumu ya Wizara na Taasisi zake sehemu mbili tofauti katika nchi moja.

**MHE. USSI YAHAYA HAJI:** Mheshimiwa Spika, kwa kuwa ikifika Aprili, 2005 tutasherehekea miaka 41 ya Muungano na umri huo ni mkubwa sana, je, kwa zile Taasisi ambazo bado hazina majengo ya kudumu atakubaliana nami kwamba Bajeti ya mwaka 2005 kuomba fedha ili zijengewe ofisi hizo?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS (MHE. ARCADO D. NTAGAZWA):** Mheshimiwa Spika, ni kweli ifikapo Aprili, 2005 Muungano wetu utakuwa umefikisha miaka 41, swali lake ni kwamba katika Bajeti hiyo tutaomba fedha zaidi ili kukidhi lile alilouliza la kujenga majengo ya kudumu kwa Wizara na Taasisi ambazo hazina majengo hayo Tanzania Zanzibar.

Mheshimiwa Spika, nina hakika Mheshimiwa Mbunge atakubaliana nami kwamba katika kipindi cha chini ya mwaka mmoja kuanzia hivi sasa hali ya uchumi wa Tanzania kama tunavyoifahamu siamini kwamba itakuwa imebadilika kiasi cha kutuwezesha kutimiza yapitiwayo.

Na. 104

**Kilimo cha Alizeti - Singida**

**MHE. MOHAMED H. MISSANGA** aliuliza: -

Kwa kuwa Wilaya ya Singida kwa muda mrefu hawakuwa na zao la uhakika la biashara hivyo kutegemea mazao kama mtama na mahindi kama mazao ya biashara na

chakula; na kwa kuwa hivi sasa wananchi hao wameanza kulima zao la alizeti kama zao lao la biashara na linaonekana kuwaletea manufaa; na kwa kuwa Serikali katika ngazi ya Mkoa na Wilaya ya Singida imeamua kuwa zao lao la biashara ni alizeti na mazao ya chakula ni mtama na mahindi: -

Je, Serikali itawasaidia vipi wananchi hao hasa wale wa Jimbo la Singida Kusini ili waweze kulima zao hilo kwa wingi na kwa ubora kama njia ya kuondokana na umaskini?

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO NA CHAKULA** alijibu: -

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Mohamed Missanga, Mbunge wa Singida Kusini, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, uzalishaji wa zao la alizeti katika Mkoa wa Singida umeongezeka kutoka tani 11,000 msimu wa mwaka 1999/2000 hadi tani 74,000 katika msimu wa 2003/2004. Bei ya zao hilo imeongezeka kutoka wastani wa shilingi 92 kwa kilo katika mwaka wa 1999/2000 hadi shilingi 184 kwa kilo katika mwaka wa 2003/2004.

Aidha katika Mkoa wa Singida kuna jumla ya viwanda 24 vya kusindika mbegu za alizeti zenye uwezo wa kusindika tani 12 hadi 13 kwa siku. Tunawapongeza sana wananchi na uongozi wa mkoa wa Singida kwa mafanikio makubwa ya kuendeleza kilimo cha zao hili la alizeti.

Mheshimiwa Spika, ili kuwasaidia wananchi wanaozalisha zao la alizeti kwa Mkoa wa Singida na maeneo mengine nchini, Serikali itaendelea kutekeleza mambo yafuatayo: -

(i) Utafiti na uzalishaji wa mbegu bora za alizeti. Hadi sasa aina mbili za mbegu bora zijulikanazo kama *Record* na *PAN 7352* zimetolewa kwa wakulima. Mbegu hizo zina uwezo wa kuzalisha kati ya kilo 2,000 na 3,000 za alizeti kwa hekta. Aidha, mbegu aina ya *PAN 7352* ina sifa ya ukinzani dhidi ya ugonjwa wa kutu ujulikanao kama *Puccinia rust.*

(ii) Katika msimu wa mwaka 2001/2002, Serikali ilianzisha utaratibu wa kulinda uzalishaji wa mbegu za mafuta nchini kwa kutoza kodi ya asilimia 10 kwa mafuta yote yaliyosafishwa yanayoingizwa nchini kutoka nje. Hii itahakikisha upatikanaji wa soko la uhakika kwa mbegu za mafuta zinazozalishwa nchini.

(iii) Kusimamia utekelezaji wa Mipango ya Maendeleo ya Kilimo ya Wilaya *(District Agricultural Development Plans - DADPs)* kwa kuwahakikishia wananchi ili kuongeza uzalishaji wa zao hili. Kwa mfano, kupitia mipango hiyo, wananchi wa Singida wamepewa malengo ya kuongeza matumizi ya wanyamakazi na zana bora za kilimo ili kupanua maeneo ya kilimo cha mazao ya chakula na biashara, likiwemo zao la alizeti.

Mheshimiwa Spika, Serikali kwa kushirikiana na Halmashauri za Mkoa wa Singida, itaendelea kuwapatia wakulima wa Mkoa huo mbinu bora za kilimo na usindikaji wa alizeti.

**MHE. MOHAMED H. MISSANGA:** Mheshimiwa Spika, kwa kuwa viwanda vidogovidogo alivyovitaja vilivyopo mjini Singida vinafanya kazi nzuri lakini kwa kukidhi mahitaji ya sasa. Lakini kutokana na uamuzi wa Serikali ya Wilaya na Mkoa wa Singida kwa kufanya zao hili kuwa zao la biashara matarajio ni kwamba alizeti italimwa kwa wingi na zao litakuwa kwa wingi zaidi, je, Serikali ina mpango gani wa kuwahakikishia wananchi wa Wilaya Singida kupata soko la uhakika la zao la alizeti linalotarajiwa kuongezeka kwa kiasi kikubwa?

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO NA CHAKULA:** Mheshimiwa Spika, napenda nimhakikishie Mheshimiwa Mohamed Missanga, kuwa soko la alizeti litaendelea kukua. Kama nilivyokwishasema tunawatoza kodi kwa mazao yote ya mafuta kutoka nje na kwa hiyo zao la alizeti linapata ahueni katika masuala ya ushindani.

Mheshimiwa Spika, lakini zaidi ya hilo ni kuwa imegundulika kisayansi kuwa alizeti ni mafuta yasiyo na rehemu *(Cholesterol)* nyingi kama ilivyo kwa mafuta yanayotokana na michikichi hata karanga. Kwa hiyo, kutokana na hiyo wananchi wanazidi kupata uelewa, watalishabikia zaidi zao hili kwa sababu tu ya uzuri wake dhidi ya *cholesterol. (Makofi)*

**SPIKA:** Leo vile vile Waheshimiwa Wabunge tumeweka maswali yaliyokosa nafasi siku ile kwa sababu ya tatizo la vipaza sauti. Ningependa yote sasa yapate nafasi ya kujibiwa. Kwa hiyo, tutakwenda kwa kasi kubwa kidogo.

Na. 105

**Kuinua Sekta ya Kilimo**

**MHE. HASSAN C. KIGWALILO (k.n.y. MHE. MARGARETH A. MKANGA)** aliuliza:-

Kwa kuwa katika Bajeti ya mwaka 2002/2003 Serikali ilitenga fungu maalum la fedha kwa lengo la kuinua sekta ya kilimo na katika kujibu swali namba 67 katika Mkutano wa Kumi na Moja, Serikali ilifafanua kwamba fungu hilo pamoja na mambo mengine litatumika kununulia chakula cha hifadhi ya Taifa:-

Je, ni kiasi gani cha mazao kilinunuliwa kwa lengo la kujihami na upungufu wa chakula ambao unaweza kuikumba nchi yetu kwa msimu wa mwaka 2003/2004?

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO NA CHAKULA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Kilimo na Chakula, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Margareth Agness Mkanga, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Katika Bajeti ya mwaka wa 2002/2003, Wizara ya Kilimo na Chakula ilitengewa shilingi bilioni 1.9 kwa ajili ya kununulia mahindi ya Hifadhi ya Chakula ya Taifa *(SGR).* Jumla ya tani 22,543 za mahindi zilinunuliwa.

Mheshimiwa Spika, wakati huo huo, Hifadhi ya Chakula ya Taifa *(SGR)* ilinunua tani 5,932 za mahindi kwa kutumia shilingi milioni 500 zilizotokana na mauzo ya mahindi katika mwaka uliotangulia wa 2001/2002 na kufanya kiasi chote cha mahindi kilichonunuliwa katika mwaka wa 2002/2003 kuwa tani 28,475. Aidha, Hifadhi ya Chakula ya Taifa ilianza mwaka ikiwa na albaki ya tani 47,048 za mahindi na kuifanya Hifadhi kuwa na jumla ya tani 75,523.

**MHE. HASSAN C. KIGWALILO:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, lakini ningependa kujua je, Serikali iko tayari kuendelea na utaratibu huu mzuri wa kuweka chakula hadi kufikia mwakani wakati wa uchaguzi ili wananchi wasiweze kuathirika wakati ule wa uchaguzi?

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO NA CHAKULA:** Mheshimiwa Spika, ni kweli Serikali ina azma hiyo, hadi sasa maandalizi yaliyoko ni tani zaidi ya 90,000 kwenye *SGR.*

Na. 106

**Chuo cha Utafiti na Kilimo Ukiriguru**

**MHE. JACOB D. SHIBILITI** aliuliza:-

Kwa kuwa Chuo cha Utafiti na Kilimo Ukiriguru, Wilayani Misungwi, kimekuwa na matatizo makubwa ya maji na umeme kutokana na upungufu wa fedha:-

(a) Je, Serikali inasemaje juu ya matatizo hayo ili watafiti waweze kuifanya kazi yao vizuri?

(b) Je, katika kufufua mabomba ya maji, wanavijiji jirani na kituo hicho watapatiwa lini maji kama ilivyokuwa hapo awali?

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO NA CHAKULA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Kilimo na Chakula, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Jacob Dalali Shibiliti, Mbunge wa Misungwi, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Kituo cha Utafiti wa Kilimo na Chuo cha Mafunzo ya Kilimo vya Ukiriguru vimekuwa na matatizo ya maji kuanzia mwaka wa 2000. Matatizo hayo yanatokana na kuchakaa kwa mfumo wa maji ambao ulijengwa mwaka wa 1958 na mfumo wa maji ukakatiwa umeme mwaka wa 2002 kutokana na limbikizo la deni la shilingi milioni 123.

Serikali imekwishachukua hatua za kutatua tatizo la maji la Ukiriguru. Deni la *TANESCO* la shilingi milioni 123 lililipwa kikamilifu katika mwaka wa fedha 2003/2004. Ukarabati wa mfumo wa maji ulianza katika mwezi wa Septemba, 2004 kwa ushirikiano na Jumuiya ya Ulaya na unatarajiwa kukamilika katika mwezi wa Januari, 2005.

(b) Baada ya kukamilika kwa ukarabati wa mfumo wa maji, wananchi wanaoishi kwenye vitongoji vilivyo kando kando ya bomba linalopeleka maji kwenye Kituo cha Utafiti wa Kilimo cha Ukiriguru watapatiwa maji kama ilivyokuwa katika miaka iliyopita.

**MHE. JACOB D. SHIBILITI:** Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu ya Mheshimiwa Naibu Waziri, kwanza ningependa kuipongeza Serikali kwa hatua iliyochukua kwa wanachuo wa Chuo cha Ukiriguru kwa kuwatekelezea shida zao, nawapongeza sana. *(Makofi)*

Pamoja na majibu hayo mazuri ningependa vile vile nimshukuru kwa kutekeleza shughuli za Mwalugababole, Buganda, Ukiriguru pamoja na Ngudama ambao nao wana matatizo ya maji kama alivyoeleza.

Swali, kwa kuwa idadi ya watu inazidi kuongezeka kwenye Chuo cha Ukiriguru, vile vile kwenye eneo ambalo bomba litapita, je, tanki lililopo ambalo sasa hivi ni dogo kuna uwezekano wa kuongeza ili baadaye maji yaweze kuwatosheleza kwa urahisi? *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI KILIMO NA CHAKULA:** Mheshimiwa Spika, kwanza nazipokea pongezi kwa niaba ya Wizara kuhusu utatuzi wa tatizo la maji katika Chuo cha Utafiti Ukiriguru na kwa wananchi wa eneo hilo. Ahsante kwa pongezi. *(Makofi)*

Pili, napenda nikuthibitishie kuwa yanayofanyika sasa ni pamoja na kuangalia mfumo mzima bomba na *storage.* Hata kama fedha hazitatosha tuna mpango wa kuwashirikisha wananchi kuwa na Mfuko wa Maji ambapo wananchi wakipata maji watalipia na hela zile zitakuwa katika mfuko maalum kwa kutatua matatizo hayo endapo tatizo la ukubwa wa tanki litajitokeza zaidi siku za usoni.

Na. 107

**Mafao ya Wafanyakazi Walioachishwa Kazi**

**MHE. TALALA B. MBISE** aliuliza:-

(a) Je, kuna wafanyakazi walioachishwa kazi kwenye Mashirika ya Umma ambayo mengine yalibinafisishwa na ambao hawakulipwa mafao yao yote?

(b) Je, ni kiasi gani cha madai hayo kinadaiwa na *PPF* italipa lini?

(c) Miongoni mwa waliostaafishwa kabla ya muda wao, je, watafaidi pensheni kama wenzao wa Serikali kama ilivyotangazwa katika Mkutano wa Bunge wa Aprili, 2004?

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. ABDISALAAM ISSA KHATIBU)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Fedha, kabla ya kujibu swali la Mheshimiwa Talala Bana Mbise, Mbunge wa Arumeru Mashariki, napenda nitoe maelezo ya ujumla kama ifuatavyo:-

Katika jitihada za kurekebisha uchumi nchini, Serikali iliamua kurekebisha pia Mashirika ya Umma kwa kuyabinafsisha, kuyauza au kuyakodisha. Uamuzi huu ulifikiwa baada ya Mashirika haya ya umma kushindwa kujiendesha yenyewe na kuwa mzigo mkubwa kwa Serikali. Miongoni mwa matatizo yaliyojitokeza kutokana na Mashirika hayo kushindwa kujiendesha ni kutowalipa wafanyakazi mishahara yao na pia kutowasilisha michango ya wafanyakazi katika Mifuko ya Hifadhi ya Jamii ikiwemo *PPF.*

Katika zoezi la urekebishaji kuna baadhi ya wafanyakazi waliondolewa katika ajira. Aidha, baadhi ya Mashirika hayakuweza kuwasilisha michango ya wafanyakazi wao kwa ajili ya mafao yao kwa mujibu wa sheria. Serikali ilichukua jukumu la kulipa mafao ya kisheria ya wafanyakazi kupitia kwenye vyombo vya Hifadhi ya Jamii kama *PPF,* kama nitakavyoeleza punde.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo hayo, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Talala Bana Mbise, lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba kuna baadhi ya wafanyakazi wapatao 17,000 wa Mashirika ya Umma yapatayo 157 yaliyobinafsishwa ambao hawakulipwa mafao yoyote. Hii ilitokana na Mashirika hayo kama nilivyoeleza hapo mwanzo kutowasilisha michango ya wafanyakazi hao ikiwa ni pamoja na ya mwajiri Mfuko wa *PPF* kwa mujibu wa sheria. Hivyo, Serikali ililazimika kuchukua jukumu la kulipa mafao ya wafanyakazi hao.

(b) Mheshimiwa Spika, kiasi cha madai ya mafao ya pensheni kilichokuwa kikidaiwa na *PPF* ni shilingi bilioni 18.4. Fedha hizi zimekwishalipwa *PPF* kwa njia ya fedha taslimu (shilingi bilioni 5.0) na Hati Fungati zenye thamani ya shilingi bilioni 13.4. Zoezi la kulipa mafao ya wahusika linaendelea.

Mheshimiwa Spika, aidha, zoezi la kutathmini linaendelea kwa Mashirika ambayo bado yanarekebishwa. Zoezi hili litakapokamilika, ikibidi Serikali itaangalia uwezekano wa kufidia michango inayotakiwa kwa *PPF* ili mfuko huo nao uendelee kuwapatia wanachama hao mafao yao kwa mujibu wa sheria.

(c) Mheshimiwa Spika, kama nilivyosema katika Mkutano wa Kumi na Sita wa Bunge lako Tukufu wakati najibu swali la Mheshimiwa Khadija Kusaga, Mbunge wa Temeke, wafanyakazi wa Mashirika ya Umma wanalipwa na wataendelea kulipwa mafao chini ya Sheria ya *PPF* Na. 14 ya 1978 kama ilivyorekebishwa na Sheria Na. 25 ya mwaka 2001.

Mheshimiwa Spika, marekebisho hayo pamoja na mambo mengine, yalisimamisha malipo ya mafao ya pensheni kwa wale ambao hawajatimiza umri wa kustaafu kwa mujibu wa Katiba. Kwa msingi huu, wastaafu wa aina hii watapata mafao yao ya uzeeni (pensheni) baada ya kufikisha umri wa miaka 55 kwa mujibu wa sheria. Kufanya vinginevyo itakuwa ni kukiuka Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Sheria ya *PPF* na kanuni za Pensheni.

**MHE. JOEL N. BENDERA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipatia nafasi ya kuuliza suala la nyongeza.

Mheshimiwa Spika, juzi niliuliza swali la nyongeza kwamba bado mpaka sasa wafanyakazi wa iliyokuwa Mamlaka ya Mkonge hawajalipwa na baada ya lile swali kupata waliniletea majina ya watu 120 ambayo ninayo sasa hivi hawajalipwa, kutoka Shamba la Mgombezi, Magoma, Hale. Mheshimiwa Waziri alizungumza kwamba wamelipwa.

Mheshimiwa Spika, je, Serikali iko tayari haya majina nimkabidhi Mheshimiwa Waziri ili aweze kuwalipa? *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. ABDISALAAM ISSA KHATIBU):** Mheshimiwa Spika, tunakubali kwamba alete hayo majina na tutaangalia kwa utaratibu wa kuyafanyia kazi. *(Makofi)*

Na. 108

**Utaratibu wa Kufidia Kodi ya *VAT***

**MHE. VENANCE M. MWAMOTO (k.n.y. MHE. DR. DIODORUS B. KAMALA)** aliuliza:-

Kwa kuwa katika Bajeti ya mwaka 2002/2003, Bunge lilikubali mapendekezo ya Serikali ya kurejesha utaratibu wa kufidia kodi ya *VAT* inayolipwa na wakulima wakati wa kusafirisha, kusindika na kwenye vifungashio vya mazao ya kuuza nje; na kwa kuwa ilielezwa kwamba kodi hiyo ingerejeshwa kwa wakulima kupitia Vyama vya Ushirika na

vyombo vingine vya wakulima vilivyosajiliwa na *Tanzania Bureau Authority* kwa ajili ya kodi hiyo.

(a) Je, uamuzi huo umewaongezea wakulima mapato kwa kiasi gani?

(c) Je, wakulima wa Kahawa wa Mkoa wa Kagera wamerejeshewa shilingi ngapi za Kitanzania kutokana na unafuu wa kodi iliyotajwa hapo juu?

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. ABDISALAAM ISSA KHATIBU)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Fedha, kabla ya kujibu swali la Mheshimiwa Dr. Diodorus Kamala, Mbunge wa Nkenge, napenda kutoa maelezo mafupi kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kifungu cha sita cha jedwali la kwanza la Sheria ya Kodi ya Ongezeko la Thamani *(VAT)* ya mwaka 1997 kinawataka wakulima wanaouza mazao nje ya nchi kurejeshewa kodi waliyolipa ili kuwezesha uuzaji huo. Urejeshaji huo unafanywa kupitia Vyama vya Ushirika na vyombo vingine vya wakulima vilivyosajiliwa na Mamlaka ya Mapato. Kodi inayorejeshwa na ile iliyolipwa kwenye ukoboaji, usindikaji wa mazao, gharama za usafiri hadi kwenye minada, huduma za Bandari na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, ili kuondoa usumbufu ambao unaweza kujitokeza, Mamlaka ya Mapato inajihusisha moja kwa moja na Vyama vya Ushirika vinavyosajiliwa kwa ajili hiyo. Hata hivyo, wakulima wakubwa wanaosafirisha mazao nje ya nchi na ambao wamesajiliwa kwa ajili ya *VAT* wanapata marejesho ya kodi wanazolipa moja kwa moja.

Mheshimiwa Spika, baada ya kutoa maelezo hayo, napenda sasa kujibu swali la Mheshimiwa Dr. Diodorus Kamala, Mbunge wa Nkenge, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Si rahisi kujua ni kiasi gani cha mapato wakulima wameongezewa kutokana na uamuzi huo kwa sababu mamlaka haijapata takwimu kamili za idadi ya wakulima katika kila chama husika.

(b) Chama cha Wakulima wa Kahawa wa Mkoa wa Kagera *(KCU) (1990) Ltd.)* ni moja kati ya vyama vya wakulima vilivyosajiliwa na Mamlaka ya Mapato kwa ajili ya mpango huu.

Kati ya Agosti, 2002 na Oktoba, 2004, Chama hicho kilirejeshewa kiasi cha shilingi 93,832,711.32. Baadhi ya vyama vingine vilivyorejeshewa kodi ya *VAT* ni *KNCU (1984) Ltd.* ilirejeshewa shilingi 102,106,433.03 kati ya Julai , 2002 na Oktoba, 2004 na *SHIRECU (1984) Ltd.* iliyorejeshewa shilingi 49,336,438.00 hadi Oktoba, 2004. Ni matumaini yetu kwamba wanachama wa vyama hivi wamenufaika na marejesho hayo.

**MHE. VENANCE M. MWAMOTO:** Mheshimiwa Spika, kwa kuwa *VAT* katika vifungasho hivyo inaleta mkanganyo mkubwa katika kurejesha hasa kwa wakulima wa mazao kama chai, tumbaku, kahawa na alizeti, je, kwa nini Wizara yako isifute kabisa *VAT* kwenye vifungasho iwe *zero rated? (Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. ABDISALAAM ISSA KHATIBU):** Mheshimiwa Spika, tutaangalia hali itakavyokuwa huko siku za mbele tutatazama utaratibu ambao unaoweza kufaa zaidi kwa manufaa ya wakulima.

Na. 109

**Ukarabati wa Majengo na Uzio katika Shule za Sekondari**

**MHE. GEORGE M. LUBELEJE** aliuliza:-

Kwa kuwa majengo ya Shule za Sekondari za Mpwapwa, Kilakala na Dodoma hayajafanyiwa ukarabati kwa kipindi kirefu na vile vile hazijawekewa uzio kwa ajili ya ulinzi na usalama wa shule hizo.

Je, Serikali ina mpango gani wa kuyakarabati majengo ya shule hizo pamoja na kuziwekea uzio?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS (MHE. ARCADO D. NTAGAZWA) (k.n.y. WAZIRI WA ELIMU NA UTAMADUNI)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Elimu na Utamaduni, napenda kujibu swali la Mheshimiwa George Malima Lubeleje, Mbunge wa Mpwapwa, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, mpango wa Serikali wa kukarabati shule za Serikali nchini umeainishwa katika Mpango wa Maendeleo ya Elimu ya Sekondari *(MMES)* 2004 - 2009. Aidha, Serikali imekwishaandaa maelekezo katika ngazi zote kuanzia shuleni hadi Taifani kuhusiana na utekelezaji wa *MMES* katika masuala yanayohusu ujenzi na ukarabati wa shule.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa kwanza wa utekelezaji wa *MMES* jumla ya shule za sekondari 40 za Serikali zimepangwa kukarabatiwa kwa gharama ya shilingi 2,734,000,000. Aidha, Serikali imepanga kukarabati shule za sekondari nane zenye wanafunzi wenye ulemavu na kuchangia ujenzi wa shule mpya mbili za wenye ulemavu. Shule za sekondari za Kilakala na Dodoma ni miongoni mwa shule 40 zilizoainishwa na *MMES* kufanyiwa ukarabati katika mwaka wa kwanza ambapo shule ya sekondari ya Mpwapwa ipo katika mpango wa kuanzishwa kidato cha tano.

**MHE. GEORGE M. LUBELEJE:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ili niweze kuuliza swali dogo la nyongeza. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Waziri, nina swali la nyongeza.

Pamoja na mpango mzuri wa *MMES* si wa kuboresha Elimu ya Sekondari, je, Mheshimiwa Waziri atakubaliana nami kwamba majengo haya yasipokarabatiwa muda mrefu pamoja na mpango wa *MMES* yanaweza kusababisha kwamba hapo baadaye gharama itakuwa kubwa sana kuyakarabati?

Swali la pili, kwa kuwa katika Mpango huu wa *MMES* nimeulizia vile vile kuweka uzio kwa ajili ya ulinzi na usalama katika shule hizo, je, Mheshimiwa Waziri anasema nini kuhusu hili?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS (MHE. ARCADO D. NTAGAZWA):** Mheshimiwa Spika, nakubaliana naye kwamba majengo yasipokarabatiwa yanaharibika na hata wakati mwingine kubomoka. Ndio maana katika lugha ya Kiswahili tuna msemo kitunze kidumu.

Mheshimiwa Spika, lakini sote tunafahamu kwamba mwenendo au utaratibu wa kukarabati vitu vyetu mbalimbali hata hili neno ukarabati tu limepatikana hivi majuzi. Kwa hiyo, ni vizuri tukajifunza kuwa na utaratibu kweli wa kukubaliana na msemo Kitunze kidumu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuhusu la pili ameulizia upatikanaji wa kuweka uzio katika shule ya sekondari ya Mpwapwa. Si kwamba tumekwepa kulijibu, nilivyokuwa najibu nimesisitiza suala la ujenzi kuanzishwa Kidato cha tano katika mpango mzima tukijua tunakarabati shule kwa mpango wa *MMES* lazima na suala la uzio lizingatiwe.

Na. 110

**Kikosi cha *NAVY* - Kigamboni**

**MHE. MOSSY SULEIMAN MUSSA** aliuliza:-

Kwa kuwa wanajeshi wa Jeshi la Wananchi, Tanzania wamekuwa wakichangia kwa kiasi kikubwa kubuni miradi ya maendeleo nchini:-

Je, ni utaratibu gani mahsusi umepangwa ili kuendeleza w*orkshop* ya Kikosi cha *Navy* Kigamboni ikiwemo chelezo?

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI (k.n.y. WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa, kabla ya kujibu swali la Mheshimiwa Mossy Suleiman Mussa, napenda kutoa maelezo yafuatayo:-

Karakana ya Kamandi ya Wanamaji Kigamboni ilianzishwa miaka ya 1969/1970 kwa msaada wa rafiki zetu, Serikali ya watu wa China. Wakati wa kuanzishwa kwa Karakana hiyo yenye Idara 19, za matengenezo ya sehemu mbalimbali za meli, kilijengwa pia chelezo *(dock yard)* chenye uwezo wa kuchukua meli za tani 170-200. Kwa wakati huo, uwezo wa chelezo hicho ulionekana kuwa ni mkubwa kwani nyingi ya meli zetu zilikuwa katika kiwango cha uzito huo. Baada ya matumizi ya miaka mingi na uchakavu wa baadhi ya vifaa katika chelezo hicho; uwezo wa awali umepungua. Kwa hivi sasa uwezo uliopo ni wa kubeba meli za tani 100 - 120 tu.

Mheshimiwa Spika, baada ya kutoa maelezo hayo ya utangulizi napenda kujibu swali la Mheshimiwa Mossy Suleiman Mussa, Mbunge wa Mfenesini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kutokana na uchakavu wa karakana ya kikosi cha *Navy* na uwezo mdogo wa chelezo kuhudumia meli kubwa, Wizara yangu ikishirikiana na rafiki zetu Serikali ya China, tunachukua hatua zifuatazo:-

(a) Mpango umekamilika wa kuifanyia ukarabati mkubwa Karakana hiyo kwa lengo la kuiboresha ili iwe ya kisasa kabisa na pia kuongezea uwezo wa chelezo ili kukiwezesha kuwa na uwezo wa kuhudumia meli za tani kati ya 400 - 600. Hii ni pamoja na kukiwezesha kuchukua meli zaidi ya moja kwa wakati mmoja, kwa kuzingatia mahitaji ya meli za kisasa. Kazi hiyo itaanza kufanyika mwishoni mwa mwaka huu wa fedha.

(b) Uboreshaji wa karakana hiyo utakwenda sambamba na kuboresha utaalam wa wataalam wa kuiendesha, ili tupate wataalam wa kutosha kwa ajili ya uendeshaji wa karakana iliyoboreshwa. Aidha, Serikali itaendelea kuinua viwango vya wataalam wetu katika karakana hiyo kwa kuwapa mafunzo ndani na nje ya nchi.

Mheshimiwa Spika, katika mpango kabambe wa maendeleo ya JWTZ wa miaka 15, huduma mbalimbali ikiwa ni pamoja na kuongeza uwezo wa Kamandi ya Wanamaji kwa ujumla wake, ni eneo ambalo mpango umelipa uzito maalum. Karakana ya kisasa na chelezo kilicho bora na cha kisasa ni sehemu muhimu ya maboresho hayo.

**MHE. MOSSY SULEIMAN MUSSA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi ya kuuliza suala la nyongeza. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri. Kwa kuwa *workshop* ya *Navy* Kigamboni inafanya kazi kubwa na nzuri za kiufundi.

Je, wananchi wa kawaida wanaweza kwenda na kuitumia *workshop* hiyo?

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba karakana ile ya *Navy* ni karakana kubwa ina fani zaidi ya 19 na inafanya kazi nzuri na kama nilivyosema katika jibu langu la msingi tunaiboresha zaidi ili ifanye kazi nzuri zaidi.

Sasa kuhusu kutoa huduma uraiani jibu ni kwamba kimsingi hii ni karakana inayoweza kuhudumia vifaa vya kijeshi sasa nyakati ambazo kazi zimepungua vile vile tunaruhusu meli za kiraia vile vile kupata huduma katika karakana hiyo.

**MHE. MOHAMED RISHED ABDALLAH:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi niulize swali moja la nyongeza.

Kwa kuwa umri wa kustaafu wanajeshi wetu unatofautiana na watumishi wengine wa Serikali; na kwa kuwa hawa ni wataalamu ambao wamebobea katika shughuli hizi za karakana ile.

Je, Mheshimiwa Waziri anasema nini juu ya kuongeza muda wa kustaafu wataalamu wale kwa sababu ni adimu katika nchi yetu?*(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Spika, ni kweli kama alivyosema Mheshimiwa Mbunge kwamba katika Jeshi umri wa kustaafu unategemea na cheo cha askari au cha afisa tofauti na uraiani huko ambako umri wa kustaafu ni miaka 60. Kule wanastaafu kwa ngazi ya vyeo vyao.

Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba katika fani za utaalamu sio kwenye karakana hii tu lakini na fani zingine za Uhandisi za Mizinga ni kweli kwamba kuna baadhi ya wataalamu wetu wanastaafu wakiwa bado wana nguvu na hilo tumeshaliona kwamba halileti maslahi kwa nchi kwa sababu baadhi ya hawa sasa wanachukuliwa na nchi jirani, wanakwenda kufanya kazi huko. Hilo tumeshaliona na sasa hivi Wizara yangu inalifanyia kazi. *(Makofi)*

Na. 111

**Polisi Kushirikiana na Raia Wema**

**MHE. ALI MACHANO MUSSA** aliuliza:-

Kwa kuwa raia wema wanapookota au kuona kitu ambacho hawakitambui au kinatiliwa mashaka hutakiwa kutoa taarifa kwenye kituo cha Polisi kilicho karibu nao na kwa kuwa kuna raia wema kutoka katika Kisiwa cha Tumbatu waliokiona kitu kinachoshukiwa kuwa ni silaha inayofanana na bomu na kwa raia hao wametekeleza jukumu lao la kutoa taarifa Polisi lakini wakaambiwa waende wenyewe wahakikishe kama kweli ni silaha.

(a) Je, sababu gani zilizosababisha kuwataka raia kufanya kazi za Polisi ambazo hawana utalaalamu nazo wakati Polisi wenyewe wapo?

(b) Je, askari Polisi wanapotoa maelekezo kama hayo hawaoni kuwa wanawavunja moyo raia wema ambao wanatoa ushirikiano kwa polisi?

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Ali Machano Mussa, Mbunge wa Tumbatu, lenye sehemu (a) na (b) kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Nakubaliana na Mheshimiwa Mbunge kuwa mara kwa mara Serikali imekuwa ikiwasisitizia raia wema kutoa taarifa Polisi wanapokiokota au kukiona kitu wasichokifamu na kutilia mashaka. Katika taarifa yao kwa Polisi raia hao wema huombwa kueleza mahali kitu hicho kilipo na wasifu wa umbile la kitu hicho. Lengo ni kuwasaidia Polisi wajue aina ya kitu wanachotaka kukifuatilia na mahali kilipo, kabla ya kwenda kukiangalia.

Mheshimiwa Spika, wananchi wa Kisiwa cha Tumbatu walipotoa taarifa kwenye kituo cha Polisi baada ya kukiona kitu walichokitilia mashaka kuwa ni bomu waliombwa na Polisi watoe wasifu wa kitu walichokitilia mashaka yaani umbile lake na mahali kilipo ili Polisi waweze kufuatilia. Polisi hawakutaka raia hao waende wenyewe wakachunguze kama kweli ni silaha, wala kukibeba na kukipeleka kituo cha Polisi. Kwa hiyo, hapakuwepo usumbufu wowote ambao ungeweza kuwavunja moyo wananchi hao.

Napenda kutumia nafasi hii kuwashukuru na kuwapongeza wananchi na Tumbatu kwa kutoa taarifa kwa Polisi ambayo iliwezesha bomu hilo kuharibiwa na wataalamu wa mabomu kabla halijaleta athari yoyote. Aidha, natoa wito wananchi wote waige mfano huu.

**MHE. ALI MACHANO MUSSA:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuuliza maswali ya nyongeza.

(a) Kwa kawaida askari polisi wanapopata matukio kama haya wanatakiwa wayafanye upelelezi na nina imani kubwa kwamba amefanya hivyo. Naomba kujua Serikali baada ya kugundua kitu hicho kwamba ilikuwa ni bomu wanaweza wakawaeleza wananchi wa Tumbatu kwamba silaha hiyo imetoka nchi gani, imeundwa mwaka gani na imeingizwa na nani?

(b) Serikali inachukua hatua gani ya ulinzi ili wananchi wa Tumbatu watokwe na hofu wanapoona vitendo kama hivi katika maeneo yao? *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Spika, napenda kujibu maswali ya Ali Machano Mussa, Mbunge wa Tumbatu, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba katika matukio kama haya yakitokea polisi huwa wanapeleleza. Lakini kwa tukio hili kwa sababu linahusika na mabomu utalaam wa mabomu uko katika Jeshi la Wananchi ndiko kwenye utalaamu huo. Kwa hiyo, bomu hili kama lilitengenezwa wapi, mwaka gani, la aina gani na kadhalika ni kazi ambayo inafanywa na wenzetu wa Jeshi la Wananchi na kwa sababu Mheshimiwa Mbunge anataka kupata habari zaidi kuhusu bomu hili la aina gani, limetengenezwa wapi, mwaka

gani, basi tutawasiliana na Wizara ya Ulinzi ili habari zipatikane na Mheshimiwa Mbunge tutakuletea taarifa hiyo.

Kuhusu hatua gani za ulinzi tunachukua katika eneo hilo, tumeshawahamasisha wavuvi katika eneo la Kisiwa cha Tumbatu waendelee kuwa macho. Lakini vile vile Mheshimiwa Mbunge, anajua kabisa kwamba kuna mawasiliano kati ya Wizara yetu na yeye mwenyewe kuhusu kusogeza huduma za ulinzi katika Kisiwa cha Tumbatu. Kuhusu kujenga Kituo cha Polisi, mwezi wa nane nilitembelea Tumbatu na walinihakikishia kwamba sasa wameshapata kiwanja cha kujenga kituo cha polisi na tuliwajulisha kwamba mara wakishaanza watuarifu ili sisi Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi, tunashirikiane nao katika kujenga kituo cha polisi ili ulinzi usogee katika Kisiwa cha Tumbatu. *(Makofi)*

Na. 112

**Ujambazi katika Ziwa Tanganyika**

**MHE. SHOKA KHAMIS JUMA** aliuza:-

Kwa kuwa wavuvi wanaovua katika Ziwa Tanganyika huwa mara nyingi wanapata matatizo ya kunyang'anywa mali zao kama vile nyavu, mashine, mashua na kadhalika na majambazi wanaotoka nchi jirani.

Je, Serikali ina mpango gani wa kukomesha tatizo hilo linalowasumbua wananchi wetu?

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Shoka Khamis Juma, Mbunge wa Micheweni, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba wavuvi katika Ziwa Tanganyika siku za nyuma walipata matatizo ya kunyang'anywa mali zao kama vile nyavu, mashine, mashua na kadhalika na majambazi waliotoka nchi jirani.

Tatizo hili hivi sasa limedhibitiwa na vyombo vya ulinzi na usalama na hali ya usalama inaridhisha sana katika eneo hilo. Kamati ya Bunge ya Ulinzi na Usalama, ilipotembelea eneo hili mwezi uliopita iliridhika na hali ya usalama na hali iliyopo katika Ziwa Tanganyika. *(Makofi)*

Hata hivyo bado Serikali inachukua hatua zaidi ya kuimarisha ulinzi katika Ziwa hilo. Hatua hizo ni pamoja na mambo yafuatazo:-

(i) Tunaimarisha boti za doria zilizopo za Jeshi la Wananchi, za Polisi na za Idara ya Maliasili ili boti hizo zifanye kazi ya doria Ziwani kwa ufanisi mkubwa zaidi.

(ii) Serikali inaendelea kuhamasisha wananchi, hususan wavuvi washiriki kikamilifu katika ulinzi ndani ya Ziwa Tanganyika kwa kuweka vifaa vya mawasiliano *(Radio Call)* katika mashua zao kwa lengo la kutoa taarifa kwenye vyombo vya dola wanapowaona watu wanaowatilia mashaka huko Ziwani.

(iii) Tunaendelea kuimarisha mikutano ya ujirani mwema na nchi tunazopakana nazo yaani *DRC,* Burundi na Zambia ili kwa pamoja tushirikiane kudhibiti wahalifu katika Ziwani hilo. *(Makofi)*

**MHE. HALIMENSHI K. R. MAYONGA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi.

Pamoja na majibu ambayo yametolewa kuhusu ujambazi unaoendelea katika Ziwa Tanganyika na mimi ambako natoka na mali zangu ziliibiwa nyingi tu. Sasa kwa kuwa hilo jibu lilishatia hasara wavuvi wengi wamekuwa ni maskini kwa kupoteza mamilioni ya fedha na nyavu zao.

Je, Serikali na vyombo vya fedha viko tayari kuweza kuwasaidia wale ambao walikopa kwenye benki za fedha halafu hawawezi tena kulipa na ni maskini wa kupindukia na wizi huo umepelekwa huko sehemu kama Kongo ambako hakuna usalama na Burundi ambako kuna vita vya kudumu sasa huu ujirani mwema utafanikiwaje? Naomba kwamba tuweze kupewa fidia ya kutosha?Hapo sasa! *(Makofi/Kicheko)*

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Halimenshi Mayonga, Mbunge wa Kigoma Kaskazini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwanza kama nilivyosema katika jibu langu la msingi kwamba hali katika Ziwa Tanganyika sasa hivi imedhibitiwa na ni nzuri na Kamati ya Ulinzi na Usalama ya Bunge hili mwezi uliopita ilikwenda kuthibitisha ukweli huu. Kwa hiyo, nilifikiri kwanza Mheshimiwa Mbunge, kwanza angetoa pongezi walau kwa hatua ambazo vyombo vya dola vinachukua. *(Makofi/Kicheko)*

Sasa kuhusu vita vya kudumu huko Burundi na Kongo kusema kweli utulivu kule Kongo *(DRC)* utulivu ambao sasa uliopo umesaidia sana vile vile kuleta utulivu ndani ya Ziwa Tanganyika kwa sababu wengi wale waliokuwa wanapora, vilikuwa ni vile vikundi ambavyo vilikuwa vinapigana *DRC* vinapokosa chakula, sasa vinavizia wavuvi wetu katika *Lake Tanganyika* kwa hiyo, utulivu ule tunaomba uendelee na mwezi huu tuna mkutano mkubwa kabisa Dar es Salaam wa Nchi za Maziwa Makuu ambao unajielekeza katika kudumisha usalama *DRC,* Burundi na kwingineko. *(Makofi)*

Sasa kuhusu fidia kwenye mabenki hili kwa kweli Mheshimiwa Mbunge, ule mkataba kati ya mvuvi na benki yake kule alikokopa sasa mimi kuutolea kauli katika Bunge hili si rahisi. Ninachoomba tu kwamba wale wavuvi wazungumze na yale mabenki yaliyowakopesha ili waelewane jinsi ya kulipana. *(Makofi/Kicheko)*

**MHE. DR. WILLIAM F. SHIJA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi niulize swali la nyongeza.

Kwa kuwa hali ya ujambazi haijatokezi tu katika eneo la Ziwa Tanganyika lakini vile vile katika eneo la Ziwa Victoria na maeneo mengine nchini; na kwa kuwa kwa maoni yangu naona kwamba hali ya ujambazi inaongezeka siyo kwenye Maziwa tu bali hata nchi kavu, je, Serikali itakubaliana na mimi kwamba sasa umefika wakati wa kutengeneza mfumo wa kuunganisha Jeshi la Polisi na Jeshi ili vikosi maalum viwezi kuangalia namna ya kusafisha hali ya majambazi kama ambavyo wenzetu wa Kenya naamini wamefanya wakati fulani? *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Dr. William Shija , Mbunge wa Sengerema, kama ifuatavyo:-

Ni kweli matukio ya ujambazi yanaongezeka katika maeneo mbalimbali kama alivyotaja Mheshimiwa Mbunge katika Ziwa Victoria na hata katika nchi kavu. Lakini nadhani Waheshimiwa Wabunge, wanakumbuka kabisa katika hotuba yetu ya Bajeti tulielezea kwa undani kabisa hatua mbalimbali, tunazochukua katika kukabiliana na wimbi hili, kwa mfano *Lake Victoria* boti zetu za polisi zilikuwa hazifanyi kazi sawa sawa, Bunge hili hili limetupa karibu shilingi bilioni mbili za kukarabati boti za doria kwa hiyo, tuna hakika kabisa baada ya ukarabati huo, ulinzi katika Ziwa Victoria utaimarika.

Mheshimiwa Spika, huko nchi kavu vile vile Bunge hili hili, limepitishwa vifaa vya kuwezesha polisi kukabiliana na uhalifu. Limepitisha ajira ya polisi wapya 2000, limepitisha magari karibu 200 kwa sababu hata *RPCs* na sasa wamepitisha mapya na yameshaanza kutoka, *RPCs* sasa mkirudi mtakuta kule sasa wana magari mapya *Land Cruiser* imara kabisa kufukuzana na majambazi. *(Makofi)*

Vile vile baada ya hapo *OCDs* watapata magari mapya, *OC CIDs* wote hii yote ni kuwapa nguvu Jeshi la Polisi kupambana na majambazi. Vile vile tumetoa vifaa vya karibu bilioni 2.5 kwa ajili ya mawasiliano, majambazi yana mawasiliano mkasema polisi wetu hawana mawasiliano mmetoa vifaa vya bilioni 2.5 kwa ajili ya polisi wapate mawasiliano ya kisasa kupambana na hiyo. *(Makofi)*

Mwisho, juzi Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani, alifungua mkutano wa wadau kutazama mfumo gani mzuri wa kushirikisha polisi na jamii, mfumo unaitwa polisi jamii. Wadau wametoa mawazo yao nia yetu nikutaka sasa tushirikishe jamii kwa ukamilifu zaidi, yaani polisi washirikiane na jamii katika kupambana na uhalifu, Jeshi la Wananchi tunalishirikisha kwenye *operation* maalum, si kwamba halihusiki kabisa.

Mheshimiwa Spika, kwenye *operation* maalum nadhani watakumbuka Wabunge kutoka Kagera mwaka jana tulifanya *operation* ya pamoja, Polisi na Jeshi la Wananchi katika kufagia wahalifu. Kwa hiyo, huwa tunashirikisha Jeshi la Ulinzi katika *operation* maalum. *(Makofi)*

**MHE. PONSIANO D. NYAMI:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa niulize swali la nyongeza.

Kwa kuwa Kamati ya Ulinzi na Usalama ya Bunge ilitembelea Mkoa wa Kigoma ambako kuna Ziwa Tanganyika lakini haikutembelea Mkoa wa Rukwa ambako kuna Ziwa Tanganyika na hususan katika maeneo ya Mpanda Magharibi pamoja na Nkasi ambako kumeathirika zaidi maeneo ya Kirando, Ninde na kadhalika.

Je, Serikali gani hasa wa kuongeza vifaa kwa wanajeshi waliopo wachache pamoja na wanajeshi wenyewe katika maeneo niliyoyataja ikiwepo na Kalambo ili kusudi eneo hilo na lenyewe liwe salama kama eneo la Kigoma ambavyo limepata usalama? *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Ponsiano Nyami, Mbunge wa Nkasi kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba Kamati ya Bunge ya Ulinzi na Usalama, haijaenda Rukwa lakini nina hakika kwa sababu wamejipangia utaratibu wa ratiba bila shaka na Rukwa watafika kutembelea ule mpaka wetu katika eneo hilo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, asa kuhusu taratibu za kuongeza ulinzi katika eneo hilo la mpaka wetu na *DRC* kwa upande wa Rukwa, Jeshi la Wananchi limepeleka kule viteule *(detachments)* za kutosha kabisa na katika mwaka huu wa fedha katika Bajeti mliyoipitisha hapa ya Jeshi la Wananchi, mliongeza vifaa ambavyo vitapelekwa kule ili wafanye kazi ile ya doria kwa vizuri zaidi.

Kwa upande wa Wizara ya Mambo ya Ndani, tunashirikiana na wananchi kujenga vituo vya polisi viwili katika Tarafa ya Karema, Mheshimiwa Waziri alishatoa ahadi kwamba kuna vituo viwili katika eneo lile ambalo karibu vinakamilika tunashirikiana kukamilisha ili juhudi za Jeshi la Wananchi, pale mpakani na juhudi vya vituo vya polisi ambavyo tunaviweka pale mpaka kwa pamoja tuweze kuimarisha ulinzi katika eneo hilo. *(Makofi)*

Na. 113

**Wafanyabiashara Kupanga Bei katika Mfumo wa Soko Huria**

**MHE. ALHAJ AHAMADI H. MPEME** aliuliza:-

Kwa kuwa kusudi la kuanzishwa kwa mfumo wa soko huria katika biashara ni kushindanisha bei katika ununuzi na uuzaji wa bidhaa mbalimbali na kwa kuwa sasa wafanyabiashara huwa wanakuwa na mikutano ya kupanga bei sasa katika ununuzi wa mazao ya kilimo badala ya kufanya mashindano ya bei kitendo ambacho husababisha mazao ya kilimo kuwa na bei ndogo.

(a) Je, Serikali haioni kwamba kitendo hicho cha kupanga bei kinawakandamiza wakulima?

(b) Kwa kuwa, utaratibu wa kupanga bei unafanywa na wafanyabiashara binafsi, je, Serikali haioni kwamba wakati umefika sasa kuviwezesha vyama vya ushirika vya wakulima viweze kununua mazao na kuleta ushindani wa bei?

**NAIBU WAZIRI WA USHIRIKA NA MASOKO** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Alhaj Ahmadi Hassan Mpeme, Mbunge wa Mtwara Mjini, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, Serikali haiungi mkono utaratibu wa kupanga bei unapofanyika na wafanyabiashara kwa njia ya magenge na hivyo inaupiga vita utaratibu huo usitumike popote pale. Hata hivyo upo utaratibu wa wadau wa mazao makuu kama vile pamba, tumbaku na korosho kukutana na kupanga bei dira ya zao kabla ya ununuzi wa zao kuanza. Utaratibu huu pia unaruhusu bei dira kuangaliwa upya pindi inapoonekana kuwa bei hiyo haina maslahi kwa wadau kulingana na mwenendo wa bei katika soko la dunia.

Aidha, Serikali inatambua kwamba wapo wafanyabiashara wachache wanaokiuka makubaliano yanayofikiwa katika vikao vya wadau na hivyo kuwalipa wakulima chini ya bei dira. Serikali huchukua hatua mbalimbali za kudhibiti ukiukwaji wa makubaliano hayo ikiwa ni pamoja na kuwafutia leseni wafanyabiashara wa aina hii mara inapodhihirika wamekiuka makubaliano.

(b) Mheshimiwa Spika, ili kumlinda zaidi mkulima dhidi ya wafanyabiashara wadanganyifu, Serikali imeweka mpango wa kuviwezesha vyama vya ushirika kununua kwa wingi mazao ya wakulima kwa kuzingatia udhamini wa mikopo katika vyombo vya fedha kwa kulingana na kuviongezea nguvu ya mitaji ya biashara. Chini ya utaratibu wa *Export Credit Guarantee Scheme (ECGS)* vyama vyote vinavyotimiza masharti huweza kukopeshwa kwa udhamini wa Serikali. Mfano ni vyama vya msingi vya ushirika vya kule Mtwara vilivyopata udhamini chini ya utaratibu huu. *(Makofi)*

Aidha, kwa kutumia utaratibu unaosimamiwa na mradi wa stakabadhi ya mazao ghalani yaani *(Warehouse Receipt System)* ulioanza na mazao ya kahawa na pamba kwa majaribio, wakulima wataamua kuuza mazao yao pale bei inapokuwa nzuri kwao. Utaratibu huu pia utakuwa na ufanisi zaidi utakapotumiwa ndani ya vyama vya ushirika. Serikali imo katika majadiliano na mabenki ya biashara yenye lengo la kuondoa matatizo yaliyojitokeza katika matumizi ya mfuko wa *ECGS* yanayovipunguzia vyama vya ushirika uwezo wa kushindana *(level playing field)* na wafanyabiashara binafsi. Serikali pia imeandaa programu kabambe ya mageuzi na modenaizesheni ya ushirika nchini itakayosimamiwa na Wizara yangu yenye lengo la kuviwezesha vyama vya ushirika kuwa na nguvu ya ushindani katika biashara kwa kuimarisha uongozi, elimu na ajira za watendaji.

Aidha, sera ya masoko ya kilimo inayoandaliwa na Wizara yangu itawezesha kuboreshwa kwa mfumo wa upatikanaji na usambazaji wa taarifa sahihi za masoko na bei. Hatua zote hizo zina lengo la kuviwezesha vyama vya ushirika vya wakulima viweze kununua mazao na kuleta ushindani wa bei kama inavyoshauriwa Mheshimiwa Mbunge. *(Makofi)*

**MHE. ALHAJ AHAMADI H. MPEME:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri. Nina maswali mawili ya kuuliza kama ifuatavyo:-

(a) Kwa kuwa uuzaji wa mazao ambayo hayajasindikwa nje ya nchi pia inasababisha kushuka kwa bei ya mazao ya wakulima na kwa kuwa Serikali iliahidi kwamba itajitahidi kuhakikisha kwamba mazao ya kilimo yanasindikwa hapa nchini, je, ni mazao gani sasa hivi yanasindikwa kwa asilimia 100? *(Makofi)*

(b) Kwa kuwa mara kwa mara wakulima hupata hasara kutokana na kushuka kwa bei ya mazao yao na husababisha kudumaa kwa wakulima hao kuendelea na kilimo, je, Serikali haioni vizuri sasa ikawafidia wakulima pale inapopatikana hasara ya kushuka kwa bei ya mazao? *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA USHIRIKA NA MASOKO:** Mheshimiwa Spika, napenda kujibu maswali mawili ya Mheshimiwa Alhaj Ahamadi Mpeme, Mbunge wa Mtwara Mjini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, anachosema Mheshimiwa Mbunge ni kweli kwamba mazao yetu yakiuzwa bila kusindikwa yaani yakiuzwa yakiwa ghafi hayampi tija mkulima ndiyo maana Serikali inasisitiza suala la usindikaji wa mazao. Kwa hiyo, jitihada za Serikali zinazoendelea sasa hivi ni pamoja na kuhamasisha wawekezaji kuweza kuwekeza katika viwanda vya kubangua korosho pamoja na mazao mengine kama vile viwanda vya nguo kwa ajili ya pamba.

Mheshimiwa Spika, lakini vile vile lipo suala la kuhimiza wakulima vile vile kuongeza ubora wa mazao yao ili yaweze kupata bei nzuri. Sasa ni mazao gani ambayo sasa hivi yanauzwa kwa kusindika ni kama alivyosema pengine nisingeweza nikatoa kwa takwimu lakini baadhi ya mazao yanayouzwa kwa kusindikwa ni pamoja na korosho, kahawa yetu, lakini kwa uhakika wa takwimu pengine tupate muda ambao tunaweza tukampatia kwa uhakika zaidi.

Sasa suala la kufidiwa bei kwanza nilipokuwa najibu swali la msingi hapa nimeelezea juu ya bei dira inayopangwa na wadau na nimesema kwamba bei dira inaweza ikabadilika kutegemeana na mabadiliko ya bei ya dunia, kama bei itapanda kwa vyovyote vile mkulima ananufaika, lakini kama bei itateremka itabidi vile vile uangalie utaratibu wa kuiteremsha hiyo bei. Lakini utaratibu ambao tunadhani kwamba utakuwa ni wa kudumu tulijibu hapa juzi tukasema pengine ingekuwa ni vizuri kuingia katika utaratibu wa bima ya anguko la bei ambayo itakuwa ni ya uhakika zaidi kuweza kutoa fidia hiyo. Lakini vile vile Serikali inaangalia utaratibu wa kuanzisha mfuko wa

kusawazisha bei *(Price Stabilization Fund)* ambayo inaweza kuwa na uhakika zaidi kuwafidia wakulima endapo bei itakuwa chini ya makubaliano.

**MHE. HASNAIN M. MURJI:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi ili niulizwa swali moja kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa ushindani wa baadhi ya mazao ya wakulima kwa mfumo uliopo hauna ushindani wa bei na kwa kuwa kuna baadhi ya mazao kama kahawa kwa mfumo wa uuzaji kwa mnada umefanikiwa kupata bei nzuri, je, Serikali haioni kwamba sasa wakati umefika kwa zao la korosho kutumika kuuzwa kwa mfumo huo kwa mnada? *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA USHIRIKA NA MASOKO:** Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Hasnain Murji, Mbunge wa Newala, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, utaratibu unaotumika katika uuzaji wa zao la kahawa ni kwa kupitia mnada kama alivyokuwa amesema Mheshimiwa Mbunge na hii inatokana na tu na jinsi zao lenyewe lilivyo katika mfumo wa soko la dunia.

Sasa katika zao la korosho ambalo amelitaja Mheshimiwa Mbunge kwa bahati mbaya halina utaratibu ambao unauwezesha likauzwa kwa mfumo ambao unatumika katika zao la kahawa na ndiyo maana tunasisitiza tu kwamba ili korosho zetu ziweze zikauzika kwa bei ya kuvutia zaidi ni vizuri tusisitize suala la kuuza korosho iliyobanguliwa ili iweze kuwa na bei ya kuridhisha kwa wakulima. *(Makofi)*

Na. 114

**Wizi wa Mazao ya Wakulima kwa Njia ya Lumbesa**

**MHE. JACKSON M. MAKWETTA** aliuliza:-

Kwa kuwa lumbesa ni ujazo wa mazao katika gunia lenye ukubwa usio wa kawaida, mtindo ambao wanunuzi wa mazao huongeza kipande chenye ukubwa unaochukua ujazo wa nusu gunia au zaidi kwenye gunia la kawaida kwa bei sawa na gunia lenye wa kawaida ambalo linachukua debe sita tofauti na lumbesa ambalo huchukua debe tisa.

(a) Je, Serikali inafahamu kuwepo kwa mtindo huo wa udanganyifu unaotumiwa na baadhi ya wanunuzi kuwaibia wakulima wa mazao yao?

(b) Kwa kuwa mtindo huo hufanywa na baadhi ya wanunuzi kwa baadhi ya mazao kutokana na wakulima kutojua kwa undani juu ya soko la mazao yao kwenye baadhi ya masoko nchini, je, kwa nini Serikali isishirikiane na uongozi wa Jiji la Dar es Salaam na mahali pengine nchini ili watoe mwongozo wa kuuza/kununua mazao ya

wakulima kwa vipimo maalum/sahihi bila kuingilia misingi ya uchumi wa soko na wakati huo huo ikiwalinda wakulima na walaji?

(c) Kwa kuwa usimamizi wa kanuni *(regulations)* ni moja kati ya matatizo katika uchumi wa soko, je, Serikali ina mpango gani wa kusimamia kwa makini zaidi eneo hili ili kuzuia ukiukwaji wa kanuni hizo kama ilivyotokea kuwepo kwa ujazo wa lumbesa?

**NAIBU WAZIRI WA USHIRIKA NA MASOKO** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Jackson Makwetta, Mbunge wa Njombe Kaskazini, lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, Serikali inazo taarifa za kuwepo kwa mtindo mbaya unaotumiwa na baadhi ya wanunuzi wa mazao kujaza magunia kupita kiasi ambao wanautumia kwa jina la lumbesa. Hata hivyo Serikali haina ushahidi wa kutosha kama ujazo huo wa lumbesa ni kipimo kinachotumika katika kununulia mazao hayo kwenye magulio.

Mheshimiwa Spika, uchunguzi uliofanywa na Wizara yangu umebaini kwamba ujazo huo wa lumbesa hutumika katika ufungashaji wa mazao kwa madhumuni ya kupunguza gharama za usafirishaji kwa wenye vyombo vya uchukuzi ambao hutoza gharama kwa kuhesabu idadi ya magunia badala ya uzito.

Aidha, ufungashaji huo husababishwa na utozaji wa ushuru ambao pia hutumia idadi ya magunia badala ya uzito. Pamoja na kuwepo kwa hali hii, Wizara imebaini pia kuwa kuna udanganyifu ambao hufanywa na wanunuzi kwa kutumia vipimo vya ujazo visivyo rasmi kama vile ndoo, debe na makopo na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, kwa kutambua athari mbalimbali zinazoweza kumpata mkulima kutokana na mbinu za udanganyifu anazoweza kufanyiwa na wanunuzi, Serikali kwa kutumia wakala wa vipimo *(Weights and Measures Agency)* pamoja na Halmashauri za Wilaya na Miji, imekuwa ikihimiza na kusimamia matumizi ya vipimo rasmi vinavyokubalika kisheria kama vile kilogramu na lita badala ya vipimo vya makopo, madebe na mafungu ambavyo hutofautiana kati ya sehemu moja na nyingine.

(b) Mheshimiwa Spika, Serikali wakati wote imekuwa ikisimamia taratibu za ununuzi na uuzaji wa mazao na bidhaa zote kwa njia mbalimbali ikiwemo njia ya kushirikiana na uongozi wa Jiji la Dar es Salaam katika kudhibiti udanganyifu na uvunjaji wa sheria, kanuni na taratibu za ununuzi na uuzaji wa mazao. Kwa mfano, kwa kupitia mamlaka ya masoko ya Kariakoo, Serikali imetoa miongozo mbalimbali ya matumizi ya vipimo rasmi katika ununuzi wa mazao ya kilimo. Ndiyo maana taarifa za masoko zinazotolewa na Wizara yangu kila wiki hueleza bayana vipimo sahihi vilivyotumika kwa ununuzi wa uuzaji wa mazao katika masoko. Hivyo basi ni wajibu wa wakulima na walaji kuzitumia kikamilifu taarifa hizo muhimu.

(c) Hivi sasa Serikali inakamilisha maandalizi ya sera ya masoko ya mazao ya kilimo. Sera hii itakapokamilika, sheria, kanuni na taratibu zilizopo zitarekebishwa ili ziendane na sera hiyo ya masoko ili kuboresha usimamizi wa kanuni na taratibu za ununuzi na uuzaji wa mazao ya kilimo chini ya mfumo wa soko huru. Lengo ni kuwa na mfumo ambao utaondoa ukiukaji wa sheria na kanuni za ununuzi na uuzaji wa mazao nchini.

**MHE. JACKSON M. MAKWETTA:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi. Tatizo ni kwamba lumbesa inatokea wakati wanunuzi hawa wananunua moja kwa moja kwa mkulima na siyo kwenye magulio. Kama ni hivyo kutokana na kitendo hicho ni kwamba hawa wanunuzi kwanza wanaharibu magunia kwa sababu wanakata yale magunia mazima na kuunganisha ili waunde lumbesa, pili wabebaji wa magunia haya katika maeneo ya Tandale, Dar es Salaam wamelalamika kwamba wanavunjika migongo kwa sababu ya uzito wa kupita kiasi wa magunia ya lumbesa na tatu ni kwamba wanaumiza walaji na wauzaji. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, Serikali inapotumia neno uzito wa gunia Tandale huwa inatumia lumbesa au gunia hili ninalosema ambalo nalikataza hapa? Kwa hiyo, ningependa kuuliza kwamba kutokana na tabia hii ambayo inaendelea kuumiza wakulima na walaji, Serikali katika mkakati wake wa kupunguza umaskini ambao unawagusa wakulima zaidi isingekuwa vizuri basi ikakubali kwamba haina uhakika, wakati mimi nina uhakika Mbunge wao ikachukua hatua za kurekebisha? *(Makofi/Kicheko)*

**NAIBU WAZIRI WA USHIRIKA NA MASOKO:** Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Jackson Makwetta, Mbunge wa Njombe Kaskazini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, nimesema kwamba Serikali inaulaani huo utaratibu wa lumbesa na kusema kweli nataka niseme hapa kwamba huo siyo utaratibu rasmi na mimi nilichosema kwamba katika magulio ya kawaida ambayo yanafuata utaratibu, utaratibu huu hauonekani. Lakini kama alivyosema Mheshimiwa Mbunge mwenyewe ni utaratibu ambao unatumika kinyemela huko ambako wananchi wanakwenda kulanguliwa. *(Makofi)*

Kwa hiyo, nataka niseme kwamba utaratibu huo haufai na kusema kweli Serikali inaupiga marufuku ili wananchi waweze wakatumia vipimo rasmi ambavyo vimetambuliwa na Serikali. *(Makofi)*

Na. 115

**Leseni za Uuzaji na Ununuzi wa Vyuma Nchini**

**MHE. JENISTA J. MHAGAMA** aliuliza:-

Kwa kuwa Serikali hivi karibuni imepiga marufuku uuzaji na ununuzi wa vyuma chakavu hapa nchini kwa sababu unasababisha wizi na ubomoaji wa madaraja na mataruma ya reli.

Je, kwa nini Serikali isichukue hatua ya kusimamisha au kufunga utoaji wa leseni kwa kampuni zinazohusika kwa lengo la kuzuia uharibifu huo?

**WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Jenista Mhagama, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Kwa kuzingatia umuhimu wa viwanda katika uchumi wa Taifa, Serikali iliamua kupiga marufuku uuzaji nje wa chuma chakavu kwa lengo la kuvihakikishia viwanda vyetu upatikanaji wa malighafi.

Mheshimiwa Spika, amri ya kuzuia uuzaji nje wa chuma chakavu ilitangazwa katika Gazeti la Serikali kwa Tangazo la Serikali Na. 170 la tarehe 20 Juni, 2003. Amri hii ilihusu aina tatu ya chuma chakavu ambazo ni *Iron and Steel, Aluminium* na *Brass.* Aina hizi za chuma chakavu ni zile ambazo viwanda vyetu vina uwezo wa kuzirejea *(recycle).*

Aina nyingine ambazo hatuna uwezo wa kuzirejea yaani *recycle* ni kama vile shaba yaani *Copper, Zinc,* Bati na kadhalika, hazikuhusika na amri hii. Hata hivyo kulikuwepo na utaratibu maalum wa kudhibiti uuzaji nje wa aina hizo za chuma chakavu uliosimamiwa na Kamati ya wataalam. Ingawa kumekuwepo na amri ya kupiga marufuku uuzaji wa chuma chakavu nje na kuundwa kwa Kamati ya wataalam, bado yaliendelea kujitokeza malalamiko kutoka kwa wayeyushaji ya kukosa malighafi. Wizara ilipokea malalamiko kupitia kikao cha wadau kilichofanyika hapa Dodoma tarehe 7 Februari, 2004 kuhusu kuibiwa kwa vifaa muhimu kama vile mataruma ya reli, nyaya za simu, mabomba kwenye madaraja, mifuniko ya mashimo ya maji taka na kadhalika na kusafirishwa nje kama chuma chakavu.

Mheshimiwa Spika, pamoja na amri hii, Wizara ili-*commission* Chuo Kikuu cha Dar es Salaam kufanya utafiti ili kujua kiasi cha chuma chakavu kinachozalishwa nchini, uwezo wa kuyeyusha na aina zake. Utafiti huu unatarajiwa kuwa ukikamilika utasaidia Serikali kuweka sera ya muda mrefu yaani *long term policy* kuhusu matumizi ya chuma chakavu nchini.

Ili kupambana na hujuma hizi na ujanja uliojitokeza, Serikali iliamua ifuatavyo tangu tarehe Mosi Septemba, 2004:-

(i) Kupiga marufuku mtu au kampuni yoyote kusafirisha nje ya nchi aina yoyote ile ya chuma chakavu hadi hapo itakapotangazwa vinginevyo; na

(ii) Kupiga marufuku shehena yoyote ya chuma chakavu kupitishwa katika Bandari zetu au mipakani kama *transit goods* hadi hapo itakapotangazwa vinginevyo. Wafanyabiashara wanaonunua chuma chakavu nchi jirani wapitishe chuma hicho nchi nyingine na sio Bandari zetu.

Mheshimiwa Spika, amri ya kupiga marufuku iliyotolewa tarehe Mosi Septemba, 2004 iliwazuia wale wote waliokuwa wana leseni za mauzo ya chuma chakavu nje kutoruhusiwa tena kusafirisha nje chuma chakavu aina zote kupitia Bandari zetu. Aidha, kuanzia tarehe ya amri hiyo, hakuna utoaji wa leseni mpya kwa ajili ya kuuza nje aina yoyote ya chuma chakavu. *(Makofi)*

**MHE. JENISTA J. MHAGAMA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa majibu mazuri ya Mheshimiwa Waziri, lakini ninalo swali moja dogo la nyongeza. Kwa kuwa Serikali imefanikiwa kudhibiti biashara hiyo ambayo ilikuwa inapelekea kuangusha uchumi wa miundombinu iliyokwishajengwa ndani ya nchi yetu, lakini kwa kuwa agizo hilo limesababisha pia ukosekanaji wa malighafi katika viwanda vyetu ambavyo viko ndani ya nchi yetu ya Tanzania.

Je, Wizara haioni kwamba ili kusaidia sasa uzalishaji wa chuma ndani ya nchi yetu kuanzisha vituo maalum katika Mikoa ambavyo wananchi wote watakaoweza kukusanya vyuma chakavu wakaviwasilisha hapo na ikaweza kugundulika vinatoka wapi na vikaendelea kusaidia katika uzalishaji wa chuma ndani ya nchi yetu? *(Makofi)*

**WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA:** Mheshimiwa Spika, kwanza biashara hii ya chuma chakavu inafanywa na watu binafsi. Kutokana na kuzuia kupeleka nje chuma chakavu, viwanda vilivyokuwepo nchini vilikuwa vitatu, sasa hivi viko vinane. Vitano viko Dar es Salaam, kimoja kiko Mwanza na viwili viko Arusha. Kwa hiyo, hawa wenyewe wana utaratibu namna gani ya kukusanya chuma chakavu kwa sababu wakikusanya kile lazima baadaye kifike kiwandani ili wapewe pesa zao taslimu pale pale. Hili linatokana na malalamiko ya wakusanyaji wa chuma chakavu kwamba walikuwa wanakopwa na wenye viwanda. Kwa hiyo, tumesema kwamba lazima walipwe fedha taslimu pale wanapokabidhi chuma chakavu. Ndiyo shabaha yake. Ahsante sana.

**SPIKA:** Ahsante, Waheshimiwa Wabunge, maswali yamekwisha na muda wa maswali umekwisha. Matangazo ya Vikao vya Kamati kwa leo ni kama ifuatavyo:-

Kamati ya Fedha na Uchumi wanaendelea kukutana leo saa 5.00 asubuhi katika Ukumbi namba 219. Kamati ya pili ni Kamati ya Maendeleo ya Jamii, Mheshimiwa Haroub Said Masoud, Makamu Mwenyekiti anaomba wakutane leo saa 4.30 asubuhi, imeshapita kwa hiyo, tuhesabu kwamba itakuwa ni saa 5.00 asubuhi chumba namba 231. *(Makofi)*

Kamati ya Mambo ya Nchi za Nje, Mwenyekiti wake Mheshimiwa Dr. William Shija anaomba kikao kifanyike saa 5.00 asubuhi kwenye chumba namba 227. Hizo ndiyo Kamati za Bunge. Sasa Umoja wa Wanawake Wabunge *(TWPG)* Mwenyekiti wake Mheshimiwa Anne Makinda, anaomba Kikao cha Wanawake Wabunge kifanyike saa 7.00 mchana katika chumba namba 231 ghorofa ya pili. Mwisho wa matangazo ya vikao.

Waheshimiwa Wabunge, niwafahamishe kwamba ratiba ya kesho ni kwamba tunamaliza Mkutano wa Kumi na Saba itakapofika Saa 7.00 mchana ili kutekeleza ile azma ya wale wanaosafiri kuwahi kwenda kusherehekea Sikukuu pamoja na familia zao. Kwa hiyo, shughuli zilizobaki tutaziendesha kwa namna ambayo itatuwezesha kufikia kwenye lengo hilo.

Mwisho wa matangazo. Katibu tuendelee na *Order Paper.*

## MISWADA YA SHERIA YA SERIKALI

### Muswada wa Sheria ya Usimamizi wa Mazingira wa Mwaka 2004
### *(The Environmental Management Bill, 2004)*

*(Majadiliano yanaendelea)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, kuna tangazo nimeambiwa na Mwenyekiti kwamba Wabunge wa CCM wakutane saa 7.00 mchana huu humu ndani katika Ukumbi huu huu. Sasa naita Waheshimiwa waliobaki jana, Mheshimiwa Job Ndugai, atafuatia Mheshimiwa Edson Halinga na Mheshimiwa Frank Maghoba, jiandae. Mheshimiwa Job Ndugai, unaweza kuanza.

**MHE. JOB Y. NDUGAI:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ili na mimi niweze kuchangia katika kujadili hoja iliyoko mbele yetu ya Sheria ya Mazingira ya mwaka 2004.

Naanza kwa kumpongeza Mheshimiwa Waziri, Ofisi ya Makamu wa Rais (Mazingira) Mheshimiwa Arcado Ntagazwa, ambaye ni Rais wetu wa *UNEP,* Katibu Mkuu wa Ofisi yake na Ndugu yangu Dr. John Kabudi ambaye alikuwa *consultant* katika zoezi zima la kutengeneza sheria hii.

Mheshimiwa Spika, kwa kawaida wananchi maskini ni vigumu sana kuwatenganisha na mazingira kwa sababu wanaishi kwa kutegemea mazingira. Sisi Watanzania tunayo haki ya kuvuta hewa safi isiyochafuliwa, tunayo haki ya kunywa maji safi, kula chakula kizuri na safi na tunayo haki ya kuishi katika mazingira safi. Lakini pamoja na haki hizo, tunayo majukumu na jukumu letu moja kubwa ni kuhifadhi mazingira. Sisi sote ni mashahidi kwamba katika miaka ya hivi karibuni mazingira yetu yamekuwa yakiharibiwa vibaya sana na hasa maeneo yetu mengi ya maji, iwe ni Mito,

Maziwa na hata Bahari yetu imekuwa ikiharibiwa sana na uchafuzi wa mazingira na tunajua kabisa kwamba maji yakichafuka kuyasafisha ni gharama kubwa sana.

Mheshimiwa Spika, wenzetu Ulaya na Marekani wana baadhi ya Mito na Maziwa ambayo maji yake hayanyweki, hayaogeleki, huwezi kumwagilia chochote wala huwezi kuvua samaki wala hayana faida yoyote kwa sababu waliharibu mazingira katika siku za huko nyuma. Sasa imekuwa ni vigumu kufanya chochote kwa sababu ni gharama kubwa sana kuweza kurekebisha kosa hilo.

Mheshimiwa Spika, hapa nchini kwetu mmoja wa waharibifu wakubwa wa mazingira kwa maoni yangu mimi ni bei ya umeme wa *TANESCO* na taratibu ya Taasisi nzima ya *TANESCO. (Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kupata *service line TANESCO* ni shilingi 204,000/=. Ukiwa na jiko la umeme na pasi moja na *bulb* tano hivi kwenye nyumba, bili yako inakwenda mpaka kwenye shilingi 40,000/= au shilingi 50,000/= kwa mwezi. Utamkuta mtu maskini wa kijijini ana bili ya shilingi 4,000/= na akichelewa kulipa kwa siku moja anapigwa faini ya shilingi 8,000/=, kwa hiyo, anatakiwa kulipa shilingi 12,000/=. Kwa mwananchi ambaye hana umeme, akitaka kuvuta umeme anaambiwa atoe hela ya kununua nguzo, wanya, vikombe na pamoja na kununua vitu vyote hivyo, bado vitu hivyo ni mali ya *TANESCO.* Matokeo yake nini?

Mheshimiwa Spika, kule Dar es Salaam maghorofa mengi utakuta watu wanapikia mikaa, yamejaa moshi wa mkaa. Mijini kote watu wanapikia mkaa. Kwa hiyo, uchomaji mkaa umekithiri. Ukitoka Dodoma hapa mpaka Dar es Salaam njia nzima ni vituo vya mkaa. Kwa hiyo, maana yake misitu inateketea na matokeo yake ni kwamba Mito inakauka, *catchments area* nyingi zinaharibika na mabwawa yanakauka. Kwa hiyo, matokeo yake tena, hao hao *TANESCO* ambao wanahitaji maji ya kuzalisha umeme wanakosa maji kwa ajili ya kuzalisha umeme, inakuwa ni *vicious circle* tayari.

Kwa hiyo, nashauri *TANESCO* wawe na programu mbili. Programu yao moja isiwe ni kuweka bei kwa ajili ya kupata faida tu, waangalie masuala ya mazingira, pia *impact* yake ya bei zile kwa mazingira. Lakini pili, *TANESCO* nao sasa waanze kuwa na program za kusaidia hifadhi za mazingira, programu za kuotesha miti, kusambaza miche, kupanda hiyo miti na hifadhi mbalimbali za mazingira katika maeneo ambayo ni muhimu kwa kuhifadhi mazingira katika nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, katika sheria iliyoko mbele yetu, fungu la 191 linatoa adhabu kwa mtu yoyote anayetenda kosa chini ya sheria hii pamoja na adhabu nyingine kwa kulipishwa kwa kiwango cha chini shilingi 50,000/=. Yapo makosa madogo madogo vijijini ambayo imekuwa ni kawaida kuwa kama ndio chanzo cha rushwa kwa baadhi ya watendaji wa vijijini kule. Mwananchi akisomba mchanga wa kujengea nyumba yake anakamatwa, ameharibu mazingira, akifyeka shamba jipya anakamatwa analipishwa faini kwa sababu ameharibu mazingira, akifyatua tofali za kuchoma faini, anaharibu mazingira.

Kwa hiyo, ningependa kusema toka mwanzo hapa kwamba nia ya sheria hii sio kukwaza wananchi wasifanye shughuli zao ndogo ndogo vijijini. Nia ya sheria hii ni kuweka taratibu nzuri zaidi ya kuyatumia mazingira yetu kwa maendeleo yetu kwa sababu kama nilivyosema mwanzo, mwananchi maskini hawezi kuishi bila mazingira, anategemea mazingira kwa maisha yake.

Mheshimiwa Spika, lakini pia faini hizi zitawagusa na wengine kama alivyosema Mheshimiwa Mwenyekiti wa Kamati jana akiwasilisha hotuba kwa niaba ya Kamati ya Mazingira kwamba zipo taratibu ambazo tumezizoea kwa mfano mabasi yanayotoka Tabora, Mwanza na Shinyanga yanayokwenda Dar es Salaam, yakifika maeneo ya Kongwa kule wanasimama, abiria wote wanateremka kuchimba dawa. Sasa ningependa kuwaambia watani zangu hawa, kuchimba dawa Kongwa kule marufuku, faini ni shilingi 50,000/= kwa kuchafua mazingira. *(Kicheko)*

Kwa hiyo, sheria hii inafika mbali sana katika kututaka basi katika barabara zetu zote nchini tuwe na maeneo maalum ambayo kutajengwa vyoo kwa ajili ya wasafiri kuweza kuvitumia vyoo vile wakiwa katika safari kama ilivyo kwenye barabara ya Makuyuni kwenda Ngorongoro, kumefanyika utaratibu wa namna hiyo. Sasa utaratibu ule uigwe nchi nzima na vyoo hivyo visiwe mbali. Hata watu binafsi wanaweza wakawekeza katika mambo hayo, mabasi au magari ya kawaida yasimame katika maeneo hayo, watu wakapata pesa kidogo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, fungu la 57 linakataza kufanya shughuli za kudumu ndani ya mita 60 kutoka kwenye Mto, Ziwa, Bwawa au Bahari. Jambo hili ni zuri lakini ningependa tu kumwambia Mheshimiwa Waziri, katika utekelezaji wa hili tuwe makini kidogo, tusifike mahali pa kupiga X kila kilichopo kwenye mita hizo 60 nchi nzima, inaweza kutuletea matatizo. Hapo natoa tahadhari tu.

Mheshimiwa Spika, nia yangu hasa ni kuzungumzia fungu 69 ambalo linahusu masuala ya *biosafety, biotechnology* na masuala ya *genetic modified organisms* kwa ujumla. Kwanza niipongeze Serikali kwa kuibua jambo hili na kuliweka sasa ndani ya sheria kwa kuzingatia ile *precaution principle* kama ilivyo katika Mkataba wa *CARTEGINA.* Sayansi hii wanayoiita wenyewe *Genetic Engineering* sasa iko duniani na hatuna namna ya kusema kwamba tunaweza tukaikwepa. Hatuwezi sisi kuwa kisiwa. Iko hapa na hatuna namna. Ni sayansi ya kuhamisha *genes* kutoka mmea au kutoka kiumbe kimoja kwenda kiumbe kingine.

Mwaka juzi nchi ya Zambia walikuwa na njaa kubwa sana wakapata msaada wa mahindi kutoka kwa wenzetu walioendelea mahindi hayo ya *GMO.* Serikali ya Zambia ilikataa kupokea mahindi yale. Mimi najiuliza, endapo sisi Watanzania tukapata balaa kama lile, hivi msimamo wetu utakuwa ni nini? *Position* yetu ni nini kisera na kisheria kutoka kwa Waziri wetu wa Kilimo au Waziri wa Sera anayeshughulikia masuala ya majanga au Waziri wa Mazingira? Tukipata tatizo hilo tukapata msaada iwe ni mahindi, mchele au ngano, lakini ni *product* ya *GMO,* tutapokea au hatutapokea?

Tukumbuke wakubwa wengi mnakwenda Ulaya na wananchi wengi wanakwenda Ulaya na Marekani kila mwaka, nani kasema wanaokwenda huko hawajala chakula hicho chenye *GMOs?* Maana kwa sehemu kubwa vyakula vya kule vinakuwa ni matokeo ya teknolojia hizi za kisasa wanazoziita *Genetic Engineering.* Baadhi yetu tunavaa hata mashati yanayotokana na pamba ambayo ni *product* wanaita *bit cotton,* ni *product* hiyo ya *Genetic Engineering.* Hata noti za Ulaya zilizo nyingi ni *product* ya pamba ambayo imetokana na *GMOs* hizo.

Kwa hiyo, teknolojia hii ina faida nyingi tu, muda hautoshi kuielezea lakini nasimama hapa kusema ule utaratibu ambao umewekwa ndani ya fungu hili la 69 la kuweka umakini wa namna ya *introduction* ya teknolojia hizi ndio ninaounga mkono hapa. Unaweza ukakuta mtu labda hali ndizi au mhogo kwa sababu ya *enzyme* iliyoko mle au *protein* fulani, lakini kwa kutumia teknolojia hii tunaweza tukaondoa hiyo, kwa hiyo ndizi ile au muhogo ukaliwa bila tatizo lolote.

Kwa hiyo, habari ya kusema kwamba mimi sinywi maziwa au sifanyi hiki, teknolojia hii inaweza ika-*deal* kwa kiwango kikubwa sana na matatizo madogo madogo kama hayo. Ingawa sisi hatutaki kufika pale walipofika wakubwa pa kuanza kuzalisha watoto wa binadamu kwa njia ya *cloning,* hilo hatuhitaji, hilo libakie huko Ulaya.

Pia hatuhitaji teknolojia kama hii ambayo wametumia Wachina. Wachina wamechukua *gene* moja kutoka kwa binadamu wakaipandikiza kwa nguruwe, baadaye wakagundua kwamba nyama ya nguruwe wanaotokana na teknolojia hiyo imekuwa tamu zaidi. Sasa mtu anajiuliza, anapokula nyama ile, anakula nguruwe au binadamu? Sisi hatutaki kwenda huko. Nia yetu ni kupata faida zitokanazo na teknolojia hizi ambazo ni muhimu sana kwa maendeleo yetu.

Mapendekezo yangu kwa fungu hili, fungu hili halimwambii Waziri atengeneze kanuni za masuala ya *biosafety* na *biotechnology.* Kwa hiyo, nashauri pawepo na sehemu ambayo inatoa *provision* ya masuala ya *regulations* ili Waziri aweze kutoa *regulations* hizo humu kwa sababu ni fungu moja, liko ndani ya sheria linalohusu masuala haya.

Pili, tuanzishe *The National Biotechnology Centre* mahali fulani isaidie masuala haya. Lakini pia tukubaliane ndani ya Serikali, masuala haya ya *biotechnology* na *biosafety* yatakuwa chini ya Waziri wa Kilimo au chini ya Waziri wa Mazingira au wapi? Tukubaliane kimsingi.

Mheshimiwa Spika, mwisho nina mapendekezo kwenye maeneo manne. Fungu la 14 linasema kutakuwa na Mkurugenzi wa Mazingira atakayesimamia hasa sheria hii. Nikubaliane na Mheshimiwa Ireneus Ngwatura kwamba ni bora Mkurugenzi huyu kwa kweli tukamwita *Commissioner* kwa sababu Sheria hii ni ya uratibu na ni *cross cutting,* ni bora awe *Commissioner* ili aweze kufanya kazi hii ya uratibu ipasavyo. Kinachopungua kwenye fungu lile la 14 ni kwamba Mamlaka itakayomteua huyo awe ni Mkurugenzi au *Commissioner* haijatajwa hapa.

Kwa hiyo, tunashauri Mamlaka hiyo itajwe lakini pia kwa mtu mkubwa kama huyu anayeshika Ofisi kubwa kama hii, lazima sifa zake zielezwe hapa. Kwa hiyo, nashauri zile sifa ambazo zimewekwa huku ndani ya fungu la 21 zinazomwelezea Mkurugenzi Mkuu wa *NEMC* za kielimu na kiuzoefu basi hizo pia zichukuliwe ziongezwe kwenye fungu hili.

Pendekezo la pili, fungu la 182, sheria imemtaja *District Health Officer* kuwa yeye ndiye atakuwa *inspector.* Nashauri Maofisa wa Afya wote wa ngazi za Vijiji, ngazi za Kata na kadhalika watambuliwe na sheria hii kuwa ni inspectors ili wafanye kazi yao ipasavyo.

Kwenye *fourth schedule* tulikuwa tumekubaliana kwenye Kamati kwamba suala la Wajumbe wa Bodi ya Wakurugenzi ya Mfuko wa Mazingira litatazamwa. Ningependa kukumbushia kwamba litazamwe.

Mheshimiwa Spika, mwisho nashauri *Town Planners* katika Miji yetu na Majiji yetu waanze kupima viwanja vikubwa kidogo Mijini kwenye maeneo ambayo wamekuwa wakiyaita...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kumalizika muda wa Mzungumzaji)*

**MHE. JOB Y. NDUGAI:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante, umetuonyesha mfano mzuri wa kuzungumzia vifungu vya Muswada. Nadhani inasaidia sana kama wote tutafanya hivyo.

Sasa namwita Mheshimiwa Edson Halinga. Mheshimiwa Frank Maghoba, jiandae na Mheshimiwa John Singo, vile vile jiandae.

**MHE. EDSON M. HALINGA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipatia nafasi na mimi nichangie kidogo. Tatizo la mazingira katika nchi yetu linatuletea maafa makubwa sana. Lakini nadhani ni shauri ya upole wetu ndio maana tunapata matatizo hayo.

Mheshimiwa Spika, mimea ya aina nyingi imepotea kutokana na uharibifu wa mazingira. Hii inatokana na kuchoma moto ovyo ambao kwa kweli ni ugonjwa wa nchi nzima, hasa wafugaji wanachoma misitu ili yaote majani mapya, kumbe wanaunguza viini vingi vya mazao ambayo yangeweza kutusaidia kwa maendeleo yetu kwa baadaye. Kukata miti, kuni na mkaa, hii inawasaidia sana watu walio wengi katika nchi hii.

Mimi nadhani tukiweka utaratibu wa mazingira kuwa katika Wizara fulani na huu wa nishati kuwa Wizara nyingine, bado tutapata matatizo kwa sababu hatuna mbadala wa nishati kwa mwananchi wa kawaida. Ni vizuri hii Wizara ya Nishati na Madini ingeshika yote haya ili irekebishe utaratibu wa kutumia umeme ili kuongeza tija hii ya

matumizi ya miti na mkaa na vitu kama hivyo. Lakini bila hivyo hatutasaidia sana katika kuepusha hatari inayotokea ya jangwa la nchi.

Mheshimiwa Spika, ukiangalia, nchi nzima na hasa kule kwangu, Wilaya yangu ndiyo inayolisha Mbeya nzima kwa mkaa na ukija Mbozi, miti yote imekwisha na hata visima vingi vya maji ya moto kule Songwe vimeanza kukauka. Lakini sasa unafanyaje? Kwa sababu sasa Viongozi wa Mbeya wenyewe wanatumia mkaa; sasa wafanyeje? Huwezi ukadhibiti hali hii ukaweza kukinga na kuongeza hali ya maendeleo ya mazingira katika nchi. Ni ngumu sana! Nadhani iko haja ya kuliona hili.

Mheshimiwa Spika, lazima tukumbuke kwamba tunalo janga la Taifa la gonjwa hili la Ukimwi lisilotibika. Lakini ugonjwa huu hauwezi kupata dawa kwa sababu dawa nyingi zinatokana na miti na wanyama katika dunia hii ambao wamelindwa katika mazingira yaliyo sahihi. Lakini sasa kama hatutazingatia itakuwa ni bure tu kufikiria kupata dawa za tiba za Ukimwi.

Mheshimiwa Spika, tukumbuke ndui ilipoanza iliua watu wengi sana. Lakini ilikuja kutibika kutokana na wanyama na kule Japan kutokana na samaki. Sasa kama leo hii samaki wote tunavua tunakula tunamaliza, hii tiba na utaalamu wa utafiti huu tutaufanya wapi na tutapata wapi? Kwa kweli kuna hatari ya ugonjwa huu kutokukabiliwa kama tunavyotegemea. Mimi nadhani Idara zinazohusika na usimamizi wa mazingira hazijawa makini. Leo watu wanakata magogo, hawapandi miti. Wenzetu Ulaya wanapanda miti halafu ndio wanai-*phase* kwa utaratibu wanaokubaliana. Lakini sisi tunatoa leseni watu wakate miti, wapasue mbao, wasafirishe magogo nchi za nje ambayo hawakupanda, ni kufyeka tu kwa manufaa na utajiri wao binafsi. Sio kwa manufaa ya nchi! Nadhani hili litatuletea matatizo zaidi. Ni lazima Idara inayohusika iwe imara na watumishi wanaosimamia mazingira. Tusipokuwa na watu wenye kudhamiria kukinga hali hii, hatutakwenda mahali popote. Ni lazima wawe ni watu wenye uchungu na hali tunayoipata.

Mheshimiwa Spika, leo hii Dodoma ni hatari sana. Mnaona hali ya joto inavyozidi, ingawa watu wanasema aah, joto hili ni dalili ya mvua kukaribia. Lakini ni uharibifu wa mazingira! Nenda uone mikaa, hata sasa hivi nenda hapo njiani utapata magunia mengi ya mkaa yamezagaa na hali ya upepo sio nzuri na hakuna dalili nzuri kwa mvua mwaka huu. Hii ni hatari, ingawa watu wachache wanachoma mkaa wananufaika kwa manufaa yao, lakini kwa hasara kubwa ya nchi hii.

Kwa hiyo, nchi hii tutaipeleka kwenye hasara kubwa na balaa kubwa kwa faida ya watu wachache wenye uchoyo wa kunufaika binafsi. Hawa watu wanaochoma mkaa ni watu wenye nguvu kabisa, wangeweza kulima na kuzalisha, lakini nguvu zote hizi wanapeleka kuharibu misitu na kunufaika kwa kuchoma mkaa.

Sasa nadhani lazima tuweke watu wenye kuweza kudhibiti hali hii. Watu wa namna hii wakikamatwa, basi wawekwe mahali ambapo wanaweza wakafundishwa namna ya kuzalisha zaidi wakapata kipato na wakaendelea.

Mheshimiwa Spika, suala lingine kweli tutazuia hali ya uchafu katika Miji yetu ya sehemu mbalimbali kama mwenzangu alivyosema kwamba anazuia mabasi yote yasisimame kuchimba dawa,lakini hata hapa Mjini kuna vyoo vya kulipia. Hivi watu wangapi wana uwezo wa kulipia hivi vyoo vya hapa Mjini? Matokeo yake ndio haya! Watu wanakwenda kujisaidia kwenye kuta za nyumba za watu. Sasa ni vizuri basi Serikali ilione hili. Nchi nyingine vyoo vya namna hii *(public latrines)* vinawekwa katika usimamizi maalum, sio kwa kulipia kama hapa. Nenda hata kule Sokoni kwenye vyoo vya namna hii, watu wanakwenda wanajisaidia sehemu nyingine zisizofaa kwa sababu ya taratibu hizi. *(Makofi)*

Hata hii mifuko ya *plastic* tunasemea juu ya mifuko ya *plastic,* lakini kuna kiwanda cha *NAPAC.* Kiwanda hiki kinaweza kabisa kikatengeneza mifuko ya karatasi zinazooza, lakini tumekiangalia? Tumekipa msaada ili kisaidie kupunguza tatizo hili? Iko haja ya Serikali kusaidia kiwanda kama hiki ili kiweze kuzalisha karatasi zinazoweza zikasaidia kupunguza hizi *plastics* zisizooza na zilizoharibu sana hali ya mazingira yetu hapa nchini kote.

Vile vile tuunde Mabaraza ya Wenyeviti wa Vitongoji ambao watasimamia katika maeneo yao uharibifu wowote wa misitu, ukataji wowote wa miti na tuache kutoa leseni Wilayani au Mkoani kwa kuwapa watu waende wakate miti kule bila kupitia kwa vijiji na vitongoji hili tu ndilo litakalotusaidia.

Mheshimiwa Spika, vinginevyo tutakuwa tunazungumza hadithi ambayo haina mwisho na vile vile adhabu zinazotolewa ni nyepesi mno. Ni nyepesi kwa kweli hawa watu wanaoharibu mazingira ni watu wenye nguvu. Hivi kwa kweli wakifungwa tukaacha kulipa fedha au faini si wangezalisha zaidi magerezani.

Mheshimiwa Spika, naomba kuunga hoja ya Muswada huu na naomba tuzingatie. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MHE. FRANK G. MAGHOBA:** Nakushukuru Mheshimiwa Spika, kwa kunipa nafasi kuchangia hoja iliyo mbele yetu inayohusu sheria ya mazingira.

Mheshimiwa Spika, kwanza nimpongeze Waziri, pia Katibu Mkuu na wataalam wote wa Wizara hiyo. Nasema kwamba kwa kweli Sheria hii imechelewa. Imechelewa kwa sababu kuchelewa kwake kumesababisha madhara makubwa katika nchi yetu. Nchi yetu sasa hivi imekumbwa na janga kubwa ya kukata miti ovyo kama wenzangu walivyosema. Lakini pia maplastiki yamezagaa mitaani na hakuna Sheria yoyote ambayo imewekwa kudhibiti hali hiyo.

Mheshimiwa Spika, kwa kweli tumefikia mahali pabaya sana kwa kweli kwa hali ilivyo sasa hivi. Nikija kwenye suala la wakimbizi, sijui katika hii sheria inawagusa kiasi gani. Maeneo mengi ya wakimbizi miti imekatwa kwa ajili ya ujenzi wa nyumba zao, kuni na mambo kadhaa. Sijajua Sheria hii kama itakuwa inawagusa, kwa sababu ni sheria ambayo kwa kweli wakimbizi ni watu wa mataifa mengine. Sielewi kama kweli katika Sheria hii inawagusa kiasi gani. Hata kama haiwagusi basi ningeomba tuwawekee

sheria iwaguse kwa sababu hao wamekuwa chanzo kikubwa katika uharibifu wa mazingira katika nchi yetu hasa kwa kukata miti sehemu ambazo wanaishi. Najua Tanzania tumekuwa wakarimu kiasi kikubwa, tumewakaribisha, lakini wakimbizi hao wamekuwa wakituharibia mazingira yetu na kupata hasara kubwa huku wao wenyewe wakishamaliza au nchi zao zikipata Uhuru wanarudi wakituacha katika hali ngumu ile ile.

Mheshimiwa Spika, suala la mazingira nadhani kama Watanzania hatujatilia maanani sana na nimlaumu Mheshimiwa Waziri anayehusika kwa sababu kwa kweli nitazungumzikia kitu kidogo sana kuhusu suala la kiwanda cha *KTM.* Hivi karibuni, tarehe 31 Oktoba, 2004 kabla sijaja huku niliitwa na wananchi wa Kizinga ambao wamezungukwa na kiwanda hiki.

Mheshimiwa Spika, ukiangalia hali halisi ya kiwanda kile, ukiingia kwa ndani kwenye kiwanda kile unaweza ukaona ya kwamba mambo ni mazuri. Lakini ukienda kuangalia maeneo ambayo maji yanaririka kutoka kiwandani unaweza ukalia kutokana na hali ilivyo.

Mheshimiwa Spika, nilijionea mwenyewe nilipokwenda kuzungumza na wananchi hao kwamba maji yale yanayotiririka yanavuja hovyo. Kwa sababu ile mifereji ambayo ilitengenezwa, haijatengenezwa kiuimara na kiutaalam kwamba maji yasivuje. Matokeo yake watoto wadogo ambao wanachezacheza huwa wanaenda kuchezea maji yale kwa kupikiapikia na kunywa.

Mheshimiwa Spika, leo hali ya watoto walioko maeneo yale ni mbaya sana kwa vifua na nina wasiwasi kwamba inaelekea mapafu yao pia siyo watoto tu hata wananchi ambao wanakaa kwenye maeneo yale mapafu yao hayako salama. Pia nitamwomba Waziri wa Afya aunde Tume ndogo akawapime wananchi wangu wale tuone wana magonjwa gani tuweze kuwatibu mapema kabla.

Mheshimiwa Spika, suala hili kama Serikali haikutilia mkazo kumdhibiti mwenye kiwanda cha *KTM* nadhani tutapata madhara makubwa ya kuwakosa wananchi wetu. Ni kweli Serikali inapata faida katika kiwanda kile kwa sababu inalipwa kodi. Lakini ni kitu gani bora sasa kodi au maisha ya Watanzania ambao tunawaongoza. Wamenituma, kwanza nilifurahi sana baada ya kusikia Muswada huu upo, wametuma kwamba wanaomba kile kiwanda kwanza kifungwe wakati wanafanyiwa utaratibu wa mifereji ile kudhibiti pamoja na moshi ambao kwa kweli ni nzito, wananchi wa maeneo yale wanavuta moshi nzito kwa hewa ambayo siyo ya Mungu.

Kiwanda kile kifungwe bila mjadala, kwa sababu kwanza viongozi wengi sana wanakwenda kwenye kiwanda kile, akiwemo Waziri mwenyewe. Lakini nadhani Waziri anapokwenda pale wenye kiwanda wanamchukua na kumwonyesha Waziri mle mle ndani kabla hajaona kunakohusika huko nje.

Kwa hiyo, ningeomba Waziri kwa kweli kwa hatua hii maana yake wameniambia wao wako tayari kujitoa mhanga kuharibu kiwanda. Isingekuwa vizuri kufikia hatua hiyo, kwamba watu wafikie hatua ya kujitoa mhanga kwa kukiharibu kiwanda. Nadhani

uwekwe utaratibu nzuri kwamba kile kiwanda kifungwe, kifanyiwe utaratibu unaokubalika, kwanza kikubakie kwamba maeneo yale kilipojengwa kiwanda ni maeneo ya wananchi na sijui nani alitoa idhini hiyo ya kujenga kiwanda katikati ya watu. Sijui ni kitu gani kimetokea.

Mheshimiwa Spika, baadhi ya viongozi wetu wana matatizo na ndiyo maana tunasema viongozi tunakwamishwa kwa sababu ya mambo haya haya. Haiwezekani unajua kabisa kwamba sehemu hii ni watu wanaishi, wewe unatoa idhini kiwanda kijengwe ambacho kwa kweli kinaleta madhara makubwa sasa hivi. Nadhani kwamba kile kiwanda ni mashine, yale mashine yahamishwe yapelekwe sehemu nyingine. Nina maeneo mengi Kigamboni ambayo ninaweza nikampa yule mtu akajenga kiwanda na kazi ikafanywa kama kawaida. Lakini sehemu hiyo haiathiri watu wengine.

Mheshimiwa Spika, katika hili suala nitalipigia kelele sana. Nimeandika barua ambayo nataka kumpelekea Rais pamoja na Mheshimiwa Waziri nitampa nakala. Kwa sababu naona kwamba viongozi wamekwenda pale, amekwenda Makamu wa Rais ambaye ni Marehemu, Dr. Omar Ali Juma, akazungumza na wananchi hakuna majibu yaliyotoka pale.

Amekuja Mheshimiwa Waziri, nadhani alizungumza kwamba warekebishe utaratibu wa moshi ule na maji yale. Lakini hakuna kitu kilichofanyika, ukipita pale baada ya siku mbili tatu wanafungulia maji kama kawaida.

Hiyo, ni kwa nini tusiseme? Kwa nini tufikie hatua kwamba mtu mmoja atudhibiti. Maana yake sasa hivi imefikia wananchi wanasema kwamba Serikali imewekwa mfukoni na *Jeta, Jeta* ni kiwanda cha *KTM*. Hivi ni kweli Serikali imewekwa na yule Mhindi? Maana yake mimi nakubaliana hivyo kwa sababu haiwezekani suala hili tumelizungumzia zaidi karibu mitano na kumi inakwenda tu tunazungumzia suala moja hilo hilo la *KTM* kwa nini?

Mheshimiwa Spika, kwa kweli mimi nasema wazi kwamba suala hili tulichukulie uzito, Serikali ilichukulie uzito ili tusije tukaonekana kwamba wananchi tunaowaongoza sasa hatuwathamini kwa sababu tu tunachukua kodi kwenye kiwanda kile. Kodi haiwezi kuwa ya maana kuliko maisha ya binadamu. Leo wananchi wale wanakohoa ovyo ovyo. Ukikaa nao dakika moja unaweza ukakimbia kwa jinsi wanavyokohoa kwa nini?

Mimi nadhani tufikie hatua kile kiwanda kifungwe, kifanyiwe utaratibu mpya, ikiwezekana kihamishwe. Aidha, kama mwenye kiwanda ana uwezo ahamishe watu wote wanaokaa maeneo yale awaondoe ili kiwanda chake apanue.

Mheshimiwa Spika, aidha, nashauri kitu kingine, kwa sababu sasa gesi ya Songo Songo inafanya kazi basi atumie gesi ya Songo Songo kupunguza ule moshi wakati tunafanya utaratibu wa kukihamisha kile kiwanda. Vinginevyo mimi naungana na wananchi wangu kwamba kile kiwanda kikiharibika tusije tukashangaa ni kwa sababu watu wamechoka wanaonana na viongozi wao, hatuchukui hatua za madhubuti kuwasaidia kuokoa maisha yao.

Aidha, kile kiwanda ukikiangalia vizuri kimejengwa kienyeji, kina nyufa chungu mzima. Ukizunguka kile kiwanda kina nyufa chungu mzima, yule mjenzi kile kiwanda kimejengwa bila kutumia ma-*engineer* na wataalam wanaokubalika. Ukizunguka kile kiwanda utakuta kina nyufa na nyufa zile zinakaribiana kabisa na watu ambao wamezunguka kile kiwanda sasa ni hatari, kimewahi kubomoka mara mbili kile kiwanda, wananchi waliponea chupu chupu kuvunjjika miguu au kupoteza maisha yao. Lakini sasa utakuta kwamba anakuja anazibaziba bila utaalam wa kutosha. Sasa hii ni hatari, kama tunathamini kodi kuliko maisha ya Watanzania siamini kama kweli Serikali iko katika hali hiyo.

Mheshimiwa Spika, pia suala la sheria hii, nasema kwamba pamoja na kwamba sheria iko kwa ajili ya kudhibiti hali hii ya mazingira au uchafuzi wa mazingira, lakini nasema wazi kwamba elimu kama haikutolewa kwa Watanzania, suala la mazingira bado litaendelea kutusumbua siku hadi siku. Kwa hiyo, ningeomba elimu itolewe, kwa wananchi wote ili hii sheria waijue kwamba mtu akionekana anajisaidia hadharani akamatwe na kuwe na kifungu au kulipa faini. Mtu akitupa karatasi ovyo akamatwe, nchi za wenzetu ni safi, hata kwa mfano mimi nilikwenda Afrika Kusini, ukiwa na karatasi mkononi unaogopa kutupa popote pale. Kwa sababu huoni karatasi popote pale na sisi Watanzania tumekuwa watu wa ajabu, nchi yetu ni nzuri lakini tumeichafua, sielewi kwa sababu gani. Nadhani elimu inahitajika kutolewa. Itolewe elimu ya kutosha juu ya mazingira yetu.

Mheshimiwa Spika, uharibifu wa mazingira siyo kutupa takataka tu, hata kelele pia ni uchafuzi wa mazingira. Nadhani humu ndani pia tunachafua hali ya mazingira. Kwa hiyo, tunatakiwa tuangalie utaratibu wa kutumia vipaza sauti vyetu zisitoe sauti kubwa ili sisi huku kwa sababu tunasikilizana basi tusije tukafikia hatua hiyo. Maana kupiga kelele pia ni uchafuzi wa mazingira. Kwa hiyo, naomba tuangalie suala hili.

Mheshimiwa Spika, kuna suala la kupitisha mifugo mijini katikati ya mji, ni tatizo pia la kuchafua mazingira, ng’ombe wanapita katikati ya mji, wanaacha vinyesi mle, ni tatizo. Hilo pia ni uchafuzi wa mazingira. Kwa hiyo, ningeomba Serikali hii Sheria kweli kama nilivyosema ifanye kazi kweli na sheria hii ipelekwe kwa wananchi, waielewe vizuri ili iweze kufanya kazi barabara. Ili mtu anapokuchukulia hatua, akuchukulie ambayo kweli inamhusu.

Mheshimiwa Spika, siungi hoja mkono mpaka nitakapopata maelezo haya. Ahsante. *(Makofi)*

**MHE. BEATUS R. MAGAYANE:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ili na mimi niweze kuchangia Muswada huu muhimu wa mazingira. Nianze kwa kumpongeza Mheshimiwa Arcado Ntagazwa, kwa kuchaguliwa kwake kuwa Rais wa Baraza la Mazingira Duniani. *(Makofi)*

Kuchaguliwa kwake kwa kweli ni sifa kubwa kwa nchi ya Tanzania, lakini nina hakika ni kwa sababu ya umahiri wake katika kazi hii ya uhifadhi wa mazingira. Nampongeza sana na kumtakia kila la kheri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Muswada uliopo mbele yetu ni Muswada muhimu katika maisha ya kila siku ya binadamu. Lakini katika hali ya kawaida huwezi kuzungumzia masuala ya mazingira na hifadhi yake bila kuhusisha kwa karibu sana na dhana mzima ya umaskini. Kwa hiyo, Muswada huu na dhana mzima na mtazamo mzima wa Muswada huu ni lazima uhusishwe na mkakati ambao kwa bahati nzuri uko katika Ofisi moja, mkakati wa kuondoa umaskini na kwa sababu hiyo ni lazima Sekta zote zihusishwe katika hifadhi ya mazingira. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nakubali na natambua kwamba Muswada umegusa sekta zote na unahusisha kwa kiwango kikubwa maisha ya kawaida ya kila siku. Lakini ningemwomba Mheshimiwa Waziri aliangalie kwa makini kwamba katika kuhusisha, kuna sekta ambazo na Wizara ambazo ni muhimu sana katika utekelezaji mzima wa Muswada huu nazo ni Wizara ya Maliasili na Utalii, Wizara ya Kilimo na Mifugo na Wizara ya Nishati na Madini. Hivi vinachukua umuhimu wa pekee kabisa katika utekelezaji wa Muswada huu.

Mheshimiwa Spika, kwa kiwango kikubwa Wizara ya Nishati na Madini imekuwa ni kikwazo kikubwa sana katika utekelezaji na uhifadhi mzima wa mazingira. Kwa sababu kwa kupandisha bei ya umeme na upatikanaji wa umeme hata watu ambao wangeweza kutumia umeme sasa wamekimbilia kuni na mkaa. Hili ndiyo tatizo kubwa. Lakini kwa kuruhusu wachimbaji wa madini kila kona, wameingilia hata misitu ya hifadhi. Haieleweki ni nani anatoa vibali, Maliasili na Utalii au ni Wizara ya Nishati na Madini bila kujali hifadhi zilizopo za kitaifa. Kwa hiyo, ni vyema hizi Wizara sasa zikakaa pamoja kutengeneza mkakati wa pamoja kuweza kuokoa mazingira yetu tuliyonayo.

Mheshimiwa Spika, lakini pia Wizara ya Kilimo na Mifugo, wengi wa wakulima wetu ni wakulima wadogo wadogo na wategemea kile kilimo cha kuhamahama na wafugaji si wafugaji ni waswagaji. Kwa hiyo, lazima Wizara hizi tatu kwa karibu sana, Maliasili, Nishati na Madini, Kilimo na Mifugo pamoja na Wizara inayohusika na Mazingira zikae pamoja ili zitengeneze mkakati ulio endelevu.

Mheshimiwa Spika, wote tu mashahidi juu ya *cross boarder pollution* iliyoko na kuna ugomvi kati ya wenye viwanda wa Marekani na wakulima wa ngano wa Canada. Kuna ugomvi kati ya wenye viwanda wa India na wakulima wa mpunga wa China. Kwa sababu ya *cross boarder pollution* na Mataifa makubwa yamekuwa yakisita sana hata kusaini Mkataba wa Kioto ambao ungeweza kutulinda kwa kiwango kikubwa hasa nchi zisizokuwa na viwanda.

Mheshimiwa Spika, nayazungumza haya kwa sababu ya yale yanayojitokeza katika *section two,* Ibara ndogo ya pili ambapo Zanzibar imekuwa *excluded* katika huu Muswada. Naelewa kwamba Zanzibar walitunga Sheria yao ingawa haijaanza kutumika.

Lakini kama tusipohusha Zanzibar katika Muswada huu itatuletea matatizo sana kwa sababu ya hii ninayoiita *cross boarder pollution.* Lakini zaidi kwa sababu ya uchafuzi wa bahari maana yake Zanzibar tuna-*share* bahari moja na tusipokuwa na utaratibu wa Zanzibar kuhusishwa kikamilifu katika Muswada huu inaweza kutuletea matatizo katika utekelezaji kwa sababu uchafuzi wa bahari hautakuwa na mipaka.

Mheshimiwa Spika, Muswada umetambua fidia kwa waathirika wa mazingira. Lakini cha msingi ni vyema tukaelewa kwamba hakuna fidia ya uhai wa mtu. Kwa hiyo, cha msingi kiwe zaidi kuzuia hizi athari kuliko kutoa fidia kwa wale walioathirika. Tunafahamu watu walioathirika, Mheshimiwa Frank Maghoba amemaliza kuongea sasa hivi. Kuna kiwanda cha Saruji Wazo, moshi mnauona unavyojitokeza. Tuna dampo la Mtoni na lililokuwa dampo la Vingunguti. Pale Mtoni ni mbaya zaidi kwa sababu ile harufu tu iliyoko pale Mtoni kwenye dampo inatisha na sisi Kamati ya *LAAC* tulibahatika kwenda kutembelea pale kwa kweli sijui kwamba wale watu afya zao zikoje na wamelipwa.

Pamoja na kutambua hii fidia, hivi Muswada uko silent watalipwa vipi hawa waathirika wa mazingira na ni nani ata-*access* hiyo pamoja na kwamba ukurasa wa 22 *section 5* imetambua namna ya ku-*institute remade* na *cut off date* ni lini kwa sababu wako watu tayari wameshaathirika. Tunaanza lini ili na hawa ambao wameathiriwa na shughuli hizi za uzalishaji au za maendeleo, tuseme kama ya Jiji, ya kuweka madampo ni lini hasa itaanza kutumika hii sheria ili na hawa waliokwisha athirika na wao watambuliwe.

Mheshimiwa Spika, wengi wamezungumzia juu ya kuzagaa kwa taka zinazotokana na mifuko ya plastiki. Hili ni tatizo kubwa. Ningeshauri kwamba Wizara au Serikali itenge siku maalumu kwa mwaka au kwa mwezi ambapo kutakuwa na operesheni maalum ya kuokota hizi takataka *as a starting point.* Ili tuweze kuona tunaweza kufika wapi ili takataka zikaokotwa wakati Serikali inaweka mipango mingine ya kuweza kuzuia ueneaji wa takataka za plastiki.

Mheshimiwa Spika, tumezungumzia juu ya hifadhi ya mazingira mpaka ngazi za chini kabisa na *NGOs* zikapewa fedha kutekeleza hili jambo. Nashauri, hizi *NGOs* ziwe ambazo ziko *local* kwenye eneo lile lile. Zisiwe *NGO TX,* zinazotoka maeneo mengine bila kujua kinachoendelea pale ni nini na hizi *NGO* zitambuliwe kwa karibu kabisa na Halmashauri za Serikali za Miji zilizoko pia. Pamoja na kwamba *NGO* hizi zitapata pesa lakini uhifadhi wa mazingira iwe ni jambo la kudumu kwa wananchi na wananchi wasibweteke.

Mheshimiwa Spika, sheria imetunga faini ya kiwango cha chini ya shilingi 50,000/=. Mimi sielewi, maana yake Halmashauri zetu na Vijiji vina sheria ndogo ndogo ambazo zimewekwa na kutambuliwa na Serikali kama ni za hifadhi ya mazingira. Sijui sheria hii inaziunganisha vipi na hizi Sheria ambazo zipo na zimetambuliwa tayari na Serikali.

Mheshimiwa Spika, nashauri kwa sababu ya umuhimu wa hifadhi ya mazingira na uhusiano wake na umaskini na maendeleo na ustawi wa mwananchi wa kawaida. Napendekeza kwamba uhifadhi wa mazingira iwe ni sehemu ya mitaala katika shule zetu kuanzia shule za msingi mpaka chuo kikuu, *after all* pale Chuo Kikuu tuna kitu tunaita *Institute of Resource Accessment* ambayo mara nyingi inashughulika na masuala ya mazingira.

Ningeshauri kwamba moja kuwe na mitaala kuanzia shule za msingi. Lakini la pili, kuwe na Mahakama ya Hifadhi ya Mazingira kama vitu hivyo navyo na Mahakama ya Biashara na hii *NEMC* kwa sababu wametambuliwa na kupewa nguvu zaidi wao ndio wawe na nafasi ya ku-*prosecute.*

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MHE. JENISTA J. MHAGAMA:** Mheshimiwa Spika, na mimi kwanza kabisa naomba nikushukuru kwa kunipa nafasi ya kuchangia Muswada huu wa kupitisha sheria muhimu katika nchi yetu ya hifadhi na kutunza mazingira. Naomba nichukue nafasi ya pekee kumpongeza Mheshimiwa Waziri, Wajumbe wa Kamati wakiongozwa na Mwenyekiti wa Kamati, Mheshimiwa Mama Anne Makinda na wataalam wa Wizara kwa kufanya kazi nzuri ya uchambuzi wa Muswada na hatimaye kutuletea Bungeni. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kabla sijaingia katika mambo ya jumla nilikuwa naomba labda tu nitoe ushauri ama kwa namna nyingine nitoe ufafanuzi katika maeneo machache ambayo yanahusiana na Muswada wenyewe.

Mheshimiwa Spika, katika ukurasa wa 48 wa Muswada, kifungu namba 56, pale inaonyesha ni namna gani Waziri ataweza kuwa na nafasi ya kufanya *consultation* na Waziri anayehusiana na mambo ya ardhi katika ku-*declare* maeneo chepechepe ili yaweze kuhifadhiwa.

Mheshimiwa Spika, katika kifungu hicho, nilikuwa naomba nishauri kwamba kwa kuwa maeneo chepechepe yako katika maeneo yetu ya vijiji, yako katika maeneo yetu ya *Local Government* kwa nini tusiongeze pale *Minister responsible for Land* lakini tukaongeza na *Local Government* kusudi ile *consultation* inapofanywa kwa Waziri yule mwenye dhamana ya ardhi lakini akawasiliana pia na Serikali zetu za Mitaa kwa maana ya zile Serikali za Vijiji ama Halmashauri kwa ujumla na kuweza kuyatambua maeneo hayo chepechepe na hivyo basi kuweza kuyafanyia kazi vizuri na kadri inavyotakiwa ili kuyapa uhifadhi.

Mheshimiwa Spika, hilo lilikuwa langu la kwanza. Tunapofuatilia Sheria mbalimbali za ardhi tulizozitunga humu Bungeni ambazo zinaonyesha umiliki wa ardhi katika Serikali za vijiji na umma, inaonyesha kabisa kwamba ili uweze kuwa na madaraka ya kuishughulikia ardhi iliyoko katika umiliki wa kijiji ama umiliki wa umma ni lazima ufanye mawasiliano na umma wenyewe ama kijiji. Kwa hiyo, inanipa nguvu ya kuomba hoja yangu kama inaweza kukubaliwa basi iongezwe na *Local Authority* iwe

pia ni miongoni mwa watu wa kufanyiwa *consultation* katika ku-*declare* maeneo chepechepe ama kuyatoa maeneo chepechepe yaweze kutumika ama kuhifadhiwa.

Mheshimiwa Spika, Muswada huu kwa kweli utasaidia sana nchi yetu na wananchi kwa ujumla na mimi naomba labda nianze kwa kusema kwamba maendeleo ya jamii dhaifu yanahitaji sana msaada maalum na maeneo ya jamii dhaifu ni maeneo ya wananchi wa vijijini na wananchi wa vijijini mpaka sasa hivi mtaji wao mkubwa ni mazingira na ndicho kitega uchumi chao na ndiyo maisha yao kwa asilimia kubwa yanategemea sana mazingira hayo ambayo wananchi hao wanaishi.

Mheshimiwa Spika, nchi yetu ya Tanzania ina idadi ya watu wapatao milioni 35.3 katika Sensa ya mwaka 2002 tumeona. Lakini asilimia 51 ni wanawake na asilimia 80 ni wananchi wanaoishi katika maeneo ya vijiji na miji midogo na wengi wakiwa maskini wa kipato.

Ninapotoa *data* hizo naomba kuendelea kusisitiza hoja yangu kwamba hiyo ndiyo jamii dhaifu ambayo inahitaji msaada maalum na naamini kabisa mazingira ndiyo mtaji na raslimali pekee inayomilikiwa na jamii hiyo.

Mheshimiwa Spika, wanawake asilimia 51 katika nchi hii ya Tanzania ni watunzaji wakubwa wa mazingira na ndiyo waharibuji wakubwa wa mazingira kutokana na shughuli zao za kila siku na maisha yanayowatawala kama wanawake.

Mheshimiwa Spika, Tanzania sasa hivi inaongozwa na dira ya maendeleo katika kupambana na umaskini. Lakini mkakati wa uhifadhi na utunzaji wa mazingira umekuwa ni njia nyingine moja ambayo imepewa kipaombele kabisa katika kupambana na umaskini.

Mheshimiwa Spika, katika Muswada imeelezwa kabisa kwamba Baraza litajitahidi kutafuta fedha na kuiwezesha jamii kwa namna moja ama nyingine ili itoe ushirikiano wa karibu katika kupambana na mazingira.

Mheshimiwa Spika, naomba Baraza litoe kipaumbele kwa wanawake ambao ndiyo watumiaji wakubwa wa mazingira na ninaposema kwamba wanawake ndiyo ambao wataweza sana kusaidia utekelezaji wa sheria hii.

Mheshimiwa Spika, ukiangalia kabisa suala la mazingira haliwezi kwenda mbali na suala zima la maji safi na salama. Lakini suala la mazingira haliwezi kwenda mbali na suala zima la miundombinu bora ya kuleta maendeleo.

Mheshimiwa Spika, suala la mazingira haliwezi kwenda mbali na suala zima la kupambana na magonjwa mbalimbali ya kuambukizwa kama vile vile kipindu pindu, malaria, kuharisha, homa za matumbo na magonjwa mengine yanayofanana na hayo. Lakini suala la mazingira linahusiana kwa kiasi kikubwa sana na umuhimu wa upatikanaji wa teknolojia nyepesi na rahisi lakini za kisasa za kuboresha kilimo na shughuli mbalimbali za kiutendaji za wanawake na jamii mzima ya Watanzania.

Mheshimiwa Spika, suala hilo pia la uhifadhi wa mazingira haliwezi kwenda mbali na suala zima la kuangalia namna gani tuinaweza kuepukana na majanga mbalimbali ya nchi yetu. Vile vile suala la hifadhi ya mazingira haliwezi kwenda mbali na uduni wa mawasiliano katika maeneo ya vijijini.

Mheshimiwa Spika, ninaposema hivyo ninaendelea kuonyesha ni kwa kiasi gani Sheria hii itamkomboa mwanamke na inaweza kusababisha mabadiliko makubwa ya hifadhi ya mazingira na kuleta hali mbadala katika nchi yetu ya Tanzania na kama wanawake watawezeshwa na kuelimishwa vya kutosha katika mambo hayo ambayo nimeyataja hapo juu, sina shaka tunao uwezo mkubwa wa kubadilisha mazingira yetu katika nchi yetu yakaondoka na tatizo ambalo tunakabiliana nalo sasa hivi na kuyafanya yawe safi na kuyafanya yawe salama.

Usafi kwa kiasi kikubwa hunasimamiwa na wanawake na kama nilivyosema kama tutaweza kupata nishati mbadala za kutumia katika masuala mazima ya uandaaji wa chakula na kadhalika tuondokana na matumizi ya kuni, tukaondokana na matumizi ya mkaa, basi tutakuwa tumewasaidia wanawake kusaidia kwa kiasi kikubwa kupambana na uharibifu wa mazingira.

Mheshimiwa Spika, nasema kwamba sheria hii imekuja wakati muafaka na ninaamini kabisa kwamba uko umuhimu wa kuzingatia Sheria hii na kuifanya ifike katika maeneo ya asilimia hiyo 80 ya watu niliyoisema ambayo wengi wanaishi katika vijiji na miji midogo ambako pia wanahitaji sana kushirikiana na Serikali yao katika kuyatunza mazingira.

Mheshimiwa Spika, sheria hii naomba izingatie pia kuwepo kwa vyombo vitakavyokuwa karibu na wananchi na vitakavyosaidia kutoa mchango wa mwanzo wa kupambana na wale wote watakaonekana kwamba wanakiuka taratibu za Uhifadhi wa Mazingira.

Mheshimiwa Spika, nikichukua mfano katika sheria ya Ardhi, tunayo Mabaraza ya Kata na Mabaraza ya Kata yamepewa dhamana kubwa sana ya kuanza kushughulikia kesi zinazohusu ardhi katika maeneo ya Kata. Kwa hiyo, nilikuwa nashauri kwa kuzingatia sheria nyingine ambazo zipo na vyombo vingine ambavyo tumeshaviunda katika Maeneo ya Vijiji, Maeneo ya Kata, Maeneo ya Mitaa, basi Sheria hii ingepewa nguvu pia na vyombo hivyo vikaweza kushughulikia pale kunakotokea mlipuko wa haraka wa Uharifu wa Mazingira katika maeneo husika.

Mheshimiwa Spika, kama nilivyosema hapo mwanzo miundombinu ya usafirishaji ni migumu kwa hiyo, hiyo itasaidia sana.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja na nautakia Muswada huu upite vizuri. *(Makofi)*

**MHE. PROF. JUMANNE A. MAGHEMBE:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kunifikia haraka namna hii. Nashukuru sana kupata nafasi na mimi nitoe mawazo katika sheria hii ya Mazingira.

Kwanza ningependa niishukuru Ofisi ya Makamu wa Rais kwa kazi kubwa wanayofanya katika kusukuma *agenda* ya Mazingira hapa nchini. Napenda sana kumshukuru Mheshimiwa Arcado Ntagazwa, kwa kweli kwa kazi kubwa anayofanya katika kujenga utamaduni wa kutunza mazingira nchini kwetu na namshukuru zaidi kwa kuwa na *concern* kubwa katika uchafuzi wa mazingira hasa ambao umeliathiri hata Ziwa jipya kule kwenye Wilaya ya Mwanga. Ahsante sana *Senator.*

Mheshimiwa Spika, suala la mazingira yetu unaweza kulifananisha na suala la mtu kufunga madirisha yote ya vioo kwenye gari wakati kuna jua kali sana. Baada ya muda mfupi utakuta gari lina moto mkubwa sana na dunia yetu hivyo hivyo. Inapokuwa na jua linawaka halafu nje ya dunia kuna mtandao mkubwa sana wa hewa mbaya ya *Carbon dioxide* basi linakuwa kama gari limefungwa vioo, *Carbon dioxide* na *gases* nyingine au hewa nyingine za *Carbon dioxide* ambazo zina *molecule* kubwa.

Hali hii basi zinakuwa kama madirisha yamefungwa kwa hiyo joto linapanda ndani ya dunia. Sasa *Carbon* hii inatoka kwenye viwanda lakini hapa kwetu zaidi inatokana na kuchoma Misitu ovyo, vumbi kuinuliwa na kuwa sehemu ya utandao huo. Ili tuweze kufungua madirisha sasa tuwe na hali nzuri, basi mimea hasa Misitu ndio inayoweza kutumia *Carbon dioxide* hiyo na bahati nzuri inapotumia hiyo *Carbon dioxide* inazalisha *Oxygen* na kufanya mazingira yetu yakutumia hewa yawe mazuri. Pia Misitu hii huzuia upepo ambao unavumisha vumbi na kuchukua udongo lakini pia misitu hii inasaidia kujenga kiwango cha unyevu kwenye hewa na hivyo kusaidia katika upatikanaji wa mvua kwa uhakika na haraka.

Suala lingine kubwa sana ambalo nitalitolea mfano, ni kuwa Misitu pia inasaidia maji ya mvua kuingia kwenye udongo na Mito yetu kuwa ya wakati wote badala ya kuwa ya msimu.

Mheshimiwa Spika, sasa katika nchi yetu ukataji wa miti umefikia kiwango cha kutisha. Uondoaji wa mimea na utando wa mimea hasa misitu unakwenda kasi mno. Watu wanakata miti kwa visingizio vya aina zote. Watu wanachoma mkaa kwa kiwango ambacho hakijawahi kutokea. Haijawahi kutokea. Mkaa unaochomwa nchi hii unatisha. Katika Milima yetu mikubwa kama Mlima Meru, Kilimanjaro, Pare, Usambara, Ukaguru, Uluguru, Nguru, Uzungwa na Milima mingine miti imekatwa kiasi ambacho hakiwezi kuelezeka. Kinatisha kweli kweli na athari ya kwanza imeshaanza kuonekana katika Mlima Kilimanjaro, ukiendesha gari kutoka Himo mpaka Arusha hakuna hata Mto mmoja wakati wa kiangazi unapita chini ya daraja. Mito yote imekauka. Halafu hatuoni kama kuna tatizo. Mito yote imekauka. Ukitoka Dar es Salaam unakuja Dodoma utaona Mto Mkubwa kabisa, Mto wa Wami umekauka. Mto ule utakaukaje? Milima ya Nguru, Ukaguru imechomwa moto yote. Imekatwa miti yote na imechomwa mkaa ambao umepelekwa Morogoro na Dar es Salaam. Kama hatuwezi kubadilika kidogo, baadaye tutashindwa kuishi kwenye nchi hii. Wenzetu wenye nchi za majangwa mnajua wanavyoishi kama nchi za Mali, Niger maana nchi hizi ziko umbali kutoka kwenye

*Equator* kama sisi. Tusishangae tukawa na jangwa kama wao. Jangwa hili la Somalia na Mashariki ya Kenya liko karibu na sisi kabisa hatuwezi kusema hatuwezi kuwa jangwa na tunavyosema tutakuwa jangwa watu wengi tunadhani kuwa ni mchezo tu. Lakini uchafuzi wa mazingira katika maeneo haya unatisha kweli kweli.

Katika mito hii mvua inaponyesha utakuta udongo wote unapelekwa baharani na kwenye Maziwa. Maziwa yote yana *slit* na kuna hatari Maziwa makubwa kama Victoria yakakauka. Sasa *consequences* au athari za Ziwa kama Victoria kukauka sijui kama wakati mwingine tunazifikiria. Victoria ikikauka maana yake hakuna unyevu wa kutosha kutoa maji ya mvua katika maeneo yote ya *Sukuma Land* na huko Tabora na Singida kwa hiyo eneo hilo litakuwa jangwa na sijui tutapata wapi maji?

Kwa hivyo, ni vema tujue kuwa nchi yetu ni sisi wenyewe tutaitunza. Hakuna mtu atayekuja kutoka nje atusaidie kutunza nchi yetu. Kwa hiyo, Sheria hii tunashukuru sana imeletwa wakati huu, lakini Sheria hii itekelezwe kwa nguvu kweli kweli. Tusioneane haya. Kuoneana haya maana yake tumeamua tutahama hapa au kuna mahali pengine tutakapoweza kuhamia na tunajua hakuna. Kuna lingine ambalo lipo humu. Sheria hii ingefaa isomwe pamoja na Sheria ya Misitu na Sheria za Wanyama Pori na zote ziwekwe kwa pamoja zitekelezwe kwa nguvu sana. Wote ambao mmesafiri kwa barabara mnaelewa ukitoka Dar es Salaam kuja Dodoma unaona Milima ya Uluguru imekatwa mpaka juu kileleni njiani kutoka Morogoro kuja mpaka Gairo hakuna tena miti. Kwa hiyo sheria hizi zingesomwa kwa pamoja. Tukazitumia kulinda mazingira yetu.

Kitu kingine ambacho kinatokea ni kwamba bioanwai wanaita *Biodiversity* kuna mimea mingi sana ambayo inapatikana Tanzania peke yake, haipatikani eneo lingine lolote dunia na hii huko baadaye *Chemical* zake zitatufaa sana. Wakati huu ni wakati wa *Information Technology* lakini miaka inayokuja itakuwa ni enzi ya *Chemical Technology* na *chemical* zetu tunazipata kwenye mimea yetu ambayo haipatikani mahali pengine. Lakini mimea hii yote inakatwa na kuchomwa mkaa kama vile kitu cha kawaida. Kwa hiyo, Sheria hii Sheria ya Misitu, Sheria ya Wanyama Pori na Sheria ya Kutunza Mali Hai kwenye Bahari na kwenye Mito lazima vitekelezwe kwa nguvu sana. Sasa ni vema katika kutekeleza hivi tukajua mambo machache, moja hivi ni kwani nini miti inakatwa kwa haraka namna hii? Jbu ni ili kupata kuni, mkaa, magogo, sijui ni kitu gani kimetuingia sisi Watanzania tunauza magogo.

*Cubic meter* moja tunawapa watu wanatupa shilingi laki mbili inapelekwa Indonesia wale wanaopeleka wanapata *10,000 dollars* mpaka *20,000 dollars.* Kwa mali wametupa laki mbili na sisi tupo tu, hivi sisi tumefanywa nini? Tumekata Misitu yetu yote na kuitoa bure. Tunapata *two hundred thousand shillings!* Basi kwa mali ya thamani ya shilingi milioni kumi mpaka ishirini. Kuna mtu mmoja alisema hapa Bungeni eti, amekopa ili akate Misitu. Nikakaa hapa nikasema Mungu wangu, sasa huyu anasemea tena ndani ya Bunge kwamba amekopa aruhusiwe akate zaidi. Tuna matatizo makubwa sana kwa hiyo kwanza Serikali yetu lazima iangalie kabisa bei ya magogo upya. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, ukienda Kenya kuna Kampuni moja inaitwa *Timsales* na mbao zilizoko kwenye *timber yard* si zao, zimejaa mbao zinatoka Tanzania, kwa sababu mbao za Tanzania rahisi sana, *sold for nothing.* Kila nchi ni marufuku kukata mbao kule kwao, wanakuja huku Tanzania. Nchi za China, Indonesia, Thailand wote wanakuja kukata hapa. Kwa hiyo, lazima Sheria hii itekelezwe kwa nguvu sana.

Mheshimiwa Spika, ya pili ni umeme umekuwa ghali sana. Hata kuunganisha Umeme kule kijijini kwangu katika Vijiji vya Nyumba ya Mungu na Njia Panda ambazo tumetafuta pesa kutoka kwa wafadhili tukaipa *TANESCO* iweke umeme. Wananchi wameshindwa kuunganisha umeme huo kwa sababu shilingi laki mbili mwanakijiji atapata wapi?

Kwa hiyo, hili lazima tuliangalie na umeme wenyewe lazima ushuke bei. Tuangalie pia *alternative sources* za kutengeneza umeme hasa kutoka kwenye makaa ya mawe ambayo Mwenyezi Mungu ametujalia mengi sana. Mafuta ya taa ni ghali mno.

Mheshimiwa Spika, nakushuru sana kwa kunipa fursa hii kutoa mawazo haya. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MHE. ABDULKARIM E. H. SHAH:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi hii kuweza na mimi kutoa mawili/matatu yanayohusu baadhi ya maelezo mengine yametolewa na Waheshimiwa Wabunge humu humu ndani nikaweza kuyachangia zaidi.

Mheshimiwa Spika, mimi ni Mjumbe wa Kamati ya Maliasili na Mazingira ni mmoja wa Wajumbe ambao tumeipitia vizuri kwa kina na utafiti mkubwa kwa kushirikiana na Mheshimiwa Waziri pamoja na jopo lote la wataalamu wake kutoka Ofisi ya Makamu wa Rais na Wataalamu kutoka nje ya hao kwa maana ya Chuo Kikuu na sehemu nyingine.

Muswada huu ni mzuri sana, wenzetu wanasema umechelewa lakini kila kitu kinakwenda kwa wakati. Mimi nasema umefika wakati wake na sasa tu tuupe nguvu kama ulivyoafikiwa japokuwa mmoja wetu anasema yeye ataunga mkono lakini ningemshauri angeunga mkono ili kuweza kumpa nguvu Mheshimiwa Waziri kuweza kuifanyia kazi hiyo hoja yake.

Mheshimiwa Spika, Tanzania tunaathirika kwa mambo mengi zaidi. Lakini wengi tu tunafikiria kwamba uharibifu wa mazingira ni kukata miti na mambo mengine yaliyokuwa kwenye ardhi. Lakini pia kuna siku Mheshimiwa Arcado Ntagazwa aliwahi kutuambia kwamba hata bahari inachafuka na inaharibu mazingira na watu walikuwa hawafahamu kwamba bahari nayo uwa inachafuka hata hewa uwa inachafuka.

Mheshimiwa Spika, ukitoka Mafia kama utapanda ndege kuja Dar es Salaam *time* za asubuhi kama kwenye saa moja moja ukiukaribia mji wa Dar es Salaam utaona hali ya ukungu jinsi ulivyojaa na ukungu ule sio wa mawingu ni uchafu wa moshi ambao unatokana na magari pamoja na viwanda vyetu. Kwa hivyo, naamini Sheria hii itasaidia sana katika kuhifadhi pia mtandao wa hali ya hewa katika nchi yetu. Mengi

yamezungumzwa kwa hivyo na wananchi kama nilivyosema wanahitaji elimu lakini kutokana na uwezo aliokuwa nao Mheshimiwa Waziri kupitia Wizara yake naamini elimu itafanyika na wananchi wote wa Tanzania wataweza kuelewa nini maana ya umuhimu wa kulinda mazingira ya nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, jana wakati Msemaji wa Kambi ya Upinzani anatoa hoja yake, bahati mbaya mimi nilikuwa nimetoka kidogo kwa shughuli za kikazi humu ndani. Lakini moja ya sehemu ambayo aliichangia ilikuwa ni Ibara ya (191) ambayo aliiandika yeye na kuisoma yeye mwenyewe kwamba inayohusu kuhusu mtu yeyote anayetenda kosa lolote kuhusiana na kipengele chochote kilichoelezwa ndani ya Muswada huu anatakiwa kulipa fani isiyopungua shilingi 50,000/= au isiyozidi million 50. Lakini mwisho aliendelea kusema maneno hayo kwamba sasa kama tunavyoelewa uharibifu wa mazingira ni wananchi walio na kipato kisichozidi shilingi 50,000/= kwa mwaka na wengi wanajipatia riziki zao kwa njia ambazo huhatarisha na kusababisha uharibifu wa mazingira na kuna wengine kama wakazi wa Mwambao kwa mfano, wa Mafia na Ukerewe akazidisha na kusema hasa Mafia, unaona ambao vyoo vyao ni ufukweni mwa Bahari kwa mantiki hiyo kijiji kizima kinaweza kufungwa gerezani kwani watakosa shilingi 50,000/=. Sisi Mafia tunakwambia hatuna dhiki ya kukosa shilingi 50,000/=. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, yalikuwa ni maneno ya karaha na maudhi ndani ya Bunge lako Tukufu. Lakini kwa bahati mbaya ndiyo ilikuwa nusura yake yeye aliweza yaani kutokana na kutokuwepo kwetu mimi na Mheshimiwa mama yake Mama Halima Kimbau basi yeye akaweza kunusurika.

Lakini ninachoomba kitu kimoja kwanza atuombe radhi watu wa Mafia na aombe radhi ndani ya Bunge hili, Mafia na Ukerewe ameandika na Ukerewe si kwamba labda nazidisha, atuombe radhi sisi watu wa Visiwani.

Pili humu atuombe radhi humu Bungeni, aombe radhi wananchi wa Mafia na Ukerewe kwa kutumia vyombo vya habari. Nimepigiwa simu jana usiku na leo wanasema kama hukuyazungumza hayo basi tutapambana na wewe. Sasa na sisi tuko wawili, tunaomba Mheshimiwa Mbunge kwa nia njema atuombe radhi na aombe radhi watu wa Mafia au athibitishe uchafu wetu.

Mheshimiwa Spika, Kamati ya Maliasili na Mazingira ilikwenda Mafia mwaka jana mwishoni na moja ya sehemu waliyotembelea au tuliyotembelea ni katika fukwe ya eneo la Kilindoni pale Mjini Mafia yaani Mji Mkuu wa Wilaya ya Mafia ni Kilindoni. Pembeni mwa sehemu tuliyokuwa ni Hoteli ambayo inamilikiwa na Mheshimiwa Mama Halima Kimbau, nje ya wigo wa hoteli yake pana dago la ndugu zetu wa Kikojani. *(Makofi)*

Kwa asilimia naweza nikasema 99 uchafu wa pale unasababishwa na ndugu zetu hawa wageni waliotoka nje ya Wilaya yetu na kuja kuchafua mazingira ya Wilaya yetu. Sasa namhakikishia kwamba uchafu huo haufanywi na watu wa Mafia bali hufanywa na wananchi kutoka nje ya Mafia. Naona haya kuwataja wanatoka sehemu gani itakuwa siyo

ustaarabu au ajitayarishe kuwajibika kwenye Kamati ya Haki, Maadili na Madaraka ya Bunge na nakuambia mimi ni mjumbe. Nakutaarifu kuwa mimi ni mjumbe wa Kamati hiyo. Nitataka utoe *evidence* zote za kutuhakikishia kwamba sisi watu wa Mafia hatuna vyoo. Hali ya Visiwa vya Mafia sawasawa na Visiwa vya Unguja na Pemba sawasawa na katika jimbo lako la Kojani ulikotoka Mheshimiwa Mbunge Ali Said Juma.

Mheshimiwa Spika, tumesikitishwa sana na kauli hiyo aliyotoa. Wala sikuwa na haja yoyote ya kuyasema juu ya Muswada huu kwa sababu umekamilika na sasa bado kutekelezeka. Lakini yameniudhi na kutukera sisi wananchi hasa kwa kuzungumza na ukiangalia mimi baada ya kutoka pale, tulifuatana pamoja, nilimtia kwenye gari, akaenda sehemu ile ambayo yeye anakwenda nikasema twende nikupeleke, akanihakikishia kwa sababu haya maneno mimi nimeongea kwenye Bunge kwa sababu nina uhakika. Uhakika huu umeupata wapi? Akasema Bwana, sisi kule kwetu tulimtuma mjumbe mmoja kuja kuimarisha chama chetu cha *CUF* unaona!

Huyu mjumbe anaitwa Ramadhan Jumanne Ramadhani Ngude kutoka Kisarawe. Yeye ndio akasema amefanya utafiti na kusema kuwa watu wa Mafia tunakunya porini na baharini.

Sasa tunasema tunashukuru sana kwa huyu Bwana Ngude kuja kutuchambua sisi kule Mafia na nawaambia ndugu zangu wa Mafia hayo ndio matokeo ya watu ambao tunawapokea waliokuwa nje ya taratibu na hulka ya Kisiwa chetu cha Mafia. *(Makofi)*

Tujihadharini na kundi hili ambalo limekaa na kuja kuvamia na kuja kutukashfu, kututukana ule wema wetu wa kukaribisha wageni sasa ndiyo unakuwa kashfa dhidi yetu.

Mheshimiwa Spika, sina mengi ya kusema naunga mkono hoja hii lakini na kuwaomba ndugu zetu wa jimbo analotoka Mheshimiwa Arcado Ntagazwa, watusaidie kiongozi wetu huyu kwa umahiri wake wa juu ya utetezi wa mazingira. Wasije wakapotea *step* kwa ulaghai kwa mtu akayekuja kuja kusema jamani nipeni mimi huyu achane naye bado Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, inamhitaji hata kama sisi wengine hatukujaliwa kurudi lakini yeye naamini atakuwa mchango mkubwa kabisa kwa nchi hii kuhusu suala la mazingira na ndio maana hata dunia ikamtambua na kumpa kuwa yeye ndiyo Rais wa Mazingira wa Dunia hii.

Kwa hivyo, tunaomba kwa heshima kubwa ndugu zangu wa Kibondo huko watusaidie huyu kiongozi na Mwenyenzi Mungu amjalie uhai mrefu, uzima na sisi Mwenyenzi Mungu aturejeshe humu tuweze kuja kumuunga mkono ili tuweze kufanikiwa.

Mheshimiwa Spika, nashukuru sana na naunga mkono hoja hii mara milioni. *(Makofi)*

**SPIKA:** Hayo yaliyokuudhi Mheshimiwa Waziri hawezi kuyajibu kwa sababu yanahusu Bunge. Kwa hiyo, naweza kumsaidia kujibu kwamba kama amekuudhi kiasi hicho, utaratibu unakuruhusu kupeleka malalamiko rasmi kwenye Kamati ya Haki, Maadili na Madaraka ya Bunge ili yaweze kufanyiwa kazi. Sasa narudi kwa Mheshimiwa mtoa hoja ili ahitimishe hoja yake.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS (MHE. ARCADO D. NTAGAZWA):** Mheshimiwa Spika, kwanza nakushukuru kunipa nafasi hii. Lakini pia naomba idhini yako kwa yale aliyoyasema Mheshimiwa Abdulkarim Shah, Mbunge wa Mafia niombe hiyo iwe sifa na utukufu wa Mwenyenzi Mungu mwenyewe.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo ningependa kwanza niwatambue Waheshimiwa Wabunge waliochangia kwa kusimamia humu Bungeni na wa kwanza ni Mheshimiwa Anna Makinda, Mwenyekiti wa Kamati ya Bunge ya Maliasili na Mazingira na Mheshimiwa Ali Said Juma, Msemaji Mkuu upande wa Upinzani na Mheshimiwa Ireneus Ngwatura, Mheshimiwa Semindu Pawa na Mheshimiwa Job Ndugai.

Mheshimiwa Spika, wengine ni Mheshimiwa Edson Halinga, Mheshimiwa Frank Maghoba, Mheshimiwa Beatus Magayane, Mheshimiwa Jenista Mhagama, Mheshimwa Profesa Jumanne Maghembe na Mheshimiwa Abdulkarim Shah.

Mheshimiwa Spika, pia wapo waliochangia kwa maandishi nao ni Mheshimiwa Job Ndugai, Mheshimiwa Peter Kabisa, Mheshimiwa Khamis Awesu Aboud, Mheshimiwa Esha Stima, Mheshimiwa Frank Mussati, Mheshimiwa Dr. Aaron Chiduo na Mheshimiwa Khalid Suru.
Inawezekana kuna baadhi nimesahau au karatasi yenye majina nimeweka pembeni lakini nia na madhumuni ni kuwatambua na kuwashukuru.

Mheshimiwa Spika, ninao muda mchache lakini sidhani kama nitaweza kabisa kutoa maelezo kwa kila hoja iliyotolewa, lakini ukiangalia kwa ujumla wa hoja zilizotolewa.

Mheshimiwa Spika, unakuta maeneo ya matumizi kwanza kuwa na vyoo na kuvitumia na elimu kwa Umma ni suala la umaskini kuhusishwa na Hifadhi ya Mazingira nishati mbadala suala la dhana ya uzalishaji bora kiingereza wanaita ni *Cleaner Production and Sustainable Consumption* na suala la kuwashirikisha akina mama au wanawake na suala hili la siku zote la mifuko ya *plastic* na *Genetical Modified Organisms (GMO).*

Mheshimiwa Spika, suala la viwango kutumika katika udhibiti wa usimamizi wa mazingira na uchafuzi wa maji, hewa na udongo. Sasa Waheshimiwa waliopata nafasi ya kuchangia ama kwa kusema humu Bungeni au kwa maandishi karibu kila mmoja wao amegusia eneo hili.

Mheshimiwa Spika, ningependa nianze na hili la nishati mbadala ambalo namshukuru sana Mheshimiwa Profesa Jumanne Maghembe, Mbunge wa Mwanga amelisemea kwa jinsi ambayo hata Katiba ile Ibara niliyoinukuu nilipokuwa nawasilisha hoja aliposema Mheshimiwa Mbunge kwamba sijui sisi Watanzania tunakata miti sijui utadhani, mwingine angeweza akasema sijui Watanzania tumerogwa hivi kwa lugha ya kawaida kabisa.

Mheshimiwa Spika, sasa ukiisoma Ibara ya (27) Ibara ndogo ya (2) suala hili la kusisitiza kwamba tuwajibike kwetu sisi wenyewe kama Taifa linasisitiza. Inasema hivi Mheshimiwa Spika, kwa idhini yako; "Watu wote watatakiwa na sheria kutunza vizuri mali ya mamlaka ya nchi na ya pamoja, kupiga vita aina zote za uharibifu na ubadhirifu na kuendesha uchumi wa Taifa kwa makini."

Mheshimiwa Spika, sasa maneno yanayofuata ndio ya msingi sana kama watu ambao ndiyo waamuzi wa hali ya baadaye ya Taifa lao.

Mheshimiwa Spika, suala la kutumia kuni na Mkaa, kwa kupika au kwa matumizi mengine. Nina hakika sehemu ya umaskini wa Taifa letu inachangia sana. Kuna mahali nakumbuka nilikuwa nasoma wanasema: "Umaskini ni mchafuzi mkubwa sana wa mazingira". Kwa sababu ni umaskini unaotufanya tufike mahali Mheshimiwa Spika, tusiwe na Umeme au Nishati nyingine mbadala katika Vijiji vyetu ambavyo kama alivyosema Mheshimiwa Jenista Mhagama, ndiko wananchi wengi tunakoishi.

Sasa ni suala la umaskini ndiyo linafanya tusiwe na Nishati Mbadala huko kwingine na matokeo yake tunakata miti kwa ajili ya kuni, Mkaa kumbe tunajitengenezea umaskini zaidi na zaidi. Lakini kwa sababu Mheshimiwa Spika, inabidi pia tukiri pamoja na kwamba Taifa letu ni changa, lazima tuanze kuchukua hatua za kuondokana na hali hiyo. Mimi Jumapili iliyopita nilimshukuru Mungu kwamba ilifanyika Semina hapa ndani ya ukumbi huu ya kuelezea jitihada za Taifa letu za kutafuta namna ya kuwa na umeme na kufikisha umeme huo kwa wananchi wote vijijini. Najua haitakuwa kesho wala kesho kutwa lakini hazima hii ndio itatusaidia kuondokana na suala hili la kuharibu Mazingira yetu, nchi yetu kuonekana na kugeuka kuwa jangwa kwa sababu ya umaskini na tunatumia raslimali ya miti, misitu na vitu vingine kwa mambo ambayo hayaepukiki. Wakati mmoja nakumbuka nilikuwa katika nchi ya Denmark na kwenye Semina ile wakauliza mnawezaje kufanya maendeleo na hamna umeme.

Sasa mimi sikutaka kuwachekesha wale wazungu niliwaambia ukweli, kwamba kule kijijini nilikozaliwa Nyarugusu siku tunajua kuna umeme ilipopiga radi. Walicheka sana wale wazungu lakini ndio ukweli katika maeneo mengi ya vijiji vyetu hakuna umeme kabisa. Lakini kwa mkakati ule wa semina ya jumapili nadhani inshala baada ya muda tutafika na tutamaliza tatizohili kadri taifa letu linavyozidi kujiimarisha kiuchumi.

Mheshimiwa Spika, na nikiri kwamba suala la umasikini na mazingira nikama mapacha wale wanaozaliwa wameungana. Huwezi kushughulikia moja ukasema moja niweke pembeni nitashughulikia kesho. Ni kweli kabisa na hili napenda kukubaliana na usemi huo.

Mheshimiwa Spika, suala alilolizungumzia sana Mheshimiwa Mwenyekiti wa Kamati ya namna yetu, tabia zetu za kutupa takataka ovyo halafu unakwenda hata kwenye vyombo vya usafiri unafika mahali unasema haya abiria teremkeni mwende mkachimbe dawa tunamwelewa alikuwa na maana gani. Napenda nimshukuru sana na kupongeza.

Mheshimiwa Spika, mwenyewe Mheshimiwa Anne Makinda, kwa kukiri kutukumbusha kwamba ni vizuri wakati mwingine kama taifa huru mkaazimia kubadilisha tabia.

Lakini ni tuwe na nyezo basi za kufanya hivyo. Liko pendekezo amelitoa Mheshimiwa Mheshimiwa Esha Stima, kwamba mabasi yote ya abiria yawe na utaratibu wa kuwa na vyoo. Mbona katika nchi zingine magari yana vyoo ili badala ya kuchimba dawa na kuchafua mazingira na kwingine kueneza magonjwa. Magari haya yanayosafiri tunajua mwenyezi Mungu katujalia nchi yetu kubwa na wakati mwingine unaweza ukasafiri na ukapata matatizo ya tumbo, walau magari basi yawe na huduma ya choo ili tujaribu kupunguza hili tatizo la kuchimba dawa kwa maana iliyoelezwa.

Mheshimiwa Spika, napenda kushukuru kwa maoni na ushauri huo wa Elimu kwa Umma.

Mheshimiwa Spika, kwa kweli ninakubaliana kabisa, kabisa na Waheshimiwa Wabunge waliochangia kuhusu suala hili. Sheria hii ni kweli ni nzuri inaweka misingi ya kisheria na kitaasisi kuratibu yale tunayotakiwa kuyafanya katika suala la hifadhi na usimamizi wa mazingira. Lakini bila kutoa elimu ya kutosha na nashukuru Waheshimiwa Wabunge waliopendekeza tuanze kutoa elimu kuhusiana na suala la mazingira shule zetu za msingi hadi Chuo kikuu au vyuo vikuu na taasisi za elimu ya juu. Tusipotoa elimu tunaweza tukawa na sheria nzuri ya hifadhi na usimamizi wa mazingira lakini ikabakia kuwa ni sheria nzuri na labda kwa nadharia zaidi kuliko vile ambavyo tunategemea wananchi wakielewa na kuitekeleza tutakuwa tunapambana ilivyo na yale madhara yanatokana na uchafuzi na uharibifu wa mazingira.

Mheshimiwa Spika, kuhusu suala la uzalishaji bora, zana ya uzalishaji mimi namshukuru sana Mheshimiwa Frank Maghoba kwa kulikemea hapa na kwa kusema kweli kama nilivyonukuu katika kile kitabu katika jitihada za maendeleo. Mnapoanza kuwa na viwanda. Viwanda vile vinatoa moshi vinatoa maji kutoka viwandani. Inachotakiwa kama mambo yote yakienda sawa maji yanayotoka viwandani hayatakiwi yawe na athari yoyote kwa mazingira na afya ya binadamu.

Mheshimiwa Spika, lakini tunajua binadamu tulivyo hodari wa kukwepa litakiwalo na kufanya kinyume chake. Namshukuru kwa kutambua kwamba wakati

mmoja mimi na watalamu kutoka Ofisi ya Makamu wa Rais na Waheshimiwa Wabunge wa majimbo ya uchaguzi kutoka Temeke tulitembelea kiwanda kile.

Mheshimiwa Spika, tulichokiona pale na wenye kiwanda walichokisema ni kwamba na siku ile tulikuta umeme umekatika. Wakasema umeme unapokatika ni kweli kabisa kwamba mchanganyiko wa madawa yanayotumika kutia rangi vitambaa ili viwe khanga au vitenge na kitu cha namna hiyo unaathirika.

Mheshimiwa Spika, Lakini tulifika mahali kama nilivyosema siku zote kwamba sisi ni watumishi nikawaarifu wenye kiwanda kwamba tumefika kiwandani na Mkurugenzi wa Mazingira na Mkurugenzi Mkuu wa *NEMC* au mwakilishi wake na Mkurugenzi Mkuu wa kituo cha uzalishaji bora Tanzania *(Center for Clean Production of Tanzania)* nikawaambia hawa ni wataalam lakini niwakuwatumikieni sijui ni kwa kiasi gani mnawatumia. Wananiambia tunakushangaa Waziri mbona hatujawaona hapa kama nyinyi mlivyokuja. Nikawaambia kwa sababu hamtaki kutumia haki yenu hawa si wakaguzi wa kufanya kazi kama ule mtego wa panya ni wataalam wa kuja kukuelekezeni kuzuia uchafuzi wa mazingira.

Mheshimiwa Spika, nafurahi kwa wakati ule ilikuwa imekubaliwa na kiwanda kile walishaanza kupeleka watumishi wa kiwanda kupata mafunzo katika kituo cha uzalishaji bora ili kujihakikishia kwamba kiwanda hakitowi dutu chafu kweli kweli zinazochafua mazingira na kuhatarisha afya ya binadamu na mwishoni nilichokisema pale kiwandani na nina sema pia kwa viwanda vingine vyote. Kiwanda kinapo zalisha mali lakini katika kuzalisha mali kikao dutu zinazoathiri mazingira na afya ya binadamu. Mimi niliwauliza afya ya binadamu ikiathirika hatimaye ni kifo bidhaa zako utakwenda kuuza makaburini haiwezekani.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, ndio maana tunasisitiza suala zima la mazingira tunalitazama katika hifadhi ya mazingira kwa maana katika mazingira ndimo tunafanya shughuli za maendeleo iwe ya mtu mmoja au taifa lakini na afya ya binadamu kwa sababu ndiye mlegwa. Kwa hiyo, napenda nitoe wito kwa viwanda vyote wawatumie wataalam walioko katika Ofisi ya Makamu wa Rais waone kwamba shughuli zao haziathiri mazingira wala hazidhuru afya ya binadamu na nakubaliana na Mheshimiwa Mbunge Frank Maghoba sisi Serikali ya Chama cha Mapinduzi hatuwezi kuenzi kodi kama suala mbadala kwa maisha ya binadamu haiwezekani na ndio maana tunakuja na sheria hii hapa na sheria hii. Moja ya eneo la muhimu kabisa licha ya kusema kama kuna mkorofi na hataki kusikia adhabu itatumika.

Lakini tunataka elimu kwa umma ili sote tushirikiane kutunza mazingira. Kwa hiyo, tunapenda kuwa na vivutio vya kutunza mazingira zaidi kuliko ile eneo la kupata funga. Hili ni la msingi sana na nilitaka niliseme hilo

Mheshimiwa Spika, kuhusu suala la kuwashirikisha wa kina mama namshukuru sana Mheshimiwa Jenista Mhagama Viti Maalum aliyezaliwa katika mkoa wa Kigoma katika hospital ya Kabanga Kasulu ni mtetezi mzuri sana wa kina mama.

Mheshimiwa Spika, na sisi tunajua si msemo tu lakini ni kweli unapomfundisha mwana mama mmoja umefundisha zaidi ya mtu mmoja sasa ukiwa na mtetezi wa kina mama basi tunajua kutokana na msemo tunachokifanya nini. Kwa hiyo, nashukuru sana kuligusia hili na mkisoma Muswada kuna mahali tumezingatia ushirikishwaji wa kinamama kwa makusudi. Kwa hiyo, napenda nimpongeze na kumshukuru sana anatukumbusha lile ambalo tumelizingatia na ni la msingi.

Mheshimiwa Spika, kuhusu mifuko ya *plastic* na niseme inasikitisha kwa sababu nadhani ni Mheshimiwa Mwenyekiti wa Kamati, alisema tunapozungumzia matatizo haya ya uchafuzi wa mazingira utupaji ovyo wa taka na takataka. Pengine tunazungumzia tabia ya mtu mmoja mmoja ambayo moja moja miongoni ndio tunakuwa jamii ya watadhani na kweli inasikitisha lakini tunashukuru jinsi sheria ilivyoundwa pengine itatusaidia lakini la msingi ni tabia zetu. Inashangaza sana.

Mheshimiwa Spika, mtu ananunua chupa ya maji, maji nadhani ni safi na salama yuko safarini au yupo nyumbani kwake anakunywa maji halafu ile chupa kama yupo kwenye gari anaitupa tu huko barabarani. Sasa chupa zile ukichukulia mwendo, ile kasi ya gari pengine na upepo unaovuma wakati ule chupa ile ikipiga kioo cha gari inaweza kusababisha ajali na watu wakapoteza maisha yao. Lakini nani anasema unapotembea kwa basi sehemu ile ya barabara hakuna chupa tupu ya maji wala mfuko wa *plastic* aliyekwambia utupe ni nani.

Mheshimiwa Spika, mimi ninakumbuka nilipokuwa shule mwalimu wangu mmoja alisema hivi na ndio maana siku hizi Waheshimiwa Wabunge wengine wananishangaa nikienda pale kwenye ukumbi tunaponunua kadi za simu utakuta yale maganda ya kadi zile yametapakaa ovyo sasa nikifika pale walau huokota mawili, matatu nikaweka mahali pake sasa inanikumbusha nilipokuwa shule mwalimu wangu mmoja alisema ukikuta karatasi mahali ambapo si pake basi mahali paleni choo. Sasa haiwezekani barabara ikawa ni choo, haiwezekani kumbi zetu hizi ukakuta makaratasi ukasema basi ni choo. *(Makofi)*

Sasa tabia ya mtu mmoja mmoja tu kutojali hali ya kuwa safi na nadhifu. Sasa najua tumelipigia kelele suala hili la mifuko ya *plastic* na juzi nilipouliza swali la nyongeza nilisema katika hotuba ya bajeti tulisema Serikali tunachukua hatua ya kuipiga marufuku mifuko ile isiyooza na isiyorejelezeka *non recyclable* and mifuko isiyooza. Sasa Waheshimiwa Wabunge waliguna lakini naomba niseme tu.

Mheshimiwa Spika, Waziri wa Nchi katika Ofisi ya Makamu wa Rais ni sehemu tu ya Serikali na Serikali inautaratibu wake wa kufanya kazi. Tulikwishapata maagizo kutoka Kamati ya Bunge hili ya Maliasili na Mazingira na agizo lile linafanyiwa kazi kikamilifu, ni utaratibu tu kwamba Serikali hutoki mtu mmoja ukasema mimi ndiye hapana tunafanya kazi kwa pamoja *collective responsibility.* Tutakapomaliza mchakato huo tutaweka mambo hadharani na Bunge litajulishwa na kwa kweli tulikwisha sema tunataka mifuko hii ya *plastic* isiyooza na isiyoweza kurejerezeka ipigwe marufuku kuingia nchini na kutengenezwa nchini kwetu. *(Makofi)*

Hatuwezi kufanya kosa alilosema Mheshimiwa Frank Maghoba, tukajali kodi inayotokana na utendaji kazi wa viwanda hivyo lakini huku tunahataribu afya ya wananchi wetu.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, napenda Waheshimiwa Wabunge, watuamini Serikali tunachukua hatua kweli ya kufika mahali mifuko hii isiyooza na isiyorejerezeka ipigwe marufuku. Suala la mazao ambayo yamebadilishwa viini tete kwa kichwa wanakiita kwa kiingereza *genetically modified organisms.* Ambayo inahusiana na mkataba wa bioanuwai na Itifaki ya katagina. Kuna mambo mawili kuna *biotechnology,* teknologia ya kibiologia na kuna *biosensitive* usalama wa kiteknologia unapozungumzia mazao yanayotokana na utaalam na maendeleo haya ya kisayansi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sisi katika Ofisi ya Makamu wa Rais, tunachoshughulika nacho ni suala la usalama wa matumizi ya mazao ambayo yamebadilishwa kijenetiki kwa kiteknologia ya kisasa *biosensitive* na namshukuru Mheshimiwa Job Ndugai, kwa kusema kuna msingi wa kimataifa katika *agenda 21* na inasema hivi hata kama huna ushahidi wa kisayansi lakini unahisi yanaweza yakawako madhara kwa matumizi kitu fulani, usichelewe kuchukua hatua za tahadhari. Ndio *precaution at all principles.*

Mheshimiwa Spika, sasa katika mikutano ya kimataifa ambayo kama alivyosema Mheshimiwa Abdulkarim Shah, nahudhuria ya nchi yangu. Kwa lugha inayoeleweka wanaofagilia suala la biashara na faida wanasema kuleni vyakula vilivyobadilishwa viini tete kwa *genetically modify organisms.* Lakini wako wengine wanasema hivi twende taratibu tuharikishe polepole *fenista lente hence in slowly.* Wanasema mazao haya kama utapanda mbegu za pamba ambazo ni matokeo ya *GMO* karibu na shamba ambalo umepanda mbegu za asili. Iwapo maua au *pollen* chavua kwa kiswahili ya pamba iliyobadilishwa kijenetiki ikichavusha kama itawezekana maua ambayo ni ya mimea ya asili. Mbegu zinatakazo tokana na mimea ile ya siri ukitaka kupanda hazitoota.

Mheshimiwa Spika, Sasa sisi kama alivyouliza Mheshimiwa Job Ndugai kikubwa na tatizo kama la Zambia walikuwa na njaa wakaambiwa chukueni chakula mahindi ambayo ni *GMO.* Anasema hivi tukipatwa na janga hili Tanzania tutachukua au hapana, tunasema kwanza Mungu aepushie mbali. Lakini ya pili tunachotaka tujihakikishie kwamba tusipate mbegu zitakazoua mbegu za asili katika nchi yetu. Kwa sababu kama tutakuwa watumwa wa kununua mbegu kutoka makampuni makubwa duniani utakapofika msimu wa kilimo hapa kwetu na unalazimika kuagiza mbegu kutoka kwa wakubwa umepata matatizo ya ukame unataka uagize chakula kwa ajili ya watu wasife njaa na papo hapo umefungwa unatakiwa uagize mbegu kutoka huko nje utafanyaje. Kwa hiyo, ndiyo matatizo yanayotumika kwa mbali. Hivyo tuchukue tahadhari hiyo mambo kama hayo anavyosema Mheshimiwa Waziri wa Katiba na Sheria, tusiyaendee kichwa kichwa.

Tutakuwa watumwa wa makampuni makubwa na hakuna anayejua madhara ya mambo haya kwa afya ya binadamu kwa siku zijazo. Ushahidi haupo tena siyo wazi, lakini ni vizuri kuchukua tahadhari na tuna msemo wa kiswahili tahadhari kabla ya hatari.

Sasa nizungumzie suala la viwango. Nadhani kuna Mheshimiwa Mbunge alisema kwa nini hili suala la viwango kwa sababu sasa *NEMC* imewapa meno na siku moja nilisema tena ni nimsumeno wa umeme na kwa maana hiyo meno yake yanakata kweli kweli. Anasema kwa nini sasa msiwape *NEMC* ndio wakawa na mamlaka kisheria ya kutamka viwango ili waweze kusimamia ipasavyo.

Mheshimiwa Spika, kwanza hili lina matatizo yake ukiweka viwango wewe mwenyewe halafu ukienda kusimamia nadhani unaweza kupata tatizo la *conflict of interest* unaweza na tusingependa hili litokee. Lakini vile vile tulifanya hivyo kwa makusudi.

Mheshimiwa Spika, lakini vile vile tulifanya hivyo kwa sababu kufanya kosa wanasema si kosa, kosa ni kurudia kosa tena ni kosa kubwa zaidi. Lakini sisi tumekuta kuna majirani zetu walifanya kosa wakafanya hivyo.

Sasa walipofanya hivyo kwa sababu suala la viwango ni la kimataifa maana hatuwezi tukasema Shirika letu liko pale Ubungo, Shirika la Viwango kwa hiyo namna yake ni viwango vya Kitanzania, Tanzania hapana tunaishi katika dunia ya utandawazi. Lazima viwango vyetu viwe ni vya kimataifa au vinakubalika kimataifa na kutambulika hivyo. Sasa wenzetu Uganda walipotunga sheria kama hiyo walitekeleza kama wazo la Mheshimiwa Mbunge lilivyotoka. Wakaipa *NEMA,* wanaita *NEMA* Uganda ina mamlaka ya kutamka viwango.

Sasa Shirika la Viwango duniani linasema sisi hatutambui kitu *NEMA, NEMA* sawa na *NEMC* ya hapa kwetu eeh sasa kama haitambuliki, Shirika la Viwango Duniani unafanyaje;

Mheshimiwa Spika, ndio wakaanza majadiliano ya kuwekeana mkataba *memorandum of understanding* na hii ni nembo ya nchi jirani ya Uganda ya kuwekeana mkataba kwamba hili Shirika la Viwango washirikiane sasa kwa maelewano haya na shirika kama *NEMC* ya hapa kwetu nyumbani.

Mheshimiwa Spika, Sasa kama nilivyosema tunamshukuru Mungu nchi yetu tunao wataalam wengi katika Ofisi za Makamu wa Rais, vyuo vikuu vyetu. Tulipofanya utafiti tukasema tusifanye kosa kama walilofanya wenzetu. Ndio sababu hatukuweka *NEMC* isimamie viwango ili isiwe ndio mahali ukaipa mamlaka ya kutamka viwango. Wao watekeleze na wasimamie mazingira kwa viwango vinavyotambulika kimataifa na tutafute ujuzi kwenye Shirika letu Viwango linalotambuliwa kimataifa hilo ndilo tulilolifanya na kwa kweli ninahakika Wabunge watakubaliana nami tumelenga barabara.

Mheshimiwa Spika, ndio hili nilitaka niliseme hivi. Sasa kuhusu suala la uchafuzi wa hewa ni kweli uchafuzi wa hewa na kelele ni moja ya vitu ambavyo katika Muswada wa sheria hii limezingatiwa na ningependa nijibu moja nadhani kuna Mheshimiwa Mbunge alisema haya magari yanayotumia *petrol* yenye risasi tunafanyaje.

Mheshimiwa Spika, uko uamuzi uliotokana na Mawaziri wa Bara la Afrika wanaoshughulikia Mazingira na baadaye wamekuja kupitishwa rasmi na Shirika la Umoja wa Mataifa linalosimamia Mazingira. Ambalo kwa unyenyekevu mkubwa mimi ni Rais wa Shirika hilo hivi sasa. *(Makofi)*

Lakini ni kwa niaba ya nchi yangu na kama nilivyosema chochote kama sifa iwe kwa nchi yangu, chama changu na kwa Mwenyezi Mungu. Tumeshakubaliana ifikapo tarehe 31 Decemba, 2005 matumizi ya *petrol* yenye risasi ni marufuku katika nchi yetu. *(Makofi)*

Niliwahi kupata fursa ya kueleza madhara ya moshi unaotokana na magari yanayotumia *petrol* yenye risasi madhara yake. Watoto wadogo ubongo haukuwi sawasawa ndio inakuwa kama vile unamtindio wa ubongo. Kuna vifo vya ghafla tu unashtukia watu wamekufa hujui kaugua sana sana huko vijinini utasema kalogwa. Kuna tatizo la mimba kutoka ovyo *miscarriages* kutokana na moshi unaotokana na magari yanayotumia *petrol* yenye risasi na *cancer* mbalimbali.

Mheshimiwa Spika, sasa kwa nini mambo kama haya wakati kuna *petrol* mbadala kwa nini tuyazingatie hayo.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, haya yalikuwa ni baadhi ya maeneo makuu ambayo niliona niyazungumzie kwa sababu siwezi nikasema nitazungumzia kila mchango wa kila mmoja wa Waheshimiwa Wabunge waliochangia kwa maandishi au kwa kusema katika hoja hii. *(Makofi)*

Lakini nakumbuka Mheshimiwa mmoja amechangia Mheshimiwa Aaron Chiduo kwa maandishi. Anasema hivi; ukisoma katika maandiko matakatifu na hakika ni kuruani tukufu na biblia sijui na mengineyo anasema mwenyezi Mungu alipoumba dunia aliona yote ni mazuri na kusema kweli meneja mkuu wa mazingira ni mwenyezi Mungu.

Sisi tunatakiwa kuratibu shughuli tunazozifanya katika dunia yetu. Lakini sijui kama alivyosema Mheshimiwa Prof. Jumanne Maghembe, sijui shauri ya umasikini tunafanya mambo ambayo vizazi vijavyo, kama hatukupiga breki na tukafanya marekebisho watakuja kutuuliza, watajiuliza hawa mababu wa mababu zetu walikuwa watu wa namna gani.

Mheshimiwa Spika, maana tujiulize huu uharibifu wa mazingira unaotishia nchi yetu kuwa jangwa na ni kweli mito inakauka, mabwawa yanakauka Waheshimiwa Wabunge wa Kamati ya Maliasili na Mazingira ni mashahidi tumekuta Ziwa Victoria kule Kayeze ambako kuna sehemu ilikuwa imemezwa na maji.

Sasa hivi iko juu tu kwa sababu kina cha maji katika Ziwa Victoria kimepungua. Tunaosafiri hivi tunaona mito inavyokauka. Sasa ni lazima tujiuleze hivi mababu wa mababu zetu wangeishi namna hiyo tungekuwa wapi leo sisi, tusingekuwepo.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, nilitaka niseme hili na mwisho nilitaka niseme tu kwamba wale mtakao soma nadhani gazeti la Rai la leo linasema sasa tusiseme tu kwamba wanamwambia Mheshimiwa Rais wetu kwamba sisemi tu lakini zitolewe adhabu kwa wanaoharibu na kuchafua mazingira. Sheria inasema adhabu itatumika lakini la msingi tutoe elimu kusudi tuelewe madhara ya kugeuza nchi yetu kuwa jangwa na kushindwa kuendelea kuishi.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo machache naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**WAZIRI WA FEDHA:** Mheshimiwa Spika, naafiki.

*(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

*(Muswada wa Sheria ya Serikali ulisomwa mara ya pili)*

**KAMATI YA BUNGE ZIMA**

*Hapa Mwenyekiti (Mhe. Anne S. Makinda) Alikalia Kiti.*

**Muswada wa Sheria ya Usimamizi wa Mazingira wa Mwaka, 2004**
***(The Environmental Management Bill, 2004)***

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge kama mnavyofahamu Muswada huu ni kitabu chote hiki, kina *section* zaidi ya 233. Kwa hiyo, tukisema kifungu kwa kifungu basi tutamaliza saa kumi jioni. Kwa hiyo, tutafanya kwa *section* na ziko *section 20.*

Kifungu cha 1
Kifungu cha 2

*(Vifungu viliyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Bunge zima bila mabadiliko yoyote)*

Kifungu cha 3

**MHE. BEATUS R. MAGAYANE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mchango wangu nilipendekeza sheria itumike Tanzania kote Bara na Visiwani. Msimamo wa Serikali ni nini kuhusu hili.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS (MHE. ARCADO D. NTAGAZWA):** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli na tunamshukuru sana kwa mchango wake lakini sheria ya Mazingira pamoja na kuwa suala la Mazingira ni mtambuka.

Wenzetu Serikali ya Mapinduzi Zanzibar wanasheria yao ya Mazingira na ni kweli suala hili si la Muungano, ila kama ulivyotolewa mchango hapa Bungeni wakati wa kuandaa kanuni ambazo ndizo zinawezesha utekelezaji mzuri wa sheria yenyewe tumeshauriwa tumekubali kwamba Wawakilishi wa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar watashirikishwa kikamilifu.

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Kifungu cha 4
Kifungu cha 5
Kifungu cha 6
Kifungu cha 7
Kifungu cha 8
Kifungu cha 9
Kifungu cha 10
Kifungu cha 11
Kifungu cha 12
Kifungu cha 13

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Bunge zima bila mabadiliko yoyote)*

Kifungu cha 14

**MHE. JOB YUSTINO NDUGAI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kunipa fursa hii na kwa heshima kubwa nilishirikishwa vizuri ndani ya Kamati kupitia mambo yote lakini nataka ufafanuzi kidogo toka kwa Mheshimiwa Waziri kuhusiana na fungu la 14 suala linalohusu Mkurugenzi wa Mazingira, Ofisi ambayo ni muhimu sana. Nimechangia kwa kuchangia hapa na kwa maandishi, kuhusu pendekezo ambalo tumelitoa la jina la Mkurugenzi wa Mazingira kuwa Kamishna, sijui haku- *comment* chochote wakati wa kumalizia.

Lakini pili kwenye fungu hilo Mheshimiwa Mwenyekiti, hapajatajwa mamlaka ya uteuzi wa huyu *director.* Lakini pia sifa hazijatajwa na nilishaandika hata kwenye maandishi, lakini wakati anamalizia hakuwa amesema chochote. Naomba maelezo.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS (MHE. ARCADO D. NTAGAZWA):** Mheshimiwa Mwenyekiti nakushukuru na ninamshukuru Mheshimiwa Job Ndugai. Haikutajwa kwamba Mamlaka ya Uteuzi wala sifa kwa Mkurugenzi wa Mazingira kwa sababu imechukuliwa na inaeleweka kwamba, huyu ni mtumishi katika *Public Service,* katika Utumishi wa Umma, katika mtindo na mfumo wa Utumishi wa Umma. Kwa hiyo, kama Waheshimiwa Wabunge watakumbuka kuna kipindi tulikuwa tunasema tumpunguzie Mheshimiwa Rais wale watu anaowateua pale ambapo kuna

mfumo na utaratibu wa kuwapata watendaji wakuu katika Idara zetu za Serikali. Hili la kwanza. La pili kwamba badala ya kuitwa Mkurugenzi aitwe *Commissioner.*

Tumebakia na Mkurugenzi kwa sababu karibu nchi zote ambazo ni majirani katika Jumuiya yetu hatuna *Commissioner* wa Mazingira na wale Wakurugenzi kama tunavyopendekeza katika kifungu cha 14 wanafanya kazi zao, maana sisi tumetazama maudhui na kile wanachokifanya kuliko namna wanavyoitwa na kujulikana.

**MHE. JOB Y. NDUGAI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa naiomba Serikali angalau basi itaje tu kwamba Mamlaka ya Uteuzi ya cheo hiki ni Mheshimiwa Rais. Maana kifungu kimenyamaza kabisa hata hakitaji nani atashughulikia uteuzi wa mtu huyu muhimu sana kwa Sheria nzima hii.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS (MHE. ARCADO D. NTAGAZWA):** Mheshimiwa Mwenyekiti nimemwelewa sana Mheshimiwa Job Ndugai, kwamba ingekuwa ni vizuri tukatamka. Lakini tukumbuke kwamba suala la Mazingira ni mtambuka, na hata wataalam walioko katika Ofisi ya Mheshimiwa Makamu wa Rais, utakuta wametoka Idara ya Misitu, wametoka Kilimo, wametoka Mifugo, wametoka Maji na kwingineko. Sasa hawa wote ni Watumishi wa Serikali. Kwa maana ya *Civil Service* na *Civil Service Regulations* wana ule utaratibu wa *TANGE Seniority.* Kwa hiyo, anapokuwa amefikia mahali mtumishi wa Serikali ambaye yuko katika Utumishi wa Umma *Under Civil Service Regulations.* Wanapanda vyeo na hadhi zao kama kuna nafasi ya kuitwa *Commissioner* atakuwepo. Lakini kwetu sisi tunaona Mkurugenzi ndio tulivyoeleweka kama inavyosomeka katika mapendekezo ya Sheria.

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Kifungu cha 15
Kifungu cha 16
Kifungu cha 17
Kifungu cha 18

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Kifungu cha 19
Kifungu cha 20

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na mabadiliko yake)*

Kifungu cha 21
Kifungu cha 22
Kifungu cha 23
Kifungu cha 24

Kifungu cha 25
Kifungu cha 26
Kifungu cha 27
Kifungu cha 28
Kifungu cha 29
Kifungu cha 30
Kifungu cha 31
Kifungu cha 32
Kifungu cha 33
Kifungu cha 34
Kifungu cha 35
Kifungu cha 36
Kifungu cha 37
Kifungu cha 38
Kifungu cha 39
Kifungu cha 40
Kifungu cha 41

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Kifungu cha 42
Kifungu cha 43
Kifungu cha 44
Kifungu cha 45

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Kifungu cha 46

**MHE. JENISTA J. MHAGAMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati nilipokuwa nachangia Muswada, nilikuwa nimeomba na kushauri katika Kifungu namba 56. Ni kwa nini ile *declaration of the protected wet land.* Kwa nini *Minister* afanye *consultation* na Minister *responsible for the land, na local authority* isiongezwe pale kwa sababu wale ndio wamiliki wakubwa wa Ardhi?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mbunge nitakupa nafasi tukifikia hapo.

*(Kifungu kilivyotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Kifungu cha 47

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Kifungu cha 48

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na mabadiliko yake)*

Kifungu cha 49
Kifungu cha 50
Kifungu cha 51

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Kifungu cha 52

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na mabadiliko yake)*

Kifungu cha 53
Kifungu cha 54
Kifungu cha 55

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Kifungu cha 56

**MHE. JENISTA J. MHAGAMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru nili-*overlook.* Kwa hiyo, kipengele namba 56 kiko katika Ibara ya 5. Kwa hiyo, maelezo yangu ni kama nilivyoyatoa pale awali. Nilikuwa naomba *local authority* iongezwe pale ili *Minister* anapofanya *consultation,* asifanye tu na Waziri mwenye dhamana ya ardhi ahusishwe pia na mtu mwenye dhamana ya ardhi kule kwenye Serikali za Mitaa. *(Makofi)*

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS (MHE. ARCADO D. NTAGAZWA):** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa hoja ya Mheshimiwa Mbunge Jenista J. Mhagama. Lakini maelezo yetu kutoka Ofisi ya Makamu wa Rais ni kuwa hapa ni ardhi *wave* ambayo haiko katika mamlaka kwa mfano Hifadhi za Taifa ambazo ziko chini ya Mamlaka ya sheria nyingine na kwa sababu ardhi hii inaweza ikaonekana Mheshimiwa Mwenyekiti na Waheshimiwa Wabunge, kwamba inahitaji kutamkwa au kutangazwa kwamba inahitaji kuhifadhiwa kwa sababu mazingira yake yalivyo.

Tukasema tufanye mashauriano kushauriana na Waziri wa Ardhi maana yeye ndio kwa niaba ya Mkuu wa Nchi ndiyo masuala ya ardhi yako mikononi mwake. Suala kwamba kwa nini tusimshirikishe Mheshimiwa Waziri TAMISEMI si kwamba

hatumshirikishi. Kinachofanyika tunatamka tu alafu uendeshaji unabakia kwa mamlaka zinazohusika. Kwa mfano, kama ni ardhi iko kijijini itakuwa ni Serikali ya Kijiji, kama katika Serikali za kijiji tunajua ni katika mamlaka ya Halmashauri ya Wilaya, Halmashauri ya Mji au Halmashauri ya Manispaa ni hiyo tu si kwamba tulitaka tumweke pembeni. Tulijua anahusika Waziri wa TAMISEMI katika maana nyingine ya Mamlaka za Miji, Vijiji, Manispaa na Jiji. Maelezo yetu ni hayo tu, si kwamba hatukumshirikisha lakini anahusika moja kwa moja katika management ya maeneo haya yakishatamkwa.

**MHE. JENISTA J. MHAGAMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, tumepitisha Sheria kadhaa zinazohusu ardhi. Miongoni mwa Sheria hizo, ziko Sheria ambazo zinatamka kabisa kwamba ardhi ni mali ya Rais kweli, lakini vijiji na maeneo husika yanamiliki ardhi zao kama ni mali ya Umma au ni mali ya vijiji kwa matumizi yoyote. Matumizi ya ardhi ile hayawezi kubatilishwa ama kutamkwa kwa matumizi mengine mbadala bila kufanya *consultation* na *local authority* kwa maana ya Serikali za vijiji *whatever* ama Serikali za mitaa. Sasa kwa kesi hii, mimi inaniwia vigumu kuona kwamba maamuzi haya yafanyike na Waziri mwenye dhamana ya ardhi tu, na wale wamiliki wa ardhi wenyewe wasipate hizo taarifa na kushirikishwa katika maamuzi hayo na inawezekana kabisa labda maeneo hayo yakawa kwenye mipango ya matumizi ya Wananchi katika maeneo husika. Sasa kama hawatashirikishwa na maamuzi hayo yatafanyika ngazi za juu tu, hao wana haki gani ya kutumia maeneo yao? Kwa nini wasishikishwe ili waweze kusaidia katika kutoa maamuzi?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS (MHE. ARCADO D. NTAGAZWA):** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante unajua kama ulivyosema Sheria hii ni buku hasa na unaweza usipate kifungu kinachojielekeza kwa mfano kumtoa hofu Mheshimiwa Jenista J. Mhagama. Lakini Mheshimiwa Mwenyekiti na Waheshimiwa Wabunge ukisoma kifungu kidogo cha 5 cha kifungu hicho hicho ambacho kinasema: *"The Minister in Consultation with other sector Ministries may make regulations and guide lines on the sustainable management of work land protected under this act."*

Kwa hiyo, wasiwasi wa Mheshimiwa Mbunge kifungu hiki cha 5 kimetoa mashaka kabisa aliyokuwa nayo. *(Makofi)*

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho yaliyofanywa)*

Kifungu cha 57
Kifungu cha 58
Kifungu cha 59
Kifungu cha 60
Kifungu cha 61
Kifungu cha 62
Kifungu cha 63
Kifungu cha 64
Kifungu cha 65

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Kifungu cha 66

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na mabadiliko yake)*

Kifungu cha 67
Kifungu cha 68
Kifungu cha 69
Kifungu cha 70
Kifungu cha 71
Kifungu cha 72
Kifungu cha 73
Kifungu cha 74
Kifungu cha 75
Kifungu cha 76

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Kifungu cha 77
Kifungu cha 78
Kifungu cha 79

*(Vifungu vilichotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na mabadiliko yake)*

Kifungu cha 80
Kifungu cha 81
Kifungu cha 82
Kifungu cha 83
Kifungu cha 84
Kifungu cha 85
Kifungu cha 86
Kifungu cha 87
Kifungu cha 88
Kifungu cha 89
Kifungu cha 90
Kifungu cha 91
Kifungu cha 92
Kifungu cha 93
Kifungu cha 94
Kifungu cha 95
Kifungu cha 96

Kifungu cha 97
Kifungu cha 98
Kifungu cha 99
Kifungu cha 100
Kifungu cha 101

*(Vifungu vulivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Kifungu cha 102

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na mabadiliko yake)*

Kifungu cha 103

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Kifungu cha 104
Kifungu cha 105

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na mabadiliko)*

Kifungu cha 106
Kifungu cha 107
Kifungu cha 108
Kifungu cha 109
Kifungu cha 110
Kifungu cha 111
Kifungu cha 112
Kifungu cha 113
Kifungu cha 114
Kifungu cha 115
Kifungu cha 116
Kifungu cha 117
Kifungu cha 118
Kifungu cha 119
Kifungu cha 120
Kifungu cha 121
Kifungu cha 122
Kifungu cha 123
Kifungu cha 124
Kifungu cha 125
Kifungu cha 126

Kifungu cha 127
Kifungu cha 128
Kifungu cha 129
Kifungu cha 130
Kifungu cha 131
Kifungu cha 132
Kifungu cha 133
Kifungu cha 134
Kifungu cha 135
Kifungu cha 136
Kifungu cha 137
Kifungu cha 138

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote.)*

Kifungu cha 139
Kifungu cha 140

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na mabadiliko yake)*

Kifungu cha 142
Kifungu cha 143
Kifungu cha 144
Kifungu cha 145
Kifungu cha 146
Kifungu cha 147
Kifungu cha 148
Kifungu cha 149
Kifungu cha 150
Kifungu cha 151
Kifungu cha 152
Kifungu cha 153
Kifungu cha 154
Kifungu cha 155
Kifungu cha 156
Kifungu cha 157
Kifungu cha 158
Kifungu cha 159
Kifungu cha 160
Kifungu cha 161
Kifungu cha 162
Kifungu cha 163

Kifungu cha 164
Kifungu cha 165
Kifungu cha 166
Kifungu cha 167
Kifungu cha 168
Kifungu cha 169
Kifungu cha 170
Kifungu cha 171
Kifungu cha 172
Kifungu cha 173
Kifungu cha 174
Kifungu cha 175
Kifungu cha 176
Kifungu cha 177
Kifungu cha 178
Kifungu cha 179
Kifungu cha 180
Kifungu cha 181

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Kifungu cha 182

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na mabadiliko yake)*

Kifungu cha 183
Kifungu cha 184
Kifungu cha 185
Kifungu cha 186
Kifungu cha 187
Kifungu cha 188
Kifungu cha 189
Kifungu cha 190
Kifungu cha 191
Kifungu cha 192
Kifungu cha 193
Kifungu cha 194
Kifungu cha 195
Kifungu cha 196
Kifungu cha 197
Kifungu cha 198
Kifungu cha 199

Kifungu cha 200
Kifungu cha 201
Kifungu cha 202
Kifungu cha 203
Kifungu cha 204
Kifungu cha 205
Kifungu cha 206
Kifungu cha 207
Kifungu cha 208
Kifungu cha 209
Kifungu cha 210
Kifungu cha 211
Kifungu cha 212
Kifungu cha 213
Kifungu cha 214
Kifungu cha 215
Kifungu cha 216

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Kifungu cha 217

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na mabadiliko yake)*

Kifungu cha 218
Kifungu cha 219
Kifungu cha 220
Kifungu cha 221
Kifungu cha 222
Kifungu cha 223
Kifungu cha 224
Kifungu cha 225
Kifungu cha 226

*(Vifungu hivi viliafikiwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Kifungu cha 227

*(Kifungu hiki kiliafikiwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na mabadiliko yake)*

Kifungu cha 228

*(Kifungu Kilichotajwa hapo juu Kilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Kifungu cha 229
Kifungu cha 230

*(Vifungu hivi viliafikiwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na mabadiliko yake)*

Kifungu cha 231
Kifungu cha 232
Kifungu cha 233

*(Vifungu hivi viliafikiwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Jedwali la Kwanza

*(Jedwali hili liliafikiwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na mabadiliko yake)*

Jedwali la Pili

*(Jedwali hili liliafikiwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote.)*

Jedwali la Tatu

*(Jedwali hili liliafikiwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na mabadiliko yake)*

Jedwali la Nne

*(Jedwali hili liliafikiwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

*(Bunge lilirudia)*

**Muswada wa Sheria ya Usimamizi wa Mazingira wa Mwaka 2004**
***(The Environmental Management Bill 2004)***

*(Kusomwa Mara ya Tatu)*

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS (MHE. ARCADO D. NTAGAZWA):** Mheshimiwa Mwenyekiti, Bunge zima limefikiria Muswada wa Hifadhi na usimamizi wa Mazingira yaani *Environmental Management Act Bill,* pamoja na marekebisho yaliyofanywa. Hivyo naomba kwamba Muswada huo kama ulivyorekebishwa katika Kamati ya Bunge zima sasa ukubaliwe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**WAZIRI WA FEDHA:** Mheshimiwa Spika, naafiki.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*

*(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*
*(Muswada wa Sheria ya Serikali ulisomwa mara ya Tatu na Kuafikiwa)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, sasa Muswada huu uko tayari sasa kupewa saini ya Mheshimiwa Rais ili uweze kutumika ipasavyo.

Waheshimiwa Wabunge, sasa tumebakia na dakika 15 kufikia saa ya kuahirisha Kikao hiki cha Bunge kwa mchanga huu. Muda uliobaki hautoshi kwa ajili ya kuanzisha Muswada mwingine ambao ni *The Public Procurement Act.* Kufuatana na alivyoeleza Mheshimiwa Spika, asubuhi ni kwamba tuta-*manage time* ili kusudi kesho saa saba mchana tumalize Kikao cha Bunge.

Waheshimiwa Wabunge, tunao wachangiaji wanne katika Muswada huo. Wachangiaji atakuwa Mheshimiwa Dr. Miltoni M. Mahanga, Mheshimiwa Dr. William F. Shija, Mheshimiwa Aggrey D.J. Mwanri, na Mheshimiwa Philip S. Marmo, ndio mwisho wa wale watakaochangia. Kwa hiyo, Waheshimiwa Wabunge kwa sasa naahirisha Kikao hiki cha Bunge hadi saa 10.00 jioni. *(Makofi)*

*(Saa 06.45 mchana Bunge lilifungwa mpaka Saa 10.00 jioni)*

*(Saa 10.00 jioni Bunge lilirudia)*

*Hapa Mwenyekiti (Mhe. Anne S. Makinda) Alikalia Kiti*

**Muswada wa Sheria ya Manunuzi Katika Sekta ya Umma Mwaka 2004**
***(The Public Procurement Bill, 2004)***

*(Kusomwa Mara ya Pili)*

**WAZIRI WA FEDHA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa hoja kwamba Muswada wa Sheria ya Ununuzi ya Mwaka 2004 yaani *The Public Procurement Bill, 2004* pamoja na Marekebisho yake sasa usomwe kwa mara ya pili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote naomba kutoa shukrani zangu za dhati kwa Kamati ya Bunge ya Fedha na Uchumi chini ya uenyekiti wa Mheshimiwa Njelu Kasaka, Mbunge wa Lupa, kwa kuujadili kwa kina Muswada huu na kutoa ushauri.

Vile vile napenda kuchukua fursa hii kuwashukuru Waheshimiwa Kilontsi Mporogomyi, Mbunge wa Kasulu Magharibu na Mheshimiwa Lephy Gembe, Mbunge wa Mpanda Kati, kwa kumsaidia Mwenyekiti Njelu Kasaka vizuri sana alipokuwa na shughuli nyingine muhimu.Napenda kulihakikishia Bunge lako Tukufu kwamba Muswada huu umezingatia mapendekezo ya Kamati na Wadau wake wote.

Aidha nachukua nafasi hii kumpongeza Mwenyekiti Mheshimiwa Njelu Kasaka kwa kushinda wiki iliyopita shauri la malalamiko ya uchaguzi dhidi yake katika Mahakama Kuu ya Tanzania Kanda ya Mbeya.*(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kutungwa Sheria ya sasa ya ununuzi yaani *The Public Procurement Act 2001,* Serikali imekuwa ikifuatilia kwa karibu utekelezaji wake kwa njia ya tafiti kupitia kwa wadau mbalimbali. Tafiti hizi kwa kiwango kikubwa zimebaini mapungufu kadhaa katika Sheria hii ambayo yanahitaji marekebisho ili kudhibiti na kuongeza tija katika ununuzi wa umma.

Aidha kwa kuwa marekebisho yanayohitajika ni mengi, Serikali imeamua kwamba Sheria hii iandikwe upya ili marekebisho hayo yaweze kutiririka na kueleweka kwa urahisi na bila kuathiri misingi na maudhui yaliyokuwepo kwenye sheria hiyo. Ningependa kusisitiza kwa hiyo kwamba *Public Procurement Act 2004* siyo Muswada mpya bali ni maboresho ya Sheria ya mwaka 2001 baada ya kutafakari malalamiko yaliyojitokeza katika utekelezaji wake.

Mheshimiwa Spika, Maudhui ya Muswada, napenda sasa nieleze kwa muhtasari Maudhui ya Muswada uliopo mbele yenu ambayo ni:-

(a) Kutunga sheria inayokidhi matakwa ya Sheria bora zaidi kutumika ndani ya nchi na ngazi ya kimataifa yaani *best practices* katika kusimamia shughuli za ununuzi Serikali, kwanza kwa kuanzisha chombo cha juu cha kijumla kitakachosimamia Sheria ya ununuzi, pili kupeleka madaraka ya ununuzi yaani *Decentralization* kwenye Wizara, Idara za Serikali na Mashirika ya Umma na tatu kuzihusisha Serikali za Mitaa katika masharti ya msingi ya Sheria ya ununuzi.

(b) kuanzisha Mamlaka Kuu ya kusuluhisha migogoro itokanayo na shughuli za zabuni itakayojumuisha pia wawakilishi toka sekta binafsi.

(c ) Kuweka mfumo thabiti wa uwajibikaji kwa Wizara, Idara za Serikali na Mashirika ya Umma.

(d) Kuanzisha vitengo vya ununuzi yaani *Procurement Management Units* katika ngazi za Wizara, Idara za Serikali na Mashirika ya Umma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Muswada ulioko mbele yenu umegawanyika katika sehemu kuu nane.

Sehemu ya kwanza inahusu mambo ya utangulizi kama vile jina la Muswada, tarehe ya kuanza kutumika kwa Muswada na matumizi ya Muswada. Sehemu ya pili inazungumzia kuanzishwa kwa Mamlaka ya Usimamizi wa Ununuzi katika Sekta ya umma kazi zake na uteuzi wa Wakurugenzi wa Bodi ya Mamlaka. Sehemu ya tatu inahusu kuundwa kwa Bodi za Zabuni za Wizara, Idara za Serikali Mashirika ya Umma na kadhalika.

Sehemu ya nne na ya tano zinazungumzia misingi, taratibu na njia mbalimbali za ununuzi zinazohakikisha ushindani na uwazi. Sehemu ya sita inahusu vitendo visivyo ruhusiwa katika masuala ya ununuzi wa umma ikiwa ni pamoja na suala la rushwa. Sehemu ya saba inazungumzia jinsi ya kusuluhisha migogoro itokanayo na masuala ya ununuzi. Sehemu ya nane na ya mwisho inazungumzia masuala ya kijumla yakiwemo makosa mbalimbali chini ya Muswada huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maeneo yanayokusudiwa kufanyiwa marekebisho, naomba sasa nieleze kwa kifupi maeneo makuu yanayofanyiwa marekebisho kwa mujibu wa Muswada wa Sheria ya ununuzi ya Mwaka 2004.

Kwanza matumizi ya Sheria, Kifungu Namba 2 cha Muswada kinafanyia marekebisho kifungu namba 2 cha Sheria ya sasa ili Sheria hii iweze kutumika Tanzania Bara na Tanzania Zanzibar katika masuala yanayohusu Muungano.

Aidha kifungu hiki kinapanua wigo wa matumizi ya Muswada kwa Mashirika ya Umma na Asasi zote zinazopata ruzuku kutoka Serikalini zikiwemo Jeshi la Wananchi wa Tanzania, Jeshi la Polisi, Magereza, Jeshi la Kujenga Taifa, Taasisi ya Kuzuia Rushwa na Idara ya Usalama wa Taifa. Sheria ya sasa kupitia kifungu cha pili haitumiki katika manunuzi ya Taasisi hizi.

Pili kuanzisha Mamlaka moja ya usimamizi wa shughuli zote za ununuzi kwenye sekta ya umma, kwa mujibu wa Sheria ya sasa Halmashauri Kuu ya Zabuni imepewa majukumu ya kusimamia Sheria pamoja na shughuli za kiutendaji zikiwemo kuitisha, kupokea, kufungua , na kuidhinisha zabuni pamoja na kusuluhisha migogoro itokanayo na masuala ya zabuni.

Hali hii imesababisha Halmashauri Kuu ya Zabuni kuidhinisha zabuni na wakati huohuo kupitisha na kuhuisha maamuzi yake yenyewe, jambo ambalo ni kinyume na misingi ya uwajibikaji na utawala bora.

Ili kuondoa mapungufu haya vifungu namba 5 hadi 10 vya Sheria ya sasa vinafutwa na badala yake kuingiza vifungu vipya kuanzia namba 5 hadi 27 vinavyoainisha uanzishaji wa Mamlaka ya usimamizi na taratibu za kiutendaji.

Aidha jedwali la kwanza la Sheria ya sasa ambalo limeainisha muundo, uteuzi na taratibu za Halmashauri Kuu ya Zabuni yaani *Central Tender Board* linafutwa na kuwekwa jedwali jipya linaloainisha muundo, uteuzi na taratibu za Mamlaka ya udhibiti wa Ununuzi wa Umma.

Tatu Muswada huu unapendekeza pia kufuta vifungu vya 57 na 58 vya Sheria ya sasa ili kuondoa ukomo wa viwango *(Threshold)* vya kufanya ununuzi badala yake Muswada unatoa madaraka kamili yaani *Full Decentralization* kwa Wizara, Idara za Serikali na Mashirika ya Umma kujifanyia ununuzi kutokana na bajeti zao.

Aidha ili kuiwezesha Mamlaka kufuatilia kwa karibu zabuni kubwa, kifungu cha 31 cha Muswada kinaweka utaratibu wa mwenye *tender* kutoa taarifa kwa Mamlaka ndani ya siku 14 kuhusu kuanza kwa taratibu za zabuni.

Nne katika kuhakikisha uwajibikaji wa Wizara, Idara za Serikali na Mashirika ya Umma Muswada kupitia kifungu cha 28 na Jedwali la pili unafuta vifungu Namba 11 hadi 16 na Jedwali Namba 2 hadi 4 ya Sheria ya sasa yanayowaondoa Maafisa Wahasibu yaani *Accounting Officers* katika nafasi za Uenyekiti wa Bodi za Zabuni na badala yake nafasi hizo zinakuwa kwa maafisa watakaoteuliwa katika ngazi ya Wakuu wa Idara.

Hata hivyo kwa mujibu wa kifungu cha 28 kifungu kidogo cha 3, muundo wa Bodi wa Halmashauri za Serikali za Mitaa utaendelea kuwa kama ulivyoainishwa katika kanuni za Sheria ya Fedha ya Serikali za Mitaa ya Mwaka 1982, *Local Government Finance Act, 1982.*

Wakati taratibu zinafanyika kuwaelimisha watendaji na kujenga uwezo zaidi katika ngazi ya Halmashauri kuhusu utaratibu na kanuni za ununuzi kama zilivyoainishwa katika Muswada huu, hatua hii ni kuzingatia ukweli kuwa Halmashauri nyingi zinahitaji kujizatiti zaidi kabla ya kujiingiza moja kwa moja kwenye utaratibu mmoja wa kitaifa.

Tano, unarekebisha kifungu cha 4 cha Sheria ya sasa ili kutoa upendeleo maalumu kwa Makampuni ya Kitanzania pale ununuzi unapofanyika nje ya nchi kwa fedha ambazo Serikali imechangia, hii ni hatua ya uwezeshaji ambayo imeainishwa chini ya vifungu vya 22 na 23 vya Sheria ya sasa ambavyo vinaendelea kuwepo na pia ni njia mojawapo ya kuwafanya wananchi wafaidike zaidi na fedha zinazotengwa katika Bajeti za Serikali zao. *(Makofi)*

Sita, Kifungu cha 77 na Jedwali la 3 la Muswada vinapendekeza kufutwa kwa kifungu namba 66 na Jedwali Namba 6 la Sheria ya sasa ili kuondoa sharti katika sheria ya sasa linalotaka kwamba Mwenyekiti wa Mamlaka ya Rufaa ya Zabuni lazima awe Jaji wa Mahakama Kuu. Hii ni kwa kuzingatia kwamba jukumu ka Mamlaka ni kutoa usuluhishi wa kitaalam, na kuwa bado Sheria inaruhusu mlalamikaji ambaye hakuridhika na maamuzi ya Mamlaka ya Rufaa za Zabuni kuwasilisha rufaa yake Mahakamani kwa ajili ya mapitio ya kisheria yaani *Judiciary Reviw.*

Aidha kwa kutambua mchango wa sekta binafsi marekebisho yanapendekezwa ili kushirikisha sekta binafsi zenye taaluma katika masuala ya zabuni na katika uwakilishi ndani ya Mamlaka ya Rufaa za Bodi. Saba, kifungu cha 34 cha Muswada ambacho ni kipya kinapendekeza kuanzishwa kwa vitengo vya ununuzi yaani *Procurement Management Units* katika ngazi za Wizara, Idara za Serikali na Mashirika ya Umma ili kusimamia shughuli zote zinazohusiana na manunuzi katika asasi hizi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiacha maeneo yaliyofanyiwa marekebisho na Muswada huu Kanuni ambazo zilitengenezwa chini ya Sheria ya mwaka 2001 nazo zitafanyiwa marekebisho ili kuboresha utendaji Serikalini. Maeneo muhimu yatakayofanyiwa marekebisho katika Kanuni hizo ni yafuatayo:-

Kwanza muda uliowekwa katika kuitisha zabuni mbalimbali utapunguzwa kulingana na aina ya zabuni na washiriki wa zabuni hiyo.

Pili, Kanuni zitaweka wazi utaratibu utakaotumika katika kutekeleza miradi ya jamii katika ngazi ya kijiji mfano MMEM, *TASAF* na kadhalika kwa miradi inayofadhiliwa na Serikali au wafadhili katika jumuiya iwe ni moja kwa moja au kwa utaratibu wa kuchangia gharama yaani *Cost Sharing.*

Tatu, kanuni zitaweka pia utaratibu utakaoziwezesha Taasisi kuwa huru kununua kutoka sekta ya binafsi badala ya Bohari za Serikali na pia kununua moja kwa moja sokoni au kwa mzalishaji pale inapoonekana wazi kuwa hatua hiyo itaokoa fedha za umma au kuongeza ufanisi bora wa utendaji. Sheria ya Uwezeshaji, itakumbukwa kwamba katika kikao cha Bunge kinachoendelea Bunge lako Tukufu lilipitisha Sheria ya Uwezeshaji ya mwaka 2004 *The National Empowerment Act, 2004.* Kwa kuzingatia maudhui ya Sheria hiyo, Muswada huu umeweka maeneo ya upendeleo kwa kampuni za Kizalengo na kutoa nafasi kwa kampuni zitakazowezeshwa chini ya sheria hiyo.

Makampuni ya Kizalendo yaliyopo yatashirikishwa kwenye zabuni zinazotolewa na Serikali kwa kuyaondolea vizingiti vilivyopo ndani ya taratibu na kanuni yaani *Regulations* zilizopo sasa. Hii ni kuzingatia ukweli kuwa kumsaidia mwenye kutembea ili akimbie hatua kwa hatua ni busara zaidi kuliko kumkimbiza yule ambaye bado hajaanza kutembea yaani anatambaa. Naamini kuwa hatua hiyo inaweza kutumiwa kuzipa uwezo kampuni za Kitanzania kutimiza masharti muhimu ya zabuni na kuwadhamini Watanzania katika kufanya biashara na Serikali kwa kuhakikisha kuwa wanapata mitaji na vitendea kazi vinavyohitajika kwa kuwezeshwa kwa dhati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Muswada katika vifungu vya 49 na 50 umeweka upendeleo kwa kampuni za Kitanzani pale zinaposhiriki kwenye zabuni, kanuni zitakazotengenezwa chini ya vifungu hivi zitazingatia mambo yafuatayo:-

Kwanza viwango vya upendeleo yaani *Margin of Preference* vya 10% kwa ngazi ya ujenzi na 15% kwa bidhaa zinazozalishwa nchini zitabaki palepale, lakini msisitizo utawekwa kuhakikisha kwamba vinatumiwa kwelikweli. Viwango hivyo pia vitatumika

chini ya utaratibu huo pale ambapo kampuni za nje zinashiriki na hata pia kwenye kazi za ushauri wa kitaalamu yaani *Consultancy Services* tofauti na ilivyo sasa.

Mbili, kiwango cha Shilingi 200, 000,000/= kwa zabuni zinazotengwa kwa kampuni za Kitanzania pekee kitaongezwa hadi Shilingi 500,000,000/= ili Watanzania wawe na wigo mpana zaidi wa kufaidika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuzidi kutambua umuhimu wa ushirikishwaji wa kampuni za Kitanzania kifungu cha 49 kimeweka pia upendeleo kwa kampuni za Kitanzania zinaposhiriki katika zabuni za kimataifa au kitaifa kwa kuhakikisha kuwa vinakuwepo vivutio kwa kampuni za nje kushirikiana na kampuni za Kitanzania kwa njia ya ubia yaani *Joint Venture* au kuuziana kazi *Sub-Contracts.* Utaratibu huo utaainishwa kwenye kanuni, utaratibu huu utasaidia kuinua uwezo mdogo wa mtaji, utaalam na teknolojia wa kampuni za kitanzania ili hatua kwa hatua ziweze kuwa na sifa za kufaidika na upendeleo uliowekwa na vifungu vingine vya sheria. Kwa kuzingatia uwezo mdogo wa kampuni za Kitanzania Muswada unaruhusu kugawanya zabuni kwa lengo la kuziwezesha kampuni nyingi ndogondogo kushiriki katika zabuni moja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hitimisho, mabadiliko yanayopendekezwa ya kutunga sheria mpya ya ununuzi badala ya ile iliyopo sasa yamezingatia ukweli kwamba zaidi ya 70% ya fedha za bajeti ya kila mwaka ya Serikali hutumika kwa ajili ya ununuzi wa vifaa, huduma na kandarasi za ujenzi mbalimbali, hivyo Serikali haina budi kuhakikisha kwamba ununuzi unafanyika kwa umaskini na uwazi ili kudhibiti matumizi na pia kwamba sehemu kubwa ya fedha hizo ni kwa ajili ya kuwanufaisha wananchi wake kama inavyofanywa kote duniani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya uchumi mpana kuendelea kuimarika Serikali sasa imepata fursa ya kuanza kuchukua hatua za kuwawezesha wananchi kunufaika na neema hiyo, tayari hatua zinazolenga Elimu ya Msingi na ya Sekondari, Afya ya Msingi kwa wote, Bima za Afya, miradi ya barabara za lami na za moramu, maji mijini na vijijini na kadhalika kote nchini zitaendelezwa na kuimarishwa kadri tutakavyozingatia vita vyetu dhidi ya umaskini.

Kwa sasa hatua zinazolenga kuboresha uchumi wa wananchi hasa wanyonge hususani katika sekta za kilimo, fedha, viwanda na biashara ndogo na za kati na sekta isiyo rasmi zimeanza kuchukuliwa. Upendeleo unaopendekezwa katika Muswada huu kwa wakandarasi wa Tanzania ni sehemu tu ya utayari huo wa Serikali ambayo kama nilivyodokeza mwezi Juni, 2004 katika hotuba yangu ya Bajeti sharti uendelee kujitokeza katika sheria nyinginezo na katika Wizara na vyombo vyote vya umma ili vikidhi haja hiyo ya kuinua hali ya Mtanzania kiuchumi, kama mkakati wa kupambana na umaskini na kukuza uchumi wa Taifa unavyotaka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naamini kwa dhati kwamba Muswada huu utaishia kwenye sheria iliyobora kuliko hiyo inayorekebishwa sasa, na ni matumaini yetu sote kuwa tutaiunga mkono.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA:** Mheshimiwa Spika Naafiki

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*

**MHE. LEPHY B. GEMBE (k.n.y. MHE. NJELU E. M. KASAKA MWENYEKITI WA KAMATI YA FEDHA NA UCHUMI):** Maoni ya Kamati ya Fedha na Uchumi kuhusu Muswada wa Sheria ya Ununuzi ya Mwaka, 2004 *(The Public Procurement Bill 2004).*

Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote napenda kukushukuru wewe kwa kunipa kwa kunipa nafasi hii ili niweze kutoa maoni ya Kamati baada ya kuuchambua na kuujadili Muswada wa sheria ya Ununuzi ya Mwaka 2004.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mujibu wa Kanuni ya 70, Kanuni Ndogo ya 2 ya Kanuni za Bunge, toleo la Mwaka 2004, naomba sasa niwasilishe maoni ya Kamati kuhusu Muswada uliotajwa hapo juu ambao unakusudiwa kufanya Marekebisho na kuboresha sheria ya ununuzi ya Mwaka 2001.

Ni matumaini ya Kamati kuwa ili kuifanya sheria mpya ya kutekelezeka kwa uwazi, usawa na kwa ufanisi mkubwa mabadiliko kama hayo ni vema yakaendelea kufanyika pale itakapooneka inabidi kufanya hivyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mabadiliko yaliyofanyika yanatokana na mapungufu kadhaa yaliyokuwepo katika sheria ya mwaka 2001 pamoja na kanuni zake kutokana na urasimu mkubwa, udhibiti hafifu na tija ndogo katika manunuzi ya umma, aidha kumekuwepo na milolongo ya hatua za kupitiwa kuanzia wakati wa kuitisha mpaka kutoa zabuni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokana na uzito na unyeti wa Muswada huu, Kamati yangu ilipata fursa ya kufanyiwa semina ya siku mbili jijini Dar es Salaam iliyoandaliwa na Wizara ya Fedha na kufunguliwa na Waziri wa Fedha, Mheshimiwa Basil Pesambili Mramba - Mbunge, ambayo ililenga katika elimu juu ya makusudio ya kuifanyia mabadiliko sheria ya Manunuzi ya Mwaka 2001.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tarehe 9-10 Novemba, 2004 tukiwa hapa Bungeni Kamati ilikutana na Wadau mbalimbali ambao walitoa maoni yao kuhusu Muswada, ambayo kwa kiwango kikubwa yamesaidia kuboresha maeneo mbalimbali ya Muswada huu. Wadau hawa ni pamoja na Baraza la Ujenzi la Taifa, Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Serikali, Bodi ya Usajili ya Wahandisi, Bodi ya Usajili ya Wasanifu Majengo na Wakadiriaji, Bodi ya Usimamizi wa Vifaa, Bodi ya Uhasibu na Ukaguzi Tanzania na Baraza la Biashara, Viwanda na Kilimo Tanzania *Chamber of Commerce, Industry and Agriculture.* Kamati inawashukuru sana kwa michango yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti baada ya kuuchambua na kuujadili kwa kina Muswada na baada ya Waziri wa Fedha kuzingatia maoni yaliyotoka kwa wadau mbalimbali Kamati inaunga mkono hoja ya Serikali pamoja na maoni kama ifuatavyo:-

Moja, kuzingatia kuwa zaidi ya takribani 70% ya fedha za Bajeti ya Serikali hutumika kwa ajili ya ununuzi wa vifaa, huduma na kandarasi za ujenzi mbalimbali hivyo basi Serikali halina budi kuhakikisha kwamba ununuzi unafanyika kwa umakini, uwazi na kwa ufanisi mzuri ili kudhibiti matumizi ya Serikali

Mbili, kwa kuzingatia sheria mpya inayokuja ya uwezeshaji inashauriwa kazi mbalimbali kama vile za ujenzi zikigawanywa katika thamani ndogo ndogo ili kuzipa fursa kampuni ndogondogo za Kitanzania kushiriki katika kupata zabuni za aina hiyo *Sub - Contracting* katika ushindani wa kitaifa na kimataifa *(International and National Competitive Tendering)*

Tatu, inashauri ya kwamba Wakurugenzi wa Halmashauri wahusishwe moja kwa moja katika bodi za zabuni za Halmashauri zao na wanatakiwa wawe Wenyeviti wa zabuni hizo ili waweze kushirikishwa na kusimamia vema na kwa kuwa wao ndiyo watendaji wakuu wa Halmashauri hizo ili waweze kuwajibika kama kutakuwa na ukiukwaji wa taratibu wa *tender* hizo.

Nne, Kamati vile vile inashauri Serikali iajiri watumishi wenye sifa na kuwa na mpango maalumu wa kuwasomesha watendaji wa Halmashauri waliopo ili waweze kuwa na utaalamu unaokubalika na bodi ya usimamizi wa vifaa yaani *The National Board of Materials Management.*

Tano, Kamati inashauri pia mara baada ya sheria kupitishwa ni vema kanuni zitakazotumika katika kuitekeleza sheria zikawasilishwa mbele ya Kamati na Wadau husika ili kujitosheleza jinsi sheria itakavyofanya kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kumshukuru tena Waziri wa Fedha Mheshimiwa Basil Mramba - Mbunge, Naibu Waziri wa Fedha Mheshimiwa Abdisalaam Issa Khatibu, Katibu Mkuu Mwandamizi wa Wizara Ndugu Grayson Mgonja, Mwanasheria Mkuu wa Serikali, kwa kuitolea Kamati ufafanuzi mbalimbali uliosaidia kukamilisha kazi ya kujadili Muswada huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuwashukuru Waheshimiwa Wajumbe wa Kamati yangu ya Fedha na Uchumi na Waheshimiwa Wabunge kutoka Kamati ya Hesabu za Serikali kwa michango yao ya makini iliyosaidia kwa kiwango kikubwa kuboresha maudhui ya Muswada huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda sasa kutamka kuwa kamati yangu iliupitisha Muswada baada ya maoni mbalimbali yaliyotolewa na kuingizwa kwenye Muswada na ambayo kimsingi Mheshimiwa Waziri wa Fedha aliyakubali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo naunga mkono hoja na naomba kuwasilisha. *(Makofi)*

**MHE. DR. WILLBROD P. SLAA (k.n.y. MHE. HAMAD RASHID MOHAMED - MSEMAJI WA UPINZANI KWA WIZARA YA FEDHA):** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza napenda kuchukua nafasi hii kukushukuru wewe binafsi kwa kunipa nafasi hii ili kutoa maoni ya kambi ya Upinzani kuhusu Muswada wa Ununuzi wa Umma wa Mwaka 2004 ulioko mbele ya Bunge lako Tukufu.

Napenda pia kutoa pongezi za dhati kwa Mheshimiwa Waziri na timu yake ya Manaibu Mawaziri, Makatibu Wakuu na Wataalamu kwa kazi kubwa ya kuandaa Muswada huu. Lakini napenda kutoa pia masikitiko kidogo kwa sababu nimepokea *Schedule of Amendment* sasa hivi na karibu ni kubwa sawa na Muswada wenyewe. Kwa hiyo, kama kuna vitu nitavisema vimeshashughulikiwa basi ionekane ni kwa sababu marekebisho yamechelewa kuja na tungeomba siku zijazo ili tufanye haki basi marekebisho yoyote yaweze kutufikia mapema kwa sababu sisi tunaandika hotuba zetu na tunazifanyia kazi sasa ikitufikia wakati hotuba inaanza kutolewa hatuwezi kuzishughulikia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jina refu la Muswada ulioko mbele ya Bunge lako Tukufu ni Muswada wa Kufuta Sheria ya Manunuzi ya Umma ya Mwaka 2001, kwa lengo la kuboresha taratibu za umma katika Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, pamoja na kutoa utaratibu wa mambo yanayohusiana na taratibu hizo. Tafsiri hiyo ni ya kwangu kwa kuwa imeandikwa kwa kingereza hivyo basi Kambi ya Upinzani inayo maoni yafuatayo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza, Serikali kuwa makini katika kupitisha sheria, kwa mtu yeyote anayefanya utafiti na anayefuatilia mambo katika Bunge letu leo atakuwa na furaha ya pekee kwa vile yale yaliyosemwa na Wabunge wengi wa CCM na wa Kambi ya Upinzani leo yamethibitika. Wabunge wengi wakati wa kujadili Muswada wa Manunuzi ya Umma wa Mwaka 2001 walipendekeza mambo mengi ambayo Serikali katakata iliyaka na hayo hayo leo yameletwa mbele yetu na siyo tu sheria inafanyiwa marekebisho bali sheria ya Mwaka 2001 yote kabisa inafutwa na kuandikwa upya. Serikali ingelikuwa makini wakati ule, leo tungelikuwa tunafanya labda marekebisho madogomadogo tu kuendana na mabadiliko mbalimbali ya kisayansi, kiteknolojia au kijamii lakini si kuandika upya sheria nzima.

Mheshimiwa Mwenyekiti, isitoshe sote ni mashahidi jinsi sheria hiyo ilivyopitishwa wakati ule na matokeo yake ni kuwa toka dakika ya mwanzo utekelezaji wa sheria hiyo kwa sehemu kubwa ilikuwa ni ngumu na Mheshimiwa Waziri Ndugu yangu sana Mheshimiwa Mramba amekiri ndani ya Bunge hili mara kadhaa kwamba fedha nyingi hazikutumika kutokana na ugumu wa sheria ile pamoja na Wataalam wengi kutokuielewa sheria hiyo. Pamoja na hayo Kambi ya Upinzani inayo furaha kuwa Muswada huu umeletwa tena kwa lengo la kufanya marekebisho makubwa hasa ikizingatiwa kuwa aghalabu 70% ya Bajeti kwa matumizi ya kawaida inatumika katika

manunuzi na 100% ya Bajeti inatumika katika manunuzi ya miradi ya maendeleo, kwa Bajeti ya maendeleo.

Hivyo ili fedha za umma kidogo zilizoko siyo tu zitumike vizuri lakini pia zikasimamiwe vizuri. Muswada huo ni hatua moja katika kuweka katatibu imara za kusimamia fedha hizo. Pia Muswada huu ni hatua muhimu pia katika kuziba mianya ya rushwa katika Idara za Serikali, Taasisi na Mashirika ya Umma, Halmashauri za Miji, Manispaa na Wilaya, ni kwa msingi huu kuwa iwapo marekebisho tunayopendekeza yatazingatiwa na Serikali, Kambi ya Upinzani kimsingi haina tatizo na maudhui ya Muswada wenyewe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na furaha tulizoeleza hapo juu, Muswada huu bado unayo maeneo kadhaa yanayohitaji kurekebishwa hata sasa ili uwe na manufaa yanayotegemewa.

(a) Sheria na 3 ya Mwaka 2001 sasa inafutwa na kuweka Sheria ya Ununuzi ya Mwaka 2004 kwa malengo ambayo sote tunakiri kuwa ni kama ifuatavyo:- Matumizi mazuri ya fedha za umma, Usimamizi imara wa fedha za umma, Manunuzi kufanyika kwa misingi ya haki yaani kati ya waombaji na kufuta misingi yote ya ubaguzi katika utoaji wa Tenda za Serikali na Taasisi zake zikiwemo Halmashauri, Utoaji Tenda kwa misingi ya Uwazi *(Transparency)* na Uwajibikaji *(Accountability).* Pamoja na nia hii njema, kwa mtu yeyote aliyeisoma sheria hii vizuri bado ina mapungufu katika kufikia malengo yaliyoainishwa hapo juu. Mathalani Muswada japo unalenga kutumika pia katika Serikali za Mitaa, lakini utaratibu wa manunuzi katika Serikali za Mitaa hauko wazi kabisa na unatoa mianya mingi ya kuruhusu ubadhirifu na rushwa kama tutakavyoona hapa chini.

(b) Mheshimiwa Mwenyekiti, isitoshe Serikali za Mitaa hadi sasa inatumia Kanuni za Fedha za Serikali za Mitaa, yaani, *Local Authority Financial Memorandum.* Ni vema Waziri akafafanua wakati wa kujibu hoja uhusiano kati ya Kanuni hizo na Sheria hii mpya kuondoa utata uliokuweko na unaoweza kujitokeza tena. Katika Tafsiri ya neno *Procuring Entity* na nimeona *Schedule of Amendments* sina hakika kama imeelezwa vizuri. Kwa mfano, Muswada uliweka wazi *Local Government,* lakini *Schedule of Amendment* iliyofuta ikafuta na sasa *Schedule of Amendment* inayokuja inafuta tena neno liloandikwa *Statutory body* sijapata muda wa kuangalia maana ya hiyo ni nini? Lakini naona kwamba neno *Local Government* limerudishwa badala ya jumla *Statutory Board* hilo kwetu ni furaha. *Local Government* sasa hivi ipo kwenye hatua kubwa ya Maboresho na ina utaratibu wake uliokomaa. Lakini kwa sheria hii imefunikwa tu, jambo ambalo ni hatari sana kwani kazi nyingi za Serikali zinafanyika katika ngazi ya Serikali za Mitaa hivyo ni lazima kuwe na utaratibu ulio makini na wa wazi kabisa.

(c) Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kuwa Muswada wa Sheria ya Manunuzi wa 2004 unahusisha Taasisi na Mashirika ya Umma, Kambi ya Upinzani inadhani kuwa utaratibu wa *Dual List* unaowekwa kutumika katika majeshi yetu unahitaji kuboreshwa zaidi. Kifungu cha 2(b) kama hakijabadilika kutokana na *Schedule of Amendments* unaweka manunuzi yaliyoko katika *Restricted List*. Kambi ya Upinzani

inaamini kabisa manunuzi makubwa na ya gharama kubwa sana yanafanywa na Jeshi letu. Hivyo, badala ya kuiacha kuwa katika *Restricted List*, kuwe na Chombo kinachosimamia manunuzi hayo ya *Restricted List* ndani ya Jeshi lenyewe. Tunamtaka basi Waziri angalau wakati wa kutengeneza Kanuni za utekelezaji wa Sheria hii, aweke muundo utakaotumika katika Jeshi kwa ajili ya Manunuzi yaliyoko katika *Restricted List* yaani manunuzi yanayobaki kuwa siri ya Jeshi letu kwa sababu za ki- usalama. Lakini yasiachwe holela hata kidogo. Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mfano ndogo tu taarifa ya *CAG* tuliyopokea leo inaonyesha kuwa Ngome peke yake yaani Jeshi letu Kikosi cha Ngome ilikuwa na matumizi ya *store* ambayo hayako kwenye ledger ya shilingi bilioni 6.2. Hizi ni fedha nyingi sana tusibahatishe kuwe na utaratibu maalum wa *check and balance* na ndiyo msingi wa utawala bora.

(d) Japo Muswada unatamka kuwa *Restricted Procurement Methods set out in this act.* Lakini hazitajwi popote hizo methods baadaye katika Muswada kwa aliyesoma. Ni vema Waziri akazingatia eneo hili kwa umakini kwa lengo la kufikia malengo ya Muswada huu. Mheshimiwa Mwenyekiti, kama tulivyosema mwaka 2001 bado Kambi ya Upinzani inasisitiza kuwa Sheria ya Manunuzi itambue Sheria nyingine zilizoko. Sheria hizi zinahitaji kuoanishwa vinginevyo tutaendelea kuwa na migongano katika utekelezaji na hatutafikia malengo tuliyoyategemea. Kwa mfano Sheria iliyoweka *NBMM* inaweka viwango vya elimu vinavyotakiwa kwa Watunza *Store,* na bila kuzingatia hiyo tutapata migongano isiyo lazima. Sheria ya *Architects and Quantity Surveryors* na *By laws 2000* ambazo zinatokana na Sheria na 16 ya 1997 ni mifano hai ambayo inaweka misingi na mfumo wa ushindani katika miradi ya ujenzi wa majengo. Bodi ya Dawa nayo imeundwa kisheria na kwa mujibu wa sheria hiyo, nayo inatakiwa kuratibu manunuzi ya Madawa. Nimeona kwenye gazeti moja tayari kuna tatizo la tenda ya madawa ya milioni 500. Sasa haya ni mambo ambayo yanahitaji kuangalia sheria za Bodi mbalimbali zinazohusika. Utaratibu wa kudumu unatakiwa kufanyiwa kazi ya umakini, na Kambi ya Upinzani inaamini kuwa Marekebisho haya, kama ilivyo sheria ya 2001, yatakumbana na matatizo iwapo Serikali haitakuwa makini tena.

(e) Mheshimiwa Mwenyekiti, malighafi na hata huduma ni za aina tofauti, na kila moja ina mambo yake maalum. Kwa mfano, dawa za hospitali utaratibu wake ni tofauti sana na utoaji wa Tenda ya mahindi au maharage shuleni. Tenda ya mbao nayo ina utaratibu tofauti na wa Madini, kwani kila kimoja inaratibiwa pia na sheria yake tofauti. Kambi ya Upinzani inaamini kabisa kuwa hatujafanya kazi ya kutosha kuoanisha na kuhuisha sheria hizi mbalimbali ndani ya sheria hii mpya. Hivyo muundo wa Bodi za Tenda nao ni lazima uzingatie masharti ya huduma au shughuli zinazohusika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, dunia ya leo iko kwenye Karne ya Sayansi na Teknolojia. Hatuwezi tena kuwa Kisiwa sisi Tanzania. Ulimwenguni leo inawezekana kabisa kununua jambo lolote kwa njia ya Mtandao *( E-Procurement).* Ni kweli kuwa kimsingi utaratibu wa matumizi ya karatasi ni vigumu kabisa kuondoa. Lakini matokeo ya mtandao ni kuwa katika manunuzi mengi badala ya kubadilishana barua, badala ya majadiliano ya bei kufanyika kwa watu kukutana uso kwa uso yote haya yanaweza kufanyika kwa mtandao. Manufaa ya mtandao ni kuwa mambo yanaenda kwa haraka sana, taarifa juu ya upatikanaji wa jambo fulani ni wa haraka zaidi na wa uhakika zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Muswada ulioko mbele yetu haugusii nafasi ya Mtandao pamoja na kuwa unazungumzia tu juu ya *Wide Data System,* hakuna mahali anapoeleza maana ya *Wide Data System* na kwenye *interpretation* wala haielezwi. Lakini pia haitoi ufafanuzi wowote wa *E-Procurement.* Kambi ya Upinzani inafikiri kuwa kuingia Karne ya Sayansi na Teknolojia ni pamoja na matumizi ya mtandao katika shughuli mbali mbali za Serikali. Wakati tunafanya maandalizi ya *E-Government,* ni lazima pia tuzingatie matumizi ya *E-Procurement,* ama sivyo tutajikuta tuko nyuma, na hatuhitaji kutunga sheria nyingine, wakati tungeliweza kuweka vifungu mbalimbali vya *E-Procurement* katika Sheria hii. Tunamtaka Mheshimiwa Waziri aliambie Bunge lako Tukufu, Serikali inafikiri nini kuhusu *E-Procurement* katika Sheria hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Katika Kifungu cha 5(1) ambacho kinaunda Mamlaka itakayojulikana kama *Public Procurement Regulatory Authority.* Kifungu hiki hatuna tatizo nacho kimsingi, lakini Kambi ya Upinzani tusingelipenda kuona Sheria hii inagongana na Sheria ya *NBMM* inayotoa Mamlaka ya kusimamia *Training Standards* kwa Bodi ya *NBMM* kama ilivyo katika kifungu cha ( 7)(1)(c) cha Muswada huu. Wasiwasi wetu mkubwa ni katika Bodi za Tenda hasa za Mamlaka ya Serikali za Mitaa. Kambi ya Upinzani inaitaka Serikali kufikiria upya muundo wa Bodi za Tenda katika Mamlaka za Serikali za Mitaa kwa sababu zifuatazo:-

(a) Nia ya Serikali kwa muda mrefu imekuwa kujenga uwezo wa Serikali za Mitaa na fedha nyingi zimetumika katika kufikia nia na lengo hilo. Kilichotokea haionyeshi Serikali ina nia hiyo katika Muswada huu.

(b) Kwa mawazo ya Serikali, Bodi ya Wakurugenzi na Baraza la Madiwani wana jukumu la kupitisha Bajet ya Shirika au Halmashauri katika mwaka wa fedha husika. Baada ya hapo wana jukumu la kufuatilia utekelezaji. Mkuu wa Shirika au Mkurugenzi Mtendaji ana jukumu la kuhakikisha kuwa anatekeleza majukumu yote yaliyopo kwenye mpango wa utekelezaji wa mwaka na mwisho wa mwaka anatakiwa kuwajibika kwenye Bodi ya Wakurugenzi au Baraza la Madiwani. Tuna tatizo na nia hiyo ya Serikali.

(c) Serikali inasisitiza pia kuwa Mkurugenzi hapimwi kwa zabuni alizotoa mwaka ule, ila anapimwa kwa kazi alizotekeleza. Tuna tatizo kubwa na hilo. Hivyo, Kambi ya Upinzani kimsingi hatuna tatizo la kutenganisha majukumu kati ya Bodi au Baraza la Madiwani na Wakurugenzi. Lakini kwa utaratibu unaopendekezwa na Muswada, Mkurugenzi ndiye anayemteua Mkuu wa Idara kuwa Mwenyekiti wa Bodi ya Tenda. Wajumbe sita wengine wa Bodi hiyo wanateuliwa nao na yeye mwenyewe na anawateua kutoka kwa Wakuu wake wa Idara. Katibu naye, anatoka ndani ya *Procuring Entity,* yaani anatoka humo humo ndani ya chombo ambacho Mkurugenzi anakisimamia yaani wote ni watumishi walio chini ya Mkurugenzi huyo huyo. Kisha kuundwa watafanya kazi zote zilizotajwa chini ya kifungu cha 30 cha Muswada, yaani tangu kuandaa *tender documents,* kutekeleza kazi, kusimamia kazi, kutoa tathmini ya kazi na kutoa taarifa ya kazi kwa mamlaka husika, yaani Baraza la Madiwani kwa maana ya Halmashauri. Mkurugenzi au *CEO* akiwa mtu mzuri mambo yanaweza kuwa mazuri pia. Lakini akiwa bomu, rushwa sasa inakuwa ndiyo imeidhinishwa rasmi. Kambi ya Upinzani inaona kuwa kwa vile:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, hakuna mahali popote sheria inapowataka watoe taarifa kwa Mamlaka. Inaonekana kutoa taarifa ni hisani ya Mkurugenzi na Bodi yake ya Tenda. Pale Mkurugenzi anapokuwa mtu mzuri na safi hakuna tatizo. Lakini taarifa za mara kwa mara za *CAG* ni ushahidi ulio wazi kuwa mambo katika Halmashauri nyingi sivyo Serikali inavyotaka tuamini na kila mwaka mabilioni ya fedha yanapotea kutokana na matatizo ya ukosefu wa uaminifu. Waziri anataka kutuaminisha kuwa leo tuna Malaika katika Halmashauri au katika Mashirika yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivyo, Kambi ya Upinzani inadhani *Check and Balance* ni suala la muhimu katika kulinda mali za umma na fedha nyingi za umma zinazohusika katika manunuzi mbalimbali hasa katika ngazi ya Halmashauri. Natoa mfano, katika taarifa ya *CAG* tuliyopokea leo, taarifa hiyo iliyoishia tarehe 30 Juni, 2003 inaonyesha kwa mfano, manunuzi ambayo hayakufika *store* ni shilingi bilioni 7,842,000,000/= na tenda bodi zenyewe za Serikali Kuu matumizi ambayo yameidhinishwa bila kuwa na idhini ni shilingi bilioni 4,301,000,000/=. Manunuzi ambayo hayana idhini ni sawa tena na bilioni 8,754,000,000/=. Hali hii inataka umakini wa hali ya juu na hasa kuandaa sheria ambayo ni makini kweli kweli. Mheshimiwa Waziri anakumbuka kuwa mwaka 2001 aliahidi ndani ya Bunge hili wakati tunatunga sheria ya mwaka 2001 kuwa usimamizi utakuwa imara. Lakini taarifa ya 2003 imetokana na baada ya mwaka 2001 sheria imeshakuwepo inaonyesha bado kuna matatizo. Kwa hiyo Mheshimiwa Waziri leo asitwambie kwamba atasimamia au atatoa ahadi, lakini ni sheria yenyewe ndiyo iwe msimamizi siyo Waziri.

Hivyo, hata leo asipende kutoa ahadi wakati mianya yenyewe haijazibwa vizuri. Katika kipindi hicho hicho jumla ya matumizi yenye thamani ya shilingi bilioni 49,927,000,000/= ilikuwa au haina hati kamili au haina kabisa. Malipo ya shilingi bilioni 5, 963,000,000/= hayana hati kabisa na *CAG* anasema: *"In all cases of inadequate vouching they are authenticity. of expenditure incurred and the purpose for which the payments were made cannot be ascertained and fraud all miss appropriation of the somes involved cannot be ruled out."* Maana yake hatuwezi ku-*rule out* pamoja na kwamba leo bado hatujui kama imeibiwa. Lakini kwa kawaida kutokuwa na hati ni dalili kuwa kuna wizi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivyo, sheria tunayotunga ni lazima imsaidie Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu wa Serikali katika utekelezaji wa wajibu wake na kulinda mali ya umma. Katika Taarifa tuliyopokea pia *CAG* analalamika na ninaomba ninukuu: *"Poor controls of expenditure under Accounting of Stores constitute a very serious concerned."* Kwa wale wanaosoma taarifa za Mkaguzi hii ni kilio cha kila mwaka cha Mkaguzi ni lazima sasa haya tuyazibe sio kwa ahadi tu ya mdomo, lakini kwa sheria iliyo dhabiti na inayoweza kuhakikisha kwamba tunasimamia yale tunayoyatamka. Udhibiti hauwezi kuwepo kama hakuna *mechanism* ya *check and balance* na *mechanism* hiyo haitapatikana tu pale Bodi itakapohusisha watu wasiohusika moja kwa moja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kutamka hilo. Tunafikiri kwamba kuna mambo mengi ambayo bado yanahusika. Katika mambo mengi ambayo tumeyaona

yanahusika ni suala nzima ambalo tumeona halikuwekewa mkazo na Serikali ni tatizo ambalo Serikali yetu imeliweka pembeni. Hili ni suala ambalo Madiwani kwenye Bodi za Tenda sisi hatudhani kwamba ni lazima wawepo Madiwani wala sisi tusingelipenda iwe hivyo.

Lakini kwa ajili ya Uwajibikaji na uwazi, Kambi ya Upinzani inasisitiza kuwa Mwenyekiti apendekezwe na Mkurugenzi na kati ya majina mawili au matatu yatakayopendekezwa kwa Baraza la Madiwani, Baraza la Madiwani limteue Moja asipewe kazi ya kuteua Mkurugenzi ambaye ndiye anasimama kila kitu. Hii itahakikisha uwajibikaji kwa Baraza. Lakini vinginevyo tumeua uwajibikaji kabisa, na wala hapatakuwa na Uwazi *Transparency* ambayo Serikali inataka kujenga kila siku.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali pia inasisitiza kuwa Taarifa itawasilishwa mwisho wa Mwaka. Lakini Waziri anasahau tulikotoka, kwa kuwa taarifa ya *CAG* kuchelewa, fedha nyingi zinazopotea zinakuwa vigumu kuzirudisha yaani kuzi-*recover* wakati zimekwishakutumia baada ya mwaka mzima. Hivyo, Kambi ya Upinzani inapendekeza kwamba baadhi ya Wajumbe angalau wawili, watoke nje ya Mamlaka ya Halmashauri yaani wanaweza kuwa wafanya Biashara au viongozi wa dini au *NGO* katika eneo husika la Mamlaka na Mkurugenzi awe na mamlaka ya kupendekeza majina angalau kadhaa, mathalani 5 na kati yao wawili wateuliwe na Baraza la Madiwani. Hii itajenga Bodi imara na kuhakikisha uwajibikaji na uwazi katika matumizi ya mali na fedha za umma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Sheria au Kanuni itamke kabisa kipindi maalum ambapo Bodi ya Tenda itatoa Taarifa kwa Baraza la Madiwani au angalu Kamati ya Fedha ili kufuatilia kwa karibu kabla ya mwisho wa mwaka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tulikuwa tunadhani vilevile kwamba katika utoaji wa taarifa zetu ni muhimu Serikali ising'ang'anie msimamo wake. Lakini historia inaweza kuja kuihukumu, Serikali isikilize Waheshimiwa Wabunge wanasema nini na wana uzoefu gani kule kwenye maeneo yao. Matatizo kwenye Halmashauri yanajulikana na Waheshimiwa Wabunge wameyasema na Mheshimiwa Waziri sidhani kama ameyachukua vizuri kabla ya kuweka hii sheria yake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kambi ya Upinzani hatimaye, inamtaka Mheshimiwa Waziri alieleze Bunge hili pia, hatima ya Kanuni zilizotungwa chini ya Sheria ya Ununuzi 2001 na Kanuni zilizotungwa na Mheshimiwa Waziri wa Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa kwa mujibu wa kifungu cha 14 cha Sheria ya Manunuzi ya 2001 yaani *GN 48* na 49 ya 2003 kwa ajili ya matumizi ya Serikali za Mitaa. Je, kwa Sheria hii kanuni zote hizo sasa zimefutwa au zinabaki na kama zinaendelea kutumika sambamba, ikiwa ni pamoja na *Local Government Financial Memorandum* ni vipi zitaoanishwa na sheria hii mpya? Ufafanuzi huu ni muhimu kuondoa mikanganyiko ambayo ipo na inaweza kuendelea baada ya Sheria hii mpya. *Local Government Financial Memorandum* haitajwi popote katika sheria mpya, lakini ndiyo inayotumika kuendesha shughuli katika Halmashauri mbalimbali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni imani yetu kuwa Waziri atatoa ufafanuzi wa kina kuhusu masuala mbalimbali yaliyotajwa hapo juu. Kwa hayo machache.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuwasilisha. *(Makofi)*

**MHE. DR. MILTON M. MAHANGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipa nafasi ili niweze kuchangia kwenye Muswada huu wa Ununuzi wa mwaka 2004.

Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote nimpongeze Mheshimiwa Waziri wa Fedha pamoja na watalaam wake wote kwa kazi nzuri waliyoifanya kuwasilisha Muswada huu. Hii vilevile inadhihirisha yale ambayo wadau tumekuwa tukiyapigia kelele toka ule Muswada wa kwanza kupitishwa mwaka 2001. Nitamke wazi hapa kwamba kati ya watu waliofurahi sana siku ya leo ni pamoja na mimi kwa sababu mengi kwa kweli ambayo niliyazungumzia hasa ya utaalamu kwenye Muswada wa mwaka 2001 sasa imedhihirika kwamba ni kweli na yameingizwa yote. Kwa kweli nashukuru sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni wazi kabisa kwamba ununuzi unachukua asilimia kubwa sana ya bajeti ya Serikali, bajeti ya maendeleo ni asilimia karibu zote 100 na bajeti ya kawaida ni asilimia kati ya 60 na 70 zinakwenda kwenye manunuzi. Hata hiyo asilimia inayobaki 35 inayokwenda kwa watu kwa maana ya mishahara hao watu bado wanakwenda kufanya manunuzi ya nyumbani kama kununua mahindi kule Kibaigwa. Kwa hiyo, bado kwa kweli unaweza kusema fedha yote inakwenda kwenye manunuzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uzoefu unaonyesha kwamba katika bajeti kubwa hizi za Serikali mbalimbali zinazokwenda kwenye ununuzi asilimia kati ya 10 na 25 zinapotea kabla hazijafikia walengwa. Kwa maana kwamba kunakuwepo na rushwa, ubadhirifu na wizi kwenye suala nzima la ununuzi. Mimi nimezungumza na Mhasibu Mkuu wa Serikali na ameniambia kwamba kwa mwezi Serikali yetu inatumia kama bilioni 90 kwa ajili ya manunuzi ya Serikali. Sasa ukichukua hata asilimia 10 tu ya upotevu ambao unatokana na matatizo ya ununuzi kwenye nchi basi nchi hii tunapoteza bilioni 9 kwa kila mwezi au zaidi ya bilioni 120 kwa mwaka kwa ajili ya ubadhirifu, wizi, rushwa na upotevu wa vifaa wakati wa ununuzi na utumiaji wa vifaa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, na hili ndiyo maana tunasema kwamba ukiona majengo na majumba makubwa kule Mikocheni, Msasani na Masaki kwa watumishi wa umma asilimia kubwa ya majengo yale ndiyo hizi bilioni 120 zinazopotea, na ndiyo maana tunasema nchi hii hatuna *mortgage facility,* lakini watu tunaweza tukajenga majengo makubwa. Ndiyo hizi bilioni 120 kwa mwaka zinazopotea kutokana na ununuzi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo tunashukuru kwamba Muswada huu umerekebisha kasoro ambazo zilikuwepo kwenye Muswada wa kwanza, na kwamba sasa tunaamini kwamba ile bureaucracy iliyokuwepo itakuwa imeondoka baada ya Muswada huu kuanza kutumika. Lakini vilevile nia ya Muswada ya kulinda mali za

Taifa kwa njia za ununuzi unaofaa kuondoa rushwa na kero zingine za ubadhirifu kwenye manunuzi ya Serikali basi itakuwa imepungua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo kwa upande mmoja kwa kweli Muswada huu utatusaidia sana. Lakini mimi niseme kwamba bado Muswada huu umeshinikizwa kwa kiasi kikubwa na wafadhili na watu wa nje. Pamoja na kwamba anatwambia kubwa ni hii transparency kwamba tunapunguza rushwa, tunataka fedha zetu tulizowapa tuone zinatumika vizuri ni vyema. Lakini nia yao kubwa ni katika kuhakikisha kwamba kunakuwa na hizi *Reforms* za *Public Procurement* kwenye hizi nchi maskini ni ile *section 49* ya Muswada na pale mstari wa kwanza. Benki ya Dunia na nchi matajiri wanachotaka kikubwa kwao ni kile kipengele kinachosema *"suppliers, contractors or consultants are allowed to participate in Procurement proceedings without regard to their nationality."* Hicho ndicho wanachotaka ili waweze kuingia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, barabara katika nchi tajiri ziliishajengwa zamani ukarabati wenyewe ni mdogo sana. Madaraja walishamaliza ma-*contractors* wao hawana kazi kule kwao. Ni namna wanaweza wakaingia kwenye nchi zetu kama siyo kwa njia hii ya kuhakikisha kwamba hakuna vizuizi vya kuwazuia wasifanye Ukandarasi kwenye nchi maskini. Ndiyo maana tunasema kwa kweli kwamba kama kifungu kile cha 49 ile *except* hatukuiangalia kwa undani namna gani tunawasaidia Watanzania ili washiriki vizuri zaidi bado tunaweza tukawa na matatizo ya kuendelea kuwafaidisha hao matajiri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nasema tuupitishe huu Muswada kama ulivyo, lakini kwa kweli tunapokwenda sasa kutengeneza kanuni au baadaye kurekebisha huu Muswada tuendelee kuangalia na sheria ya uwezeshaji. Ukweli ni kwamba nchi tajiri zilianza mpango huu zamani sana. Baada ya kuona kwamba masoko yao yamezibika ni lazima wayapanue. Walianza kwenye miaka ya 60 wanachoita *Canage Round of Trade Negotiations.* Wakasema sasa namna gani tuingie kwenye nchi zingine, wakasema lazima waondoe vizuizi vya kodi. Baadaye kwenye miaka ya 70 wakasema vizuizi wa kodi tu havitoshi, vipi vizuizi vya biashara huru kokote duniani ndiyo sasa ikaingia ile iliyokuwa inaitwa *Neckson Round of Negotiations* kwenye miaka ya 70 hadi mwaka 1973 wakaenda pale Tokyo wakatoa *declaration* kwamba Bwana sasa ni lazima tuingie kwenye nchi zote kwa kufanya biashara. Hii imepelekea baada ya Shirika la Ulimwengu lile la biashara *World Trade Organization* kuanzishwa wakaanzisha kinaitwa *Government Procurement Agreement.* Wakataka nchi zote ziingie mpaka sasa nchi zetu hazijaingia kwenye ule Mkataba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa Mheshimiwa Waziri atueleze ni kwa nini Tanzania kwa mfano hatujaingia kwenye ule Mkataba wa *Government Procurement Agreement.* Kwa sababu yale makubaliano yanatutaka tukubali hawa watu waingie kiholela. Lakini sasa hivi wametulazimisha tuingie huko kwa kuweka Miswada kama hii na hasa *section* hiyo 49 ambayo itafanya ukitaka kutangaza zabuni unatangaza dunia nzima. Kwa sasa ni nchi 28 tu na hakuna nchi ya Afrika iliyokubali kuingia kwenye huo Mkataba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini tatizo lake ndilo hilo, lakini tunalikubali kwa njia nyingine wakisema Bwana tunataka mhakikishe kwamba kunakuwepo na uwazi na fedha zetu tunaziona kwamba zinatumika vizuri. Lakini ukweli ni kwamba wanataka wapate biashara na walete Ukandarasi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Rais amesema juzi, magazeti jana na magazeti ya leo kwamba hizi nchi tajiri ni watu wabaya sana. Ni watu ambao ni lazima washibe kwanza kile kinachobaki ndiyo sisi kinakuja kwetu. Asilimia 80 na Mheshimiwa Rais amesema nimesoma kwenye gazeti. Kwa mfano, Ukandarasi au Ushauri asilimia kubwa zinakwenda kwao, zinarudi huko, barabara hizi tunazotengeneza fedha zote zinarudi huko huko hakuna zinazobaki hapa nchini, na ule uwezo ndiyo hatuupati tukitaka tupate uwezo ndiyo kunakuwa na vikwazo vingi. Kwa hiyo, wataendelea kutunyonya kwa kweli.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa ndipo tunaposema kwamba kwa nini barabara zimetengenezwa na umaskini unaendelea, kwa sababu wametengeneza barabara na fedha zote walizotengenezea zimekwenda kwao. Fedha hizi zingekuwa zinabaki hapa nchini tungeweza kupunguza umaskini kwa kiasi kikubwa.

Lakini hawa ni wajanja hatuwezi kufanya hivyo kwa sababu wametushika vilivyo. Sasa ni tatizo ambalo lazima tujikwamue kwa kuweka sheria za makusudi za kutuwezesha sisi Watanzania za kuwalazimisha wanapokuja hapa nchini lazima wapitie kwenye Makampuni ya hapa nchini. Pale Afrika ya Kusini kuna Makampuni *Black Eonomic Empowerment,* kuna makampuni matatu makubwa zaidi na mengine madogo madogo kiasi ni ya Waafrika Kusini, hupati kazi katika nchi ile kama hujapitia kwenye Makampuni hayo, lazima uingie ubia na hao Waafrika weusi.

Sasa tusipofanya hivyo kwamba hujengi barabara Tanzania bila kushirikisha Kampuni ya Kitanzania hakuna kazi, kwa makusudi tunaweka kwa nini nchi zingine zimekubali hilo. Sasa hilo nadhani ni jambo ambalo lazima tulifanye huko tunakokwenda. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nijielekeze kwenye suala la utaalamu. Mimi kama nilivyosema nashukuru sana kwamba suala la utaalamu limezingatiwa na limezingatiwa dakika za mwisho. Kwa sababu ununuzi ni utaalamu na mimi naona kwa muda mrefu tumekuwa na shukrani ya punda. Watu wakizungumza kabisa kwamba nchi hii haikuwa na wanunuzi kwa miaka yote hii hayo ni matusi.

Toka kabla ya uhuru nchi hii tunanunua vifaa kutoka nje na kutoka ndani. Leo juzi baada ya *World Bank* kuja kutulazimisha na Muswada huu unasema kwamba hakuna wanunuzi, waliokuwepo ni watunza stoo tu kweli! Kulikuwa na *Oversea Purchases Officers* katika nchi hii kwa miaka yote. Mzee Bishiri pale alikuwa Mkuu wa *Government Store* wa kwanza toka uhuru anafanya ununuzi wa nje na wa ndani. Kwenye Shirika la Umma unakuta kuna *Oversea Purchasing Officer* na *Local Purchasing Officer* na wamefanya kazi hii kwa miaka yote zaidi ya 40. Leo wanaambiwa hao wote ni watunza stoo sio wanunuzi. Kwa sababu tu suala la kujenga

barabara na ujenzi sasa limeingizwa kwenye ununuzi, basi inafanya kwamba wanunuzi wote waliokuwepo hawajui kitu ni watu wa *stores* tu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kilichobadilika ni kwamba teknolojia imebadilika. La pili, kilichobadilika ni kwamba ujenzi wa barabara na majenzi mengine sasa yameingizwa kwenye ununuzi basi lakini si kusema kwamba ununuzi ulikuwa haupo na kwa hiyo kama kuna Bodi ya Ununuzi hii hatuitambui labda hiyo Bodi ya *Stores.*

Lakini nashukuru kwamba kwa miaka mitatu yote hii ukiacha Ubunge wangu nimekuwa nikipigania suala hili na limeeleweka sasa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nadhani kwamba tukishakubali kwamba hii ni taaluma na wale wataalamu tuelekeze nguvu zetu katika kuwajenga. Hii sheria iko Wizara ya Fedha na ndiyo itapata fedha nyingi za *Capacity Building* katika sheria hii. Lakini nina wasiwasi kwamba wale watendaji wanunuzi walioko Wizara ya Ujenzi wanaweza kuachwa kwenye mataa kwa sababu hawako kwenye ile Wizara. Sasa na Bodi inayohusika inaweza kuachwa vilevile kwenye mataa, bodi ambayo inahusika kuwajenga wataalamu. Lazima tuangalie kwamba sheria hii na kanuni zake zilenge kuwajenga hao wataalamu wa ununuzi kwa namna ambavyo itakuwa imewekwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nieleze kwamba katika vifungu mimi nimeridhika kwa sababu nimefuatilia toka mwanzo mpaka mwisho na vitu vingine tumebadilisha jana jioni, namshukuru sana Waziri wa Fedha kutilia hilo maanani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, isipokuwa niseme hapa waziwazi kwamba mwaka 2001 baada ya kupitishwa sheria ile ya kwanza kilichokuja kuharibu zaidi ni zile kanuni ambazo zilikuja kutungwa na Waziri na hazikuangaliwa kwa makini na wadau walio wengi na kwa bahati mbaya kanuni haziji Bungeni. Mimi naomba nitoe rai kwamba kanuni zitakazo tengenezwa kufuatia muswada huu Wabunge kwa maana angalau ya kamati ya fedha, kamati ya *PSE* na ya *LAAC* wao wasiwashirikishe kama wadau. Tunajua kanuni huwa haziji Bungeni washirikishwe kwa muda mrefu ili waweze kuboresha na wadau wengine wote ambao wako nje ya bunge kwa sababu ni zile kanunu zilizopitishwa haraka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kulikuwa na wadau wengine tulishiriki lakini tulikusanywa kusanywa pale Dar es Salaam siku moja mbili kanuni zikapita na ndiyo mambo yakawa mabaya sana kutokana na kanuni. Kinacho haribu ni kanuni mara nyingi sheria inaweza kuwa siyo mbaya sana hata ile sheria haikuwa mbaya ukiacha ile *break us* iliyokuwepo. Lakini kanuni zilizotengenezwa ndiyo zinaleta matatizo. Kwa hiyo, mimi nimalizie kwa kusema kwamba hizo kanuni zishirikishe wadau wengi na baadhi Wabunge kwa maana ya Kamati hizo tatu washirikishwe ili zitungwe kanuni ambazo zitasaidia nchi hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo mimi nakushukuru sana na naunga mkono hoja.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Sasa nitamwita Mheshimiwa Dr.William F. Shija, atafuatiwa na Mheshimiwa Aggrey D. J. Mwanri.

**MHE: DR. WILLIAM F. SHIJA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii ili na mimi nichangie muswada wa kuanzisha mamlaka ya udhibiti wa manunuzi ya umma. Mimi nakubaliana na yale aliyoyasema Mheshimiwa Waziri na nampongeza na hayo aliyoyasema Mheshimiwa Waziri yameonekana wazi kabisa kwamba yametokana na michango ya wadau mbalimbali. Kwa hiyo nampongeza kwa kuja na sheria ambayo tunaweza tukaipa asilimia kubwa kuwa ni sheria sahihi.

Lakini vile vile wamenitia moyo wenzangu wa Kamati ya Fedha na Uchumi wakati wamewasilisha maoni ya Kamati kwa kuonyesha kwamba baada ya kukusanya mawazo yote kutoka kwa wadau na wao wenyewe kama wajumbe wa kamati wameweza kuusaidia muswada huu uwe ni muswada bora ambao tunaweza tukautumia Watanzania katika sura zetu mbalimbali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda niseme tu kwa ujumla kwamba kuna mfumo wa sheria ambao tumeanza kutengeneza nao niwakuanzisha mamlaka hizi. Hii ni sheria moja wapo ya mamlaka ya udhibiti wa manunuzi. Hapo nyuma Bunge hili Mheshimiwa Mwenyekiti tumepitisha sheria zingine za kuanzisha mamlaka zingine za udhibiti sasa nianzie pale alipokomea Mheshimiwa Makongoro Mahanga kwamba tunaweza tukatunga sheria nzuri lakini tukafanya kuanzisha mashirika mengine ya umma kupitia sheria hizo tukawa tunasura ile ile ya mashirika ya umma ambako tuna toka kwa sababu ufuatiliaji wa utekelezaji wa sheria hizo ukawa bado ni duni.

Kwa hiyo napenda nishauri kwa Serikali kwa ujumla kwamba tunapotengeneza sheria hizi kwa sura hii mpya basi tuangalie namna tunavyotekeleza ili tusije tukaangukia kwenye sura ya kuanzisha mashirika ya umma kwa namna nyingine. Nina zungumza hivyo kwa sababu hivi sasa tumeona hivi karibuni jinsi ambavyo kelele zimetokea kwenye vyombo vya habari juu ya makusudi ambayo hayajafika rasmi Bungeni yakubadili sheria ya mamlaka fulani na kuingiza vipengele ambavyo vitatupa matatizo katika msingi tuliojiwekea nao ni msingi wa kwamba Watanzania wengi zaidi ndiyo washike hatamu ya uchumi wa nchi yao.

Sasa hilo tutalizungumza kwa wakati huo mimi sasa hivi napenda nikushauri tu kwamba tujitahidi katika utekelezaji kwa kuweka kanuni zetu tusije tukaangukia tena kwenye mfumo wa kuanzisha mashirika ya umma. Nnasema hivyo kwa sababu Mheshimiwa Mwenyekiti, Waziri ametusaidia kwamba ni asilimia 70 au chini kidogo ya Bajeti ya Serikali inatumika katika manunuzi na sote tunashuhudia Watanzania jinsi tunavyonunu mali mbalimbali katika Halmashauri zetu, katika Serikali kuu na katika ofisi mbalimbali za Serikali tunashuhudia tunavyonunua mali.

Mheshimiwa Rais alikwisha tuambia, alikwisha tupa muongozo tangu mwaka 1995 kwamba mambo makubwa ambayo tungeshughulikia ni kwa kuhakikisha tunapiga vita rushwa tuhakikishe kwamba tunakuwa Watanzania wenye nidhamu tujitahidi

kukusanya kodi na tuendeshe mambo yetu kwa utaratibu wa sheria hayo ndiyo mambo manne ambayo Mheshimiwa Rais wetu William Benjamini Mkapa aliyotoa kama muongozo mwaka 1995 wakati anaanza utawala wake na maelekezo haya yalikuwa maelekezo sahihi kabisa Mheshimiwa Mwenyekiti kwa sababu leo haya mambo tunayohangaika nayo kupitia taarifa ya Mkaguzi Mkuu wa Serikali na taarifa zingine zinazotufikia hapa Bungeni kupitia kamati zetu zinaonyesha kwamba hatujapiga vita rushwa vya kutosha na bado hatuna nidhamu Watanzania ya kutosha. *(Makofi)*

Hilo ni lazima tukubaliane ili kusudi tujisahihishe na baba wa taifa hayati Mwalimu Julius Nyerere alisema katika wakati wake kwamba kama binadamu hukubalia kujisahihisha basi wewe utastukia una tumbukia shimoni na kwa sababu alivyosema Dr. Makongoro Mahanga hali ya dunia inazidi kutuelekeza mahali ambapo Waafrika tutafika mahali hatufanyi tena mambo yetu bali tunafanya mambo ya wengine sisi tunakuwa kama wakala tu. Tunachotafuta ni kilekile ambacho Mheshimiwa Waziri amejaribu kukisema kwenye hotuba yake ni sisi wenyewe Watanzania au Wakenya au Waganda au Waafrika wengine tushirikiane ili tuweze kufanya mambo yetu sisi wenyewe kikamilifu bila ya kuingia katika sura ya kuwa maboi wa watu wengine. *(Makofi)*

Kwa hiyo, lazima tujisahihishe lazima tuondoe kasoro lazima tushughulike na madhara kama ya rushwa hasa kupitia njia hizi za manunuzi kwa sababu ndiyo kuna fedha nyingi hapo ndipo tutawasaidia Watanzania wengi walio vijijini wasio jua tunalofanya hapa Bungeni ambao wanategemea Hekima zetu ili taifa letu liwezekuishi miaka mingi na karne nyingi zijazo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo kwa kweli inasikitisha tumeingia kwenye dunia gani ambapo watoto wetu wanapenda na baadhi ya wazazi labda kuiba mitihani kuliko kuuendea mitihani kwa usahihi kama ambavyo wengi tulifanya miaka ya nyuma. Leo tunaangalia namna gani katika kutazama ni mali zipi tunazinunua ambazo si za gharama kiasi cha kufirisi katika maeneo yetu ya mapato. Tunanunua mali gani lazima tujiulize na tujisahihishe haiwezekani katika nchi zinazoendelea tuwe tunakwenda na *business as usual* mnakwenda kununua mali za gharama kubwa wakati mna wananchi wenzenu vijijini ambao bado hawajapata maslahi ya taifa lazima tujiulize na lazima tujisahihishe. *(Makofi)*

Sasa tabia hizi za rushwa sote tunaambizana mara kwa mara tunakumbushana ni binadamu tuko duniani hapa na dunia Mheshimiwa Mwenyekiti imejaa watu wa sura mbili tu. Sura ya kwanza ya binadamu ni wale wanaopenda faida na kula haraka haraka. Kundi la pili Mheshimiwa Mwenyekiti ni wale wanaopenda kutoa huduma. ukitizama vitabu vya falsafa vitakwambia tuna makundi ya binadamu duniani nchi zilizoendelea na nchi zinazoendelea ya sura mbili hizo tu. Sasa sisi Tanzania na Waafrika nadhani lazima tujihadhari kukaa na watu wengi wenye kundi la kutaka kutoa huduma kuliko kupata faida.

Mheshimiwa Mwenyekiti inapokuja kwenye manunuzi tunashuhudia baadhi ya wale tuliowapa kazi za utendaji wanakimbilia kuwa wanataka faida wanataka kula na udhibiti wake unakuwa mgumu sana kwa sababu kama udhibiti uko sehemu yake iko

hapa Bungeni mpaka tunakuja kupata taarifa hapa Bungeni watu wamekwisha tafuna. Nasema lazima tutafute namna ya kusahihishana Watanzania ili kusudi tusije tukawa na rundo la watekelezaji wengi ambao wako kwenye kundi la watafuta faida. Hao wanaitwa utilitarian kiingereza na wale wanaopenda kutoa huduma ni deontologists kwa kiingereza.

Makundi haya ndiyo yale ambayo tunayaona hata kutoka kwenye nchi zilizoendelea zinazotupa misaada aliyowazungumza Mheshimiwa Dr. Makongoro Mahanga ni wale wanaokimbilia kuja nchi zinazoendelea kuja kusema lazima tutapata faida sasa hawa mkiwapata lazima kuwasimamia vizuri iwe kwenye uwekezaji iwe kwenye ubinafsishaji ili faida ibaki kwenu wasije wakaitoa yote na duniani tunawindana hivyo kwamba yule maskini ikiwezekana awe maskini zaidi hasa Mwafrika na yule ambaye anamapato apate mapato makubwa zaidi.

Sasa sisi lazima tuunde ujamaa wa namna yetu wala tusikumbwe na dhana na falsafa ya uchumi huria *market economy* tukaenda nayo tu hivyo holela tutajikuta tumewaacha wananchi wengi sana nyuma na sisi tukawa viongozi peke yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lazima tujisahihishe. Sasa nije eneo la pili linalosema kwamba tuna matatizo makubwa sisi waswahili ya kutokuwa na utamaduni wa matengenezo ya vitu mbalimbali tunavyonunua. Hatuna utamaduni wa matengenezo utaona mara nyingi tunaponunua kitu, kitu cha kwanza kutelekezwa ni ile taarifa juu ya kitu kile. Hata itakapofikia kwamba kitu kile kinatakiwa kutengenezwa iwe ni *microphone* iwe ni *camera* iwe chombo gani kiwe ni gari hatakuta fundi hakuna taarifa hiyo ya kitaalam ambayo itamsaidia kuweza kutengeneza kitu hicho kwa kiingereza Mheshimiwa Mwenyekiti *the culture of maintenance must come to us finally au eventually* hatuwezi kuendelea kuwa tunajiachia achia tu kwa sababu pamoja na manunuzi lakini ni mali nyingi sana kila mwaka.

Mheshimiwa Mwenyekiti tunazipoteza kwa sababu tumejitia kama hatujali juu ya kutengeneza vitu tunavyonunua. *The culture of maintenance is a absolutely lacking* na nilipozungumza pamoja na kamati yangu na Mkurugenzi Mkazi wa Shirika la Sayansi Elimu na Utamaduni *UNESCO* hapa nchini alitueleza kwa kusitisha kwamba sisi Tanzania hapa tunajikokota kokota sana juu ya kuwa na utamaduni wa kutengeneza vitu vyetu kabla havija haribika kwa maana nyingine hatujali magari ya Serikali ni magari tu dereva anachukua gari utamkuta hapa nje amefungua *air condition* eti amekaa mle ndani Waziri akija asione joto, koroo gari inalia inatumia mafuta lakini maana yake *wear and tear* yake inamaliza gari hilo.Tumeona mifano hiyo ya kitoto kabisa nasema *culture of maintenance* Mheshimiwa Mwenyekiti lazima tuizingatie. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, la mwisho ambalo wenzangu wameligusia lakini na mimi sina budi nilitie mkazo nashukuru sana Mheshimiwa Waziri amezungumzia juu ya umuhimu wa kuweka unit ndogo ndogo ili *tender* hizi ziende kwa wafanyabiashara wadogo wadogo wa kwetu Wazalendo waliozaliwa nchi hii waache kusema wazawa, waliozaliwa nchi hii na wana maslahi nayo na lazima wapate sehemu kubwa ya mafao ya nchi yao.*( Makofi)*

Hawa ni small tenderize ambao lazima tuwawekee utaratibu hata kama kwa kanuni makusudi kabisa wapewe. Tuna taarifa ambazo pengine si za kweli kwamba katika mambo ya *tender* au zabuni wamekuwa karibu wafanyabiashara kumi tu nchi hii ndiyo wamekuwa wakipewa zabuni kwa makampuni mbalimbali wanachanganya. Sisi hatukuzaliwa kwenye biashara hatuna uzoefu huo lakini zipo tuhuma za namna hiyo ambazo tunakumbana nazo mitaani zinasema Waheshimiwa Wabunge tusaidieni katika zabuni hizi wengine wadogo wadogo hatupati leo Mheshimiwa Waziri amenifurahisha sana kwa sababu amelijibu hilo lakini mwisho kabisa ni suala la Halmashauri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Halmashauri tuzisaidie, kule kwenye Halmashauri tunawapelekea fedha nyingi sana ambazo hawana uwezo nazo bado kitaaluma na kwa tamaa. Ndiyo maana kamati ya fedha na uchumi imezingatia namna tutakavyoteua Wakurugenzi wale kwenye bodi za zabuni mimi nakubaliana na marekebisho hayo lakini nasema lazima tuwe na mechanism. Labda ya kila miezi mitatu au miezi minne tupate taarifa ni nini wamefanya kwa Halmashauri ili tuwasaidie. *(Makofi)*

Fedha walizonazo ni nyingi na nyingi Mwenyekiti zinafujwa kupitia manunuzi ambayo yanafanyika sasa si zote lakini baadhi nyingi ukifanya takwimu unaweza ukapata pengine nyingi. Sisi tunasema ni lazima tuzisaidie Halmashauri zetu ambazo tunazipelekea mali ya nchi kuweza kutumia na ni lazima zitumie vizuri. Kusubiri tu taarifa ya *Controller the Auditor General* na kusubiri kamati ya Ndugu yangu Mheshimiwa Mgana Izumbe Msindai ifanyekazi haitoshi. Bunge hili lazima liwe na taratibu siku zijazo la kuangalia kila *quarter* ya mwaka tumepata taarifa gani ya manunuzi na fedha hizo zimetumiwa namna gani. Kama vile taarifa ya Kamati teule ya Mheshimiwa Omar S. Kwaangw' ilivyopelekwa kutizama fedha za MMEM.

Mheshimiwa Mwenyekiti, huo ni utaratibu mzuri ili kusudi tusaidiane maana tumegawanyika kati ya fungu la wanaopenda kula na wale wanaopenda kutoa huduma. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hivyo, kweli kabisa naunga mkono hoja hii na namtakia Waziri kila la heri atuarifu mara kwa mara hapa Bungeni juu ya utekelezaji. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Anayefuata ni Mheshimiwa Aggrey D. J. Mwanri, halafu atamalizia na Mheshimiwa Philip S. Marmo.

**MHE. AGGREY D. J. MWANRI:** Nakushukuru Mwenyekiti kwa kunipa nafasi na mimi niweze kuchangia katika muswada huu. Ninaomba awali ya yote ni mpongeze sana Mheshimiwa Waziri kwa *presentation* nzuri ambayo imefanyika hapa. Ninataka nikiri jambo moja Mwenyekiti kwamba mimi ni mjumbe wa *Public Accounts Committee* na kama alivyosema Dr. Milton M. Mahanga tulipata nafasi kutoka Dar es Salaam ya kwenda katika Kamati zile na semina.

Ninalotaka nikuthibitishie Mwenyekiti kwamba katika *Public Hearing* ambayo imefanyika hapa Bungeni nimeshiriki na tumefuatilia vipengele vyote vile ambavyo tulikuwa na dukuduku navyo na mimi nataka nitamke hapa kwamba *it is my judgment as a Member of Parliament* kwamba vipengele vyote ambavyo vilikuwa vinaleta utata katika Muswada huu vimekuwa *included.* Nitakalo waambia Wabunge wenzangu kwamba hakuna haja ya kuumiza kichwa hapa Muswada huu umezingatia mambo yale. Mtakapo angalia mambo *in a historical perspective* tunataka kuangalia mambo kihistoria ukiangalia mambo kihistoria unakuwa *scientific* na tuliyasema haya mambo hapa. Wako watu wanafikiri kwamba hakuna uhusiano kati ya muswada ule uliyopita *The National Empowerment* na huu muswada tunao uzungumzia hapa *there is a direct relationship* kati ya Muswada ule na Muswada huu.

Nchi hii tumesema ya kijamaa nchi imetawaliwa nchi changa juzi ilikuwa inakwambia hapa huruhusiwi kuwa na mishahara miwili huruhusiwi kuwa na nyumba ya kupanga huruhusiwi kuwa Mkurugenzi katika shirika lolote la umma au la *private* umejenga wewe *class* ya watu ambao *eventually* uwezo wao ni mdogo. Unazungumza habari ya sekta binafsi katika Tanzania ambayo ni juzi juzi tu imeanza unaileta hapa.

Leo wanakuja watu *World Bank, IMF,* Waingereza, Wamarekani wanakwambia fungua kila kitu halafu hawa watu wako waambie mkimbie wote mtimke wote watarudi hao wanaweza wakakiambia chama chao wakaiambia Serikali yao kwa hivyo basi unahaja ya kunifidia mimi nilikuwa mtiifu sikuwa na nyumba ya kupanga, mimi nilikuwa mtiifu sikuwa na mishahara miwili, mimi nilikuwa sikushiriki katika shirika lolote lile ndivyo ilivyokuwa inasema.

Leo *all of a sudden* wanasema hivi mimi anayekuja mwenye uwezo ndiyo achukue *no way,* na muswada huu ndicho unachoangalia *no way. America is for Americans, China is for Chinese, Tanzania is for Tanzanians. (Makofi)*

Lazima uiseme waziwazi wala bila kuionea aibu yoyote useme hivi mimi hii barabara inajengwa upendeleo wa kwanza natoa kwa Mtanzania ukiniuliza kwa nini umempa nampa kwa sababu ni Mtanzania nasema hivyo. *(Makofi)*

Mimi siingii kwenye ile nyingine Mtanzania wa namna gani chama changu kilishatoa msimamo na mimi ni mtu mtiifu. Lakini ukiniuliza unasema waziwazi mimi huyu nimempa kwa sababu ni Mtanzania. Waarabu ndivyo wanavyofanya, Wamarekani ndivyo wanavyofanya, Dunia nzima ndivyo inavyofanya. Ukija hapa kwetu unaambiwa unajua sisi tumeingia kwenye soko huria *the law of demand and supply* tunatakiwa tutimke *the law of competition, the law of value* ndivyo tunavyofanya kazi sasa na nyinyi tutawashangaa no way. Lazima ufike mahali useme hivi hawa Watanzania ambao huko nyuma wali walikuwa nyuma nitawashika mkono nitawapeleka kama mtoto mdogo unavyomkatisha barabara kwenda ng'ambo ya pili asigongwe na magari.

Ndivyo unavyompeleka, tukisema hivyo na mtu akatushangaa sisi tutamshangaa unatushanga nini,tutamshangaa. Wanasema tunafanyaje sasa mimi sikuwa na mtaji nifanyeje, niende nikabamize watu ntaanzisha biashara ya utumwa mpya. Nitakwenda

mimi nikauze watu ntakwenda kulimisha watu miwa saa hizi utakachofanya hapo utasema hivi pesa ya Serikali inaingia kwenye Bajeti inapotoka huwezi kwenda kuwagaia watu hivi unawapa bure tu hivi hivi. Unasema jamani kuna mradi unakuja hapa ninataka ninyi mchukue hii kitu unasema Mahanga wewe mimi nakuona una akili nzuri ya biashara unasema kwa hiyo mimi nitakupa kazi hii uende ukafanye unaisimamia.

Serikali inakuwa ni *guarantor* inawa-*guarantee* watu wake inawadhamini inasimamia ndivyo walivyofanya kule Uchina ndivyo walivyofanya kule Japan. Hawa wakina *Toyota,* hawa wakina *Suzuki,* hawa wakina Kawasaki, unavyowasikia majina haya waliweka ndani ya *Government Budget* wakasema mimi naweka Bajeti hii hapa ili kuwanyanyua hawa na kuwachukua. Wale wakina *Hyundai, the Hyundai family* ile Serikali ilikwenda ikaweka msuli wake pale ndani hivi ikawasimamia. Ukifanya hivyo siyo kwamba uta-*scare* wataudhika hao lakini wanaudhika kwa sababu wewe unataka kujenga kada yako ambayo *eventually* unachotaka katika miswada yote hii ni kuwa-*empower* Watanzania. *(Makofi)*

Ndicho unachofanya misaada yote inayoletwa hapa ndani kama haifanyi kazi ya kuwawezesha Watanzania haina maana, mimi nikipiga kelele hapa kama kelele hii haiwasaidii watu wangu wa Siha *this is a useless case. (Makofi)*

Nataka niione *one to one function* kati ya muswada huu na *development* ya watu wangu wa Siha, nione barabara zinatengenezwa kule na wanaotengeneza kule ni wananchi wa jimbo la Siha, vibarua wanaofanya kule ni vibarua kutoka Siha, wanaochukua ukarandarasi kule ni watu kutoka Siha. Nakwambia sawa barabara hii kidumu Chama Cha Mapinduzi mambo yanakwenda vizuri.*(Makofi)*

Nataka kusema nini, Waziri wa Fedha, Waziri Mkuu, Serikali na Wabunge wenzangu suala la kuwa-*empower* Watanzania tusilionee haya hata kidogo. Mimi juzi sikuzungumza hapa lakini nilijua kuna mahali pake tu, nitakuja kupasema hapa pako wazi. Muswada huu umefanya nini, muswada huu umetamkwa humu ndani na vipengele vimesomwa hapa na Waziri wa Fedha amesema kwamba tutawapa *preference* tutawaangalia tutawasaidia. Nenda Marekani, Marekani wakikupa mahindi ukiwaambia mimi nina mtu amenisaidia meli ya kupeleka pale wanakataa wanakwambia meli itakayapeleka hapa mahindi Tanzania ambayo tumekupa sisi ni ya wa Marekani ndiyo watakao peleka pale ndivyo wanavyofanya wenzetu. Sisi hapa tuna *assets* unazitengeneza *classes* zinatengenezwa kutoka kwenye *production level, classes* hazitengenezwi hapo juu. Mfumo wa kibepari ni mfumo ambao ndani yake unakahuni tulikuwa tunasema ni unyama ni sawasawa na kumruhusu binti yako aingie kwenye baa yatakayo tokea kule akifanyabiashara mle wewe utajijua. *(Kicheko)*

Utaweka *controls* ndiyo lazima utume mke wako aende saa nne akamchukue binti ampeleke nyumbani, lakini ukisharuhusu ameingia kwenye mfumo wa kwenda kuuza baa pale basi tena. Lakini unasaidia mama saa nne ukamchukue mtoto binti yule huna hakika sana na ule mfumo. Kwa hiyo, unakwenda nao ukiyumba hivi na wewe unayumba nao unakwenda nao. Huu mfumo huu katika *level* ya *production* watu wote tajiri na maskini

wote wanazalisha, ule mfumo ule wa kibepari ni *social* katika *character* yake. Mfumo ule unakuja ku-*bore* inapokuja kwenye suala la kugawana mapato.

Hapa katika *distribution* ndiyo mtu mmoja anachukua mmoja hapa ninyi wengine mnaachwa mmesambaa barabarani mnaachwa hapo. Lakini mfumo wa kijamaa ule mtazalisha wote mtagawa wote mtakwenda wote. Sasa sitaki kusema mambo ya kijamaa hapa kwa unalotakiwa hapa kichaa uongee mambo ya ujamaa hapo utapata matatizo sasa kwa sababu ni matatizo. Nataka niseme hivi muswada huu namba mbili yake ulikuwa na tatizo la urasimu, na urasimu ndiyo takataka zote na mambo yote yaliingia humu ndani.

Mimi nakumbuka kuna wakati barabara ilikuwa inajengwa katika jimbo langu mwaka, ooh, mmekosea jinsi ya kutenda, ooh lazima *central board* ipitishe, ooh sijui ifanye nini. Leo Serikali imekuja hapa na Muswada ambao unaondoa urasimu huo. Unatoa nafasi kwa Idara mbalimbali za Serikali katika Halmashauri na vyombo vingine ambavyo ni vya umma vifanye maamuzi haya bila kuhitaji kufanya *reference* kubwa kule juu. Sasa sisi tunakataa nini hapa. *(Makofi)*

Kama Halmashauri zetu zinakuwa emmpowered tunakataa nini, habari ya kwamba hii sheria ilikuwa hivi tulisema *is not an issue*. Nilipokuwa darasa la saba nilikuwa nasema hivi kazi ya Bunge ni kutunga sheria kama tukifika mahali hata huu tukafika kule mbele ya safari tukaona unamatatizo tutarudi hapa ndani tuombe Mungu tu mambo yaende vizuri huko mbele ya safari tunarudi hapa tena tunakuja kupitisha muswada mwingine. Kwa hiyo, mimi hapa kwenye suala hili mimi nimeweka tiki, namba nne *problem* yake ilikuwa ni nini ngiri, sisi tulikuwa tunakaa tunaangalia suala la *accounts* tunza mahesabu ya Serikali hakikisha hesabu zote zimekaa vizuri tukasahau kwamba wizi huo unabadilika sura yake ukiona unabanwa sana kwenye mahesabu unahamia kwenye manunuzi unaweka ma-*computer* pale hewa hayakununuliwa unakwenda unayaiba unakwenda kuyauza.

Unasema barabara imetengenezwa hapa kwamba mtu ametengeneza barabara pesa imeongoka wenzetu siku hizi wamekwenda *further than that* wanaweka zaidi udhibiti katika manunuzi na katika *store* na namna ya kutunza mahesabu katika *Book-Keeping* ndicho wanachofanya nyinyi mnabaki hapa mnaangalia pesa mnatunza mnaona vizuri *clean certificate,* amepata *clean certificate.* Wenzake wanakwenda kuziibia kule kwenye manunuzi ndiko wanakwenda kule, anamwambia kwamba wewe andika kwamba ulileta kabichi gunia ishirini, kumbe alileta kabichi gunia mbili. Muswada huu unaziba huo mwanya unakataa sasa hakutatokea jambo la namna hiyo.

Sisi tunasema hivi Bunge hili lilitoka hapa linajivuna kwamba hii ni *development* kubwa kama leo unaweza uka-*empower* Tanzania leo unaweza ukadhibiti leo unaweza uka-*create an count-ability* leo unaweza ukasimamia kiasi hiki mimi nadhani ni jambo la kujivunia na hii tukasema hivi tunatembea kifua mbele hata nikirudi jimboni wananiuliza vipi, namwambia vipi sisi tumepitisha sheria ambao tunajua kwamba itawa-*empower* Watanzania sheria ambayo tunajua kwamba itadhibiti. Lakini huishii hapo wanasema hizi *modes of production* wakina Takahashi, Takashiro Wakina Mozirisidob wanazungumza hii habari *it can change in form but in content* ikabakia vile vile.

Inaweza ikabadilika katika sura yake hivi lakini maudhui yake yakabakia pale pale. kwani si unaweza ukaandika *keep left* hapa watu waka-*keep right,* unaweza ukaandika *keep left* lakini watu wakapita huko na ndiyo maana unakuta magari yamegongana, watoto wamegongwa, mtoto amepasuka kichwa ni kwa sababu kuna watu ambao wanavuruga hiyo. Unaweza ukasema hivi kuna sheria ya kuzuia watoto wasipigwe mimba wa shule lakini unakuta watoto kila siku wanazalishwa hapo, *problem* yake ni nini. *Problem* yake hakuna udhibiti na usimamizi wa sheria ambazo tunazipitisha katika nchi yetu.

*Argument* yangu haitoshi tu kusema hapa tumepitisha muswada wa *procurement act* ya 2004 halafu tukaishia hapo tumeweka kada ya namna gani katika maeneo yetu ya udhibiti. Unapobadilisha mambo haya lazima uweke na pumzi mpya ndani ya hao watu wanaosimamia kitu hiki, lazima uweke kada mpya, lazima ufike mahali Mheshimiwa Waziri wa fedha uwape majukumu mapya useme majukumu yale ya zamani achana nayo. Tunayo kada hiyo tunao watu ambao wanatembea kifua mbele Wahindi wanatembea dunia nzima lakini ndani ya moyo wake anayo India, Wachina wanatembea dunia nzima lakini ndani ya moyo wake kuna China, Wajapan watazunguka kila mahali lakini ndani yake wanazungumza habari ya Japan.

Je, muswada huu tumefika mahali ambapo tunao Watanzania ambao akilala usiku akiamka anayo Tanzania ndani ya moyo wake? Ukishatengeneza hiyo kada na hiya *attitude* kwa hiyo suala hapa siyo suala la kupiga sheria ni suala pia la kubadilisha *the attitude na mind set* ya watu. Huu ndiyo mchango wangu, mimi nimeomba kuzungumza hapa Mwenyekiti, naomba tuwa-*empower* watu wangu, na ninaomba tupewe nafasi na kwenda kwenye Halmashauri ya Wilaya ya Hai kule Siha ntawaambia kwamba sasa tunaouwezo wa kupitisha maamuzi hapa ya kupata matenda na vitu vingine bila kuhitaji ku-*refer* kwenye *center.* Lakini jambo hili utahitaji kujenga kada maalum ambayo itafanya kazi hiyo. Baada ya kusema maneno haya kwa niaba ya wananchi wa jimbo la langu la Siha napenda kutamka hapa kwamba mimi naunga mkono hoja hii ulionipa. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Philip S. Marmo

**MHE. PHILIP S. MARMO:** Ahsante sana Ndugu Mwenyekiti kwa kunipa nafasi hii ili na mimi nitoe mchango wangu wa mawazo katika muswada uliyoko mbele yetu. Waheshimiwa wenye uwezo mkubwa sana wa kujieleza na kutafakari muswada huu wamenitangulia na mimi nitajitahidi kwa uwezo wangu wote nisirejee yale ambayo wameyasemea.

Mimi ni mmojawapo ambao nilikuwa nakerwa sana na Sheria ya Manunuzi ya Umma ya Mwaka 2001. Tulitoa rai yetu nyakati mbalimbali ikiwa ni pamoja na nyakati ya Bajeti. Ilifikia mahali ambapo tulidhani hivi *Air Tanzania* ingelikuwa bado ni Shirika la Umma kwa kuwa na sera ile si safari zote zingevunjika kwa sababu vipuri vikiagizwa kwa bei ghali namna ile itabidi *Tender Boards* zikae kwa taratibu zinazozifahamu. Wakati mwingine hata ukigharamia vikao vyao bado hawatakubali kukaa. Kwa hiyo

tulikuwa tumerejeshwa katika enzi ambazo kwa kweli hazielezeki kwa ajili ya ile sheria na sheria ndogo aliyeitunga Waziri.

Sasa hivi marekebisho haya kwa kweli yanakidhi haja kwa kiasi kikubwa. Lakini bado kuna maswali machache na ni mazito. Ukiangalia sheria hii kama ilivyo sheria nyingi siku hizi inaunda vyombo vingi sana hasa hii imeleta vyombo vingi sana. Ni kana kwamba watu wanataka kuajiri watu wao hapa. Sheria inaanzisha Mamlaka ya Udhibiti wa Manunuzi ya Umma *(Public Procurement Regulatory Authority),* kama kawaida kutakuwa na Bodi za Tenda, kutakuwa na Kitengo cha Kusimamia Manunuzi *(Procurement Management Unit),* kutakuwa na Mamlaka ya Kusuluhisha Migogoro ya Ununuzi *(Public Procurement Appeal Authority).* Hii yote ni ajira. Ebu jiulize vyombo hivi vyote ni vya lazima?

Mamlaka ya Udhibiti wa Manunuzi kwa hali ya hivi sasa inaweza ikatetewa. Bodi lazima ziwepo. Kitengo hiki cha Ununuzi ni cha lazima. Pengine Waziri angetueleza ni cha lazima kweli? Mamlaka ya Kusuluhisha Mgogoro wa Ununuzi. Hivi mwaka mzima wazabuni wangapi wanaleta migogoro mpaka tunatunga sheria ya kuunda kamahakama kadogo hivi kama hamna migogoro uliotokea maana ukiomba tenda ukashindwa unaomba tenda nyingine ya nini muda tena kwenda kutafuta mgogoro au wakikaa tu watakuja kutafuta migogoro baadaye. Tuna Mahakama lakini pia tuna vyama vyetu vya wataalamu wa sekta mbalimbali tena vilivyobobea ikiwa ni pamoja na Chama cha Usuluhishi cha *Tanzania Tanzania Arbitration Association* ambayo ina Majaji waliostaafu waliobobea ambayo ina Wanasheria na Wahandisi waliobobea ambao wako tayari muda wote kusuluhisha bila urasimu wa kisheria na ambao kwa kweli wanahitaji kazi. Makampuni makubwa makubwa haya ambayo yanachukua zabuni hawapendi vyombo vya Serikali wanataka usuluhishi wa nje ya Mahakama. Sasa chombo hiki pia ni cha lazima hatuongezi urasimu ambao umetufikisha hapa kubadilisha sheria katika muda wa miaka miwili tu. Hilo ni moja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili ambalo nilitaka kulisemea hapa ni kuhusu uteuzi au namna ambavyo tunavyopata wajumbe wa Bodi za Tenda kupitia ngazi zote. Unaposema Mkuu wa Idara atateua Wakuu wa Idara wachache au Wakurugenzi wachache ambao wanaweza wakaunda *Tender Board* atatumia vigezo gani? Uwajibikaji katika hali hii utakuwaje. Tufikirie mahali kama Halmashauri ya Wilaya ambapo Mkurugenzi huyu sasa ana uwezo mkubwa sana kuliko hata Madiwani katika eneo hili na Wakuu wa Idara wanawajibika kwake. Hivyo akiwaagiza akitaka tu kuwa kichaa hatusemi wote wanaweza kuagiza wako zaidi ya mia moja, sasa mia moja huwezi kukosa mwenye dosari akaagiza nataka tenda hizi iwe hivi na hivi Mkuu wa Idara hivi atakataa?

Pili, zabuni hizi ni za aina nyingi sana hivi kwa nini tuseme tu kila wakati zabuni ikitokea tupate wa muda. Kama ni zabuni ya madawa basi tuwe na mtu wa Madawa katika Wilaya au Bwana Mganga. Kama ikiwa ni chakula huyu ni Bwana Kilimo. Kwa nini sheria isitoe hata *caution* kuwe na *co-opted members* badala ya kukazania kuwa na watu wa kukaa pale muda wote. Pengine Waziri angetuelezea hili pia.

Kuna hili ambalo wenzangu waliotangulia wamelisemea sana. Hivi kuna ulazima gani wa kusema kwamba katika zabuni zetu utashindanisha wazabuni wa ndani na wa nje. Hivi nani anatulazimisha kwamba tuseme hivyo, hivi ukikaa kimya lakini mtu mwenye sifa akijitokeza unampokea. Nani huyo analazimisha kwamba sheria kwamba lazima itaje kwamba lazima kuwe na ushindani kati ya wazabuni wa ndani na nje. Busara gani imetumika tufikie hapo. Sawa asilimia sio kubwa sana. Asilimia kubwa ya Bajeti yetu inatoka nje. Wametufikisha mahali hapa.

Mheshimiwa Waziri alipokuwa anasema Bajeti yake watu wa Afrika Mashariki walikuwa wanafuatilia sana Bajeti yake, Bajeti ya Kenya na Uganda. Lakini wale watafiti walioko nje makini hawakuwa wanafuatilia Tanzania au ya Uganda kwa sababu wanajua sehemu kubwa itakuwa ikitoka nje, walikuwa wanafuatilia Kenya ambayo kwa zaidi ya asilimia 69 wanajitegemea, wamenyimwa. Na wao wanakusanya trillion 4 bila shaka kama ninakumbuka au *trillion* moja na nusu. Kwa hali tuliyonayo kwa kasi ya uchumi wetu hatuwezi siku moja tukakusanya trillion 4 au 3 tukawa hatuna haja kubwa sana ya fedha nyingi kutoka nje. Hapo sasa dhana hii ina maana tena. Dhana hii ya kwamba wazabuni wa ndani na wa nje washindanishwe na wa nje nani atakuwa akitulazimisha tufanye hivyo.

Kuna *message* inataka kutoka nje ya hapa kwamba tumefikishwa mahali ambapo sio pazuri angalieni hapa nje kuna ukumbi wa Bunge unajengwa ni Wachina hawa na hizi ni fedha zetu. Ukiangalia watu wengi tuliokuwa nao ambao tunakutana nao mahotelini hapa ni Wachina na Wazungu. Ukisafiri kati ya hapa na Manyoni, Manyoni/Singida, Singida/Nzega kote huko mpaka Kyaka ni Wachina na Wajapan na watu wengine. Sasa tumewafundisha hata Watanzania nje ya Serikali. Mtu anataka kujenga hoteli yake pale Arusha anamtafuta mkandarasi Mchina. Mwekezaji anamtafuta mkandarasi kabila ipi? Sasa imekuwa saikolojia tumejenga jambo hatari sana kwamba Mtanzania, kuwa Mtanzania mwenyewe inakuwa ni kigezo cha kunyimwa zabuni na leo tumeweka kwenye sheria baada ya miaka mitatu hali ya uchumi ikiwa haueni itakuwaje? Hivyo nadhani mbele ya safari hali hii haitakuwa nzuri sana.Watanzania wachache sana wameweza kufanikiwa kupata zabuni nje ya mipaka yetu na kwa sababu hakuna nchi yenye sheria kama hii na pale ambapo wamefanikiwa zabuni kubwa kubwa kama *DRC* hapa au pengine Kenya, Uganda au *Mozambique* ni kwa kutumia uhusiano mwema wala sio sheria ya nchi ile.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninalotaka kusema hapa pengine hatuna la kufanya leo wenzetu pengine huko Serikalini wamelazimishwa na wafadhili tuwe na masharti kwenye sheria zetu ambayo yanatulazimisha mambo ambayo ni wazi hayana maslahi ya nchi moja kwa moja nchi na wananchi wowote moja kwa moja. Lakini lazima tuje siku moja tutasikia kwamba tuachane na hali hii mimi hii natoa tahadhari. Sheria ndogo aliyotunga Waziri ilileta matatizo makubwa sana na urasimu na miradi mingi imekwama kati ya mwaka wa fedha wa 2003/2004, ile iliyohamishwa toka mwaka 2004/2005 sasa hivi inakwama kwa sababu ya urasimu ule. Wahusika hawakujua sheria hii na usimamizi wake. Kwa hiyo la kwanza basi sheria ndogo ndogo itoke haraka ili miradi isikwame tena na fedha zisirejeshwe Serikalini au kwa wafadhili. Mamlaka ya Serikali za Mitaa ni zaidi ya mia moja mnazitumia mabilioni ya fedha katika miradi mbalimbali na mstakabali

wa miradi ya maendeleo kati ya sasa na mwaka ujao itategemea jinsi ambavyo tutakuwa na utaratibu na sheria ndogo ndogo inayofanana na hii ambayo pia itakuwa kwa mujibu wa Sheria za Serikali za Mitaa. Na hii kwa kweli inatakiwa itoke haraka iwezekanavyo ili miradi mingi isikwame. Miradi mingi imekwama na nina hakika uzoefu tuliopata miaka miwili iliyopita ni funzo tosha. Kwa hatua tuliyofikia haitakuwa busara sana kubishana juu ya sheria hii. Ninachoomba basi usimamizi wake na baadaye tunakokwenda uangalifu utumike zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo machache nasema naunga mkono sheria hii. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge kama tulivyosema asubuhi wale waliopewa nafasi ya kuchangia wanne wamemalizika na kwamba kesho tuna lengo la kumaliza Bunge kipindi cha asubuhi saa 7.00. Kwa hiyo, nitamwita Mheshimiwa Waziri atoe hoja ya kuahirisha Bunge.

## KUAHIRISHA BUNGE KABLA YA WAKATI WAKE

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (MHE. WILLIAM V. LUKUVI):** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mujibu wa Kanuni ya 21 (6) naomba Bunge lako Tukufu liahirishwe sasa dakika 15, kabla ya muda wake hadi kesho saa tatu asubuhi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa hoja.

**WAZIRI WA USHIRIKA NA MASOKO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naafiki.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*

## HOJA YA KAMATI

### Tamko la Kamati ya Bunge ya Maendeleo ya Jamii Kuhusu Katiba ya Shirikisho la Mpira wa Miguu *(TFF)* na Kutaka Ufafanuzi Utolewe na Waziri Mwenye Dhamana ya Michezo

**MHE. SOPHIA M. SIMBA - MWENYEKITI WA KAMATI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Kwa mujibu wa Kanuni za Bunge Kanuni Na. 21(9) Toleo la 2004, naomba kutoa Tamko la Kamati ya Bunge ya Maendeleo ya Jamii kuhusu Katiba ya Shirikisho la Mpira wa Miguu *(TFF)* nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Michezo katika nchi hii inaendeshwa kwa Mujibu wa Sheria ya Bunge Na. 12 ya Mwaka 1967 iliyoanzisha Baraza la Michezo la Taifa (BMT) na kama ilivyorekebishwa mwaka 1971. Sambamba na Sheria hiyo, michezo pia inaendeshwa kwa kufuata Sera ya Maendeleo ya Michezo ya Mwaka 1995.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mujibu wa sheria hiyo, Baraza la Michezo lina jukumu la kuratibu, kusimamia na kuendeleza michezo kwa kushirikiana na Vyama vya Michezo nchini Vyama vya Michezo nchini lazima vitambue hivyo. Hivyo basi, Katiba za Vyama vyote vya Michezo lazima zizingatie Sheria na Sera za Nchi zinazosimamia shughuli za michezo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, wale wote waliopewa dhamana ya kusimamia shughuli za michezo wanawajibika kufuata sheria, kanuni na taratibu zilizowekwa za kuendesha michezo nchini, badala ya kuongoza shughuli za michezo kwa misingi ya ushabiki na kupuuza chombo cha michezo kilichowekwa kisheria. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa miaka mingi, Baraza la Michezo la Taifa (BMT) limekuwa likiheshimiwa ipasavyo na kupata ushirikiano mkubwa sio kutoka kwa Vyama mbalimbali vya michezo bali pia kutoka kwa viongozi wa ngazi za juu wa michezo nchini isipokuwa Chama cha Mpira wa Miguu *(FAT). FAT* wameonyesha dharau na kutoliheshimu Baraza ikiwa ni pamoja na kukaidi baadhi ya maagizo yake halali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kwa muda mrefu Chama cha Mpira wa Miguu *(FAT)* kimekuwa kikiendesha shughuli zake kwa kutumia Katiba yenye mapungufu mengi. Aidha kuna wakati *FAT* iliendeshwa bila ya kuwa na Katiba, kwani katika uchaguzi wa *FAT* uliofanyika Arusha tarehe 31 Desemba 2001, Baraza liliwasisitiza viongozi waliochaguliwa wakati huo kuwa katika kipindi cha mwaka mmoja wahakikishe Katiba mpya ya *FAT* yenye kukidhi maendeleo ya Mpira wa Miguu inatayarishwa. Lakini *FAT* hawakutekeleza. Kutokana na kutokuwepo kwa Katiba na hata *FAT* kutozingatia kanuni walizojiwekea wenyewe, malumbano na migogoro mingi imeibuka na kudumaza mchezo wa Mpira Miguu nchini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata Katiba ya sasa ya *TFF* ina mapungufu mengi, yakiwemo:-

(i) Katiba ya sasa ya *TFF* kwenda kinyume na Katiba ya Nchi. *FIFA* yenyewe inatambua na kuthamini Katiba na Sheria za nchi wanachama kama ilivyo katika statute ya *FIFA,* a*rticle 12 (h).*

(ii) Katiba ya *TFF* inakiuka Sheria ya Bunge Na. 12 ya mwaka 1967, ambayo ilifanyiwa marekebisho mwaka 1971 kwa kutolitambua Baraza la Michezo la Taifa. Aidha, Katiba hiyo ya *TFF* haitambui jukumu la Waziri mwenye dhamana ya Michezo. Mtazamo wa Katiba ya *TFF* unatoa umuhimu zaidi kwa *FIFA* na kudharau Sheria, Sera, Kanuni na taratibu za jinsi michezo inavyoendeshwa nchini.

(iii) Kuna uwigo finyu wa uwakilishi katika Mkutano mkuu wa *TFF* na wadau muhimu wa Mpira wa Miguu wameachwa Kando. Aidha, wadau wakuu hawawakilishwi katika Kamati ya Utendaji, hasa ikitiliwa maanani kwamba hicho ndicho chombo kinachoongoza shughuli za siku hadi siku za mchezo wa mipira wa miguu nchini.

(iv) Katiba ya *TFF* inazungumzia kuwepo kwa Katibu Mkuu na Katibu Mkuu Msaidizi wa kuchaguliwa tofauti na mapendekezo na msisitizo wa *FIFA* wa kuwepo Katibu Mkuu wa kuajiriwa au kuteuliwa na *TFF* yenyewe au kuwepo kwa Afisa Mtendaji Mkuu *(CEO).*

Haya ni baadhi tu ya mapungufu yaliyomo ndani ya Katiba ya *TFF.* Mapungufu ni mengi. Mapungufu haya ndiyo yaliyo mlazimisha awali Msajili wa Vyama vya Michezo kukataa kuisajili Katiba ya *TFF* na kuamua kuirejesha kwa Wadau wa Mpira wa Miguu ili waijadili. Lakini la kushangaza Msajili huyo huyo akakubali kuisajili Katiba hiyo hiyo yenye mapungufu, tena bila ya Masharti. *(Makofi)*

Pamoja na mapungufu ya Katiba ya *TFF* na udhaifu wa chombo chenyewe *(TFF),* pamejitokeza hali ya kusikitisha ya Serikali yenyewe kupingana na Msajili wa Vyama Michezo na Baraza la Michezo, vyombo ambavyo ni vya Serikali vya Utekelezaji.

Baada ya kutafakari yote hayo, Kamati ya Bunge inatoa mapendekezo na maoni yafuatayo:-

(i) *TFF* ni Chama kilichosajiliwa na Sheria ya BMT, na kinawajibika kufuata Sheria na sera za Nchi. Kamwe *TFF* haiwezi kuachiwa kufanya shughuli zake kinyume na Sheria na Sera za nchi. *(Makofi)*

(ii) Kitendo cha Msajili wa Vyama vya Michezo kupitisha Katiba ya *TFF* ambayo ina mapungufu mengi yanayovunja Katiba, Sheria na Sera za Nchi, hakiwezi kuvumiliwa na kukubalika. Katiba hiyo ya *TFF* ni batili na kwa ajili hiyo lazima irekebishwe. *(Makofi)*

(iii) Kwa kuwa Katiba ya *TFF* imegundulika kuwa na mapungufu mengi, Kamati ya Bunge inasisitiza Wadau mbalimbali wapewe nafasi ya kuijadili na kufanya marekebisho yanayotakiwa ili kuifanya iwe bora kwa manufaa ya Maendeleo ya Mchezo wa Mpira wa miguu nchini. Kamati inaamini muda uliopo kati ya sasa na Desemba 31, 2004 unatosha kufanya marekebisho na hatimaye kufanyika kwa Uchaguzi Mkuu. Baadhi ya Wadau tunaoshauri washirikishwe ni:-

* Umoja wa Vilabu vya Mpira wa Miguu nchini;
* Chama cha Makocha wa Mpira wa Miguu Nchini;
* Chama cha Waamuzi wa Mpira wa Miguu;
* Chama cha Waandishi wa Habari (TASWA);
* Chama cha Madaktari wa Mpira wa Miguu;
* Mabaraza ya Michezo (Mikoa na Wilaya);
* Chama cha Wachezaji wa Mpira wa Miguu;
* Wafadhili na Wapenzi wa Mpira wa Miguu;
* Vyama vya Mpira wa Miguu - Mikoa; na
  Wilaya nchini, na kadhalika. *(Makofi)*

(iv) Kwa kuwa kimsingi *TFF* imekubali kufanyika kwa Mkutano Mkuu wa Kurekebisha Katiba kuhusiana na kipengele cha Katibu Mkuu wa Kuajiriwa, Kamati ya

Bunge inashauri Mkutano Mkuu huo pia ufanye marekebisho kama yatakavyopendekezwa na wadau mbalimbali, kama vile kupanua uwigo wa uwakilishi.

(v) Katika kuzingatia utawala bora unaozingatia sheria, Serikali haina budi kuthamini na kuheshimu vyombo vyake vya utekelezaji katika sekta ya Maendeleo ya Michezo nchini vilivyopo kisheria.

(vi) Kwa kuzingatia umuhimu wa suala hili Kamati ya Bunge, inaishauri Serikali ifanye kila jitihada kuiwezesha *TFF* kufanya Mkutano wa Marekebisho ya Katiba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati ya Maendeleo ya Jamii inashangazwa pia kuona viongozi wa Wizara wenye dhamana ya kusimamia Sheria na Sera ya michezo wamekaa kimya. Hatuna uhakika wanafanya hivyo kwa manufaa ya nani. Kutokana na mapungufu mengi ya Katiba ya *TFF,* ikiwa ni pamoja na kutowashirikisha Wadau muhimu, Kamati inaitaka Serikali kuhakikisha kuwa Katiba ya *TFF* inajadiliwa na Wadau wote ili ifanyiwe marekebisho yanayostahili kwa kufuata taratibu zote za *TFF.* Marekebisho ya Katiba yafanywe kwanza. Baada ya hapo ndipo Uchaguzi Mkuu ufanywe kwa kuzingatia Katiba na maagizo ya *FIFA.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuwasilisha. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Serikali mna maneno yoyote?

**NAIBU WAZIRI WA KAZI, MAENDELEO YA VIJANA NA MICHEZO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa hoja hii ya Kamati ya Bunge ya Maendeleo ya Jamii kuhusu Katiba ya Shirikisho la Mpira wa Miguu Tanzania inagusa maeneo mengi yakiwemo ya *TFF,* Msajili, BMT na busara za Waziri mwenye dhamana ya michezo katika maamuzi yake na kwa kuwa wadau mbalimbali wa soko nchini wanavunjika moyo na hoja hii naomba ufafanuzi wa Mheshimiwa Waziri wa Kazi, Maendeleo ya Vijana na Michezo utolewe katika mkutano ujao. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, Mheshimiwa Waziri anaomba muda aweze kujibu hoja hii. Nafikiri Mheshimiwa Waziri amezingatia kwamba hiyo tarehe ya Desemba Kamati inayosema itakuwa Bunge halijakaa. Nadhani watatumia bidii ya kuweza kutoa hoja yao kabla hatujaahirisha. Kwa hiyo, sasa nitawahoji kuhusu Hoja ya Kuahirisha Bunge mpaka kesho saa tatu asubuhi.

*(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

*(Saa 11.54 jioni Bunge liliahirishwa mpaka siku ya Ijumaa Tarehe 12 Novemba, 2004, Saa Tatu Asubuhi)*